ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
30. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi

33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini - Tarehe 16 Juni, 2016

(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani kauli ya Serikali kuhusu uhamasishaji wa uchangiaji katika upatikanaji wa madawati Zanzibar.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: (Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuhusu kauli ya Serikali inayohusiana na uhamasishaji wa uchangiaji katika upatikanaji wa madawati Zanzibar. Ahsante.

KAULI YA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha kauli ya Serikali kuhusu uhamasishaji wa uchangiaji katika upatikanaji madawati Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Skuli za Zanzibar hasa zile zinazomilikiwa na kuendeshwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa muda mrefu sasa zinakabiliwa na tatizo la upungufu wa madawati kwa ajili ya mahitaji ya wanafunzi wetu. Upungufu huo wa madawati umeathiri kwa kiasi fulani wa maendeleo ya elimu ikiwemo ubora wake kwa wanafunzi wetu wa skuli mbali mbali za hapa Zanzibar mjini na mashamba kutokana na baadhi ya wanafunzi wetu kukosa mazingira mazuri ya kujifunzia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutambuwa na kuguswa na hilo la upungufu wa madawati katika skuli zetu za Unguja na Pemba, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na jitihada anazozichukuwa katika kutatua tatizo hilo, ameunda Kamati ya Kitaifa kuhamasisha jamii, watu binafsi na taasisi mbali mbali kuchangia katika kutatua tatizo hilo. Kamati hiyo inaongozwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman,

Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Orodha kamili ya Wajumbe wa Kamati hiyo ni kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Haroun Ali Suileiman	- Mwenyekiti
2.Mhe. Riziki Pemba Juma	- Makamo Mwenyekiti
3.Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed	- Mjumbe
4.Ndugu Salim Said Bakhressa	- Mjumbe
5.Ndugu Abdulhafour Ali Muhammed	- Mjumbe
6.Ndugu Abdulrahman Mwinyi Mbegu	- Mjumbe
7.Ndugu Seif Nassor	- Mjumbe
8. Mhe. Mohammedrazza Hassanali	- Mjumbe
9. Ndugu Nayla Jidawi	- Mjumbe
10.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	- Mjumbe
11.Ndugu Abdulwakil Hafidh	- Mjumbe
12 .Ndugu Nassor Dachi	- Mjumbe

Mhe. Naibu Spika, Kamati hiyo imeanza shughuli zake za kuchukuwa hatua za uhamasishaji ili wananchi na Taasisi mbali mbali ziweze kuchangia katika kuondosha tatizo hili la madawati.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutambua nafasi muhimu waliyonayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika jamii yetu, Kamati hiyo ya Kitaifa imeona ni vyema ikawahamasisha Waheshimiwa Wajumbe katika hatua za kuondoa tatizo hili. Umuhimu huo wa nafasi za Waheshimiwa Wajumbe unatokana na uhusiano mkubwa ambao waheshimiwa wameujenga baina yao na wananchi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, jambo hili ni letu sote, hivyo, ni vizuri viongozi wote kuanzia Shehia, Majimbo, Wilaya, Mikoa na Mashirika ya Serikali, Watu binafsi pamoja na wafanyabiashara popote wale walipo ndani na nje ya Zanzibar tukachangia suala hili ili kuunga mkono jitihada za Serikali yetu za kupunguza tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa, tatizo la upungufu wa madawati linatuhusu sote wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako Tukufu. Jitihada za kuliona tatizo hili zitasaidia jamii yote kwa ujumla wake wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako ambao tatizo hili linawagusa sana majimboni mwao.

Mhe. Naibu Spika, kwa mnasaba huo, Kamati hii iliyoundwa na Mhe. Rais, inawasilisha pendekezo maalumu la kuomba tatizo mbele ya Baraza hili tukufu kwa kuzingatia kuwa dawati moja linagharimu kiasi cha Tanzania Shilingi laki tatu, endapo kila mjumbe wa Baraza atashajihisha wananchi wa taasisi mbali

mbali katika jamii inayotuzunguka pamoja na yeye binafsi kuchangia upatikanaji wa madawati angalau kumi kwa kuanzia yatakayogharimu kiasi cha Tanzania shilingi milioni tatu, basi kwa umoja wetu chombo hiki kikuu cha Uwakilishi wa wananchi kinaweza kutupatia madawati mia nane na hamsini yatakayogharimu jumla ya Tanzania shilingi milioni mbili na hamsini na tano.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapendekeza kuwa kila Mjumbe ambapo sote tumo humu ndani ahamasishe na kuchangia kiasi hicho kwa awamu tatu, kwa maana kwamba kila awamu achangie kiasi cha Tanzania shilingi milioni moja katika kipindi cha miezi miwili na hivyo, baada ya kipindi cha miezi sita jumla ya madawati mia nane na hamsini yatakuwa yamepatikana na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo hili la madawati.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu mkubwa wa kuwajengea watoto wetu mazingira mazuri ya kujifunzia, kamati inawaomba sana sana sana Wajumbe waunge mkono jitihada hizi za Serikali chini ya uwongozi wa Kepteni mahiri Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Muhammed Shein kwa kuchangia na kuhamasisha uchangiaji wa ununuzi wa madawati haya. Kwa pamoja Waheshimiwa tunaweza kulitokomeza janga hili.

Mhe. Naibu Spika, Naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, sasa tumpishe basi Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: (Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kuzungumzia suala zima la kauli ya Serikali kama alivyowasilisha Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhusu uhamasishaji wa uchangiaji katika upatikanaji wa madawati Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lazima tutowe pongezi za dhati kabisa kwa Serikali kuhusu kauli hii iliyokuja nayo ya uhamasishaji wa uchangiaji katika suala zima la upatikanaji wa madawati Zanzibar.Ni kweli usiopingika kwamba wanafunzi wetu wameshajihika sana kupelekwa maskuli na wazee na kwa kweli nafasi imekuwa ndogo ya kukaa kwenye vikalio.

Kwa hiyo, suala zima la upatikanaji wa madawa ni suala la msingi sana na kama Kamati sisi tumetafakari, tumeona hii kampeni ambayo Mhe. Rais, amekuja nayo ni ya msingi kabisa na tunampongeza sana kwa kuwa na muono

wa mbali, yaani *broad vision* katika suala zima la elimu nchini mwetu. Na tumekuja hasa kulinganisha yaani kufanya *linkage* pamoja na ile adhma nzima ambayo au *theme* waliyotoa Wizara ya Elimu yenyewe kwamba; 'Elimu Bora Kwanza' na tunaposema elimu bora kwanza lazima tuwalee watoto wetu au tuwafunze watoto wetu, niseme wabadilike, maana watoto wengi sasa wamezoea kuandika chini, tena hata wewe ukimpa kalamu tu basi juu ya meza wengine hawawezi, ataondoka juu ya meza aende chini kwa sababu ya kule tulikotoka, sasa lazima tuwabadili kutokana na muelekeo huo, na hiyo hasa imetokana na kukosa madawati. Kwa hiyo, kauli hiyo ya Serikali sisi kama Kamati tumeitafakari kwa kina kabisa na tunaiunga mkono kwa asilimia mia moja.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wa Kamati naomba niwasisitize tena muwafahamu, Mwenyekiti ndiye mimi hapa ninayezungumza, halafu Makamo Mwenyekiti Mhe. Tatu Mohammed Ussi, Mjumbe Mhe. Ame Haji Ali, Mjumbe Mhe. Hidaya Ali Makame, Mjumbe Mhe. Makame Said Juma, Mjumbe Mhe. Masoud Abrahman Masoud, Mjumbe Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Makatibu wetu Ndugu Aziza Waziri Kheir na ndugu Khamis Hamadi Haji.

Mhe. Naibu Spika, katika kutafakari kauli hii ya Serikali, tumehisi Kamati tuende kidogo kitaalamu, yaani twende *in scientific approach*, hili suala twende nalo kitaalamu zaidi,yaani kimipango zaidi. Kwa nini nikasema hivyo, ukiangalia kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri, tuliyoipitisha juzi ukurasa wa saba, naomba nikariri. Amezungumza kwamba; "taratibu za manunuzi ya madawati mia tatu thalathini kupitia mfuko wa kodi ya bandari na madawati 926 ya Milele Zanzibar *Foundation* zinaendelea na taratibu zikikamilika madawati hayo yatasambazwa katika skuli ya Abdalla Sharia iliyopo Tomondo, Bandamaji, Kiboje na skuli ya Kidoti kwa unguja na skuli ya Michakaeni, Jadida, Birikau, Msuka na Uwandani kwa Pemba".

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Mhe. Waziri, naomba nim-*quote;* "Jumla ya madawati 315 ya wanafunzi, viti 27 na meza 27 kwa walimu vimenunuliwa kwa ufadhili wa *SIDA* na vimesambazwa katika skuli ya Donge Mtambile, Zingwe Zingwe na Kinuni kwa Unguja na Tumbe, Kilindi na Pujini kwa Pemba".

Mhe. Naibu Spika, Kamati inauliza tu, je, lengo hili lililowekwa miaka kumi na tano kumi na sita limekamilika na limetimizwa kama alivyoelezwa Mhe. Waziri. Ingekuwa vizuri akalijuilisha Baraza Mhe. Waziri, juhudi hizi ambazo za awali Serikali yetu imezifanya tumefikia wapi, tuko wapi na nini malengo

yetu ya mbele. Na katika malengo ya mbele ukiangalia bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha, anasema kwenye uchambuzi wa bajeti mwaka huu mapato yaliyotengewa matumizi maalum kuna ruzuku Bodi ya Mapato, ruzuku ya Mfuko wa Barabara, ruzuku ya Vyuo vya Amali na Madawati shilingi bilioni moja.

Mhe. Naibu Spika, sasa ninataka kujuwa bilioni moja hizi Mhe. Waziri, amezipanga kununuwa madawati mangapi na kwa utaratibu gani na usambazaji wake umeshapangwa vipi, yaani ndio kama ninavyosema iko haja kauli ni nzuri, Kamati inaikubali, lakini twende Mhe. Naibu Spika, kitaalamu zaidi, *more scientific approach* kulikabili suala hili ambalo ni letu sote, hili ni suala letu sote, hakuna mjadala hili. Mhe. Rais, tunamshukuru sana kwa muono wake na maelekezo yake.

Mhe.Naibu Spika, vile vile, naomba kuzungumza suala zima la *sustainability* ya hili suala.Kuna kodi ya bandari inayokusanywa kwa madhumuni haya kama nilivyosema. Kodi hii inakusanywa takriban huu mwaka wa tatu. Mhe. Waziri, atuambie kodi hii kwa miaka mitatu, je, madawati mangapi yameshanunuliwa au kama alivyosema ya mwaka tumepata *figure*, je, hizo *figures* za nyuma na yamesambazwa wapi? Itakuwa vizuri tuanzie pale nguvu zetu wenyewe za Serikali ambazo tunathamini sana, nguvu zetu wenyewe tushazianza halafu ndio tushajihishe na jamii. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali na orodha hii ya Waheshimiwa waliotajwa pia tunawapongeza na tunasema tu iongezwe kundi la Diaspora wa Zanzibar, ni watu nao muhimu sana, humu hawakutajwa nao wanashajihisha sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia hata ndio itakuwa kazi ya Kamati hiyo, lakini suala zima la wenye Mahoteli, kama kwetu kule mfano Fumba kuna Hoteli ndogo tu mbili lakini tumewaomba madawati, *alhamdullillahi* tumejaza skuli zetu za Bwefumu pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa, kimsingi Kamati haina pingamizi na wazo hili, tunaiomba tu Serikali kwanza tutumie vyanzo vyetu wenyewe ili *top up* hii juhudi ambayo tunaitaka kuifanya.

Mhe. Naibu Spika, lakini la mwisho ninaomba tutafakari zaidi suala zima la kuchangia Waheshimiwa, shilingi milioni tatu, suala zuri kila mmoja wetu anapenda kusaidia jimbo lake na kitaifa kwa jumla, lakini tukiangalia majukumu ya Waheshimiwa katika majimbo yao, kwa hiyo, Kamati inashauri kwamba, Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, waendelee na mpango huu wa milioni tatu. Waheshimiwa Wawakilishi, wengine iwe asilimia hamsini ya hapo, huo ndio ushauri wa Kamati Mhe. Mwenyekiti na naomba kuwasilisha. Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Sasa basi kwa mujibu wa kanuni zetu kauli ambayo inatolewa na Serikali inaweza kwa mujibu wa atakavyoamua aliyekaa kwenye kiti inaweza kujadiliwa na inaweza kuchangiwa, sio kuchadiliwa, kuchangiwa na baadae sasa Mheshimiwa, kuuliza masuala na baadae Mheshimiwa, anaweza vile vile kunanii, hiyo ni kanuni ya 43 ambayo inatoa ruhusa hiyo.

Kwa hiyo, kama kutakuwa na mchangiaji labda mmoja ni masuali, ni masuali ambayo sasa kwa mfano kama anaweza mchangiaji mmoja, wamejitokeza watu wawili lakini nimemuomba Mhe. Razza, ametaka kuchangia hotuba na vile vile, ametaka kuchangia hotuba ya Ardhi na ametaka kuchangia hii.Lakini nakuomba uamue moja uchangie kwa sababu ya muda wetu hatuna na wachangiaji sasa hivi wa hotuba ya Mheshimiwa wa Ardhi ni 30 wameshafika, kwa hiyo, kama unataka kuchangia hii ina maana kwenye hotuba ya ardhi hutapata tena nafasi ya kuchangia Mheshimiwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba uulize maswali umuulize Mhe. Waziri.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia kidogo na kuuliza maswali mawili.

Mhe. Naibu Spika: Ni maswali, sio kuchangia, mimi nilikuwa nimesema uchangiaji tu imenipitikia, ni maswali.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, ahsante. Mimi naipongeza taarifa hii muhimu kwa ajili ya wanafunzi wetu, lakini katika taarifa hii Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, alisema kwamba kuna madawati kupitia Mfuko wa Bandari na *Milele Foundation*. Katika 330 na 926 utapata 1,256. Je, haya yana uhakika yatapatikana. Kama yatapatikana gharama ni kiasi gani.

Kwa ujumla nataka kumuuliza tu Mheshimiwa, ili tufanikishe zoezi hili kwa Zanzibar nzima Unguja na Pemba ni madawati mangapi yanayotakiwa katika skuli zetu ili kuondoa hii adha ya kila siku isitufike tena katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Unajua hivi karibuni zoezi kama hili lilifanyika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na liliendeshwa na *Channel Ten* na kwa masikio na macho yangu nilimuona Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Benno Ndulu alitoa zaidi ya

shilingi mia mbili na arobaini na kitu zaidi na akazungumza pesa au madawati yale yatayopatikana pale yatagawiwa katika pande zote zenye taasisi ya *BoT* ikiwa Zanzibar ni wadau. Je, katika mgao ule tumepata kiasi gani.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, nina swali dogo la kuuliza, kwa kuwa mara nyingi watu wanapotaka ku-*donate,* maana yake katika hapa mtu alizungumza kuhusu hii ripoti Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwamba, washirikishwe watu wa Diaspora na wengine. Nilikuwa nataka kufahamu tu, mara nyingi watu wanapo-*donate* vitu kama vya *desk* wanakuwa na kumbukumbu hasa hawa watu wa Diaspora wanakuwa wanapenda ku-*donate* mambo kama haya katika zile skuli ambazo wamesoma. Je, haya madawati ambayo mtu akitaka kuamua ku-*donate* anaweza kuandika nembo ya kampuni yake au jina lake kule nyuma. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Shera, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, mimi naomba ruhusa kidogo kwa sababu nimebahatika kuwa ndiye mwenyekiti wa hii kamati, niendele kutoa maelezo mawili matatu kuongeza nguvu katika jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, kwanza niishukuru sana hii Kamati ya Mwenyekiti Dkt. Mwinyihaji Makame, kwa maelezo yao mazuri sana na sioni ajabu kwa sababu mwenzetu ni msomi mzuri, yeye mwenyewe kaja *very scientific* na ninamhakikishia kwamba kamati yetu italitafakari sana jambo hilo na kulichukulia hatua kama alivyopendekeza.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili nataka niwaambie sote tuna majimbo, tuna maeneo yetu ya wilaya na mikoa huko, hata kama kuna Mfuko wa nini; kama wa Bandari, *Milele Foundation* na taasisi nyengine bado tatizo la madawati halitotosheleza mahitaji yetu kwa sasa hivi. Kwa sababu upungufu wa madawati uliopo Zanzibar ni karibu 47,000; sasa dawati moja kama lina *cost* karibu shilingi 300,000 ukiifanya hesabu ya madawati 40,000 peke yake tunahitaji pesa nyingi sana. Kwa hivyo, hili ni sehemu au ni jambo la kuchangia tu huu Mfuko wetu na nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu, kwa taarifa hii aliyotuletea hapa na tumuunge mkono Rais wetu kwa sababu jambo hili linatugusa sote, watoto wetu wanaumia sana.

Mimi mtoto wangu mwenyewe mpaka darasa la nane anaandika chini na ilikuwa kazi kama alivyosema Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kweli, alikuwa anasema kwamba mtoto yule hata ukimpa karatasi ya kuandika basi atatafuta mahali alale hata kama pana meza na kiti nyumbani hafanyi, ni kweli. Sasa tuondokane na tatizo hili, wanaumia watoto na wanaathirika sana tusiendelee

kuwaachia watoto wetu nafasi hii wakaumia, tuchangiane, tukichangia sisi na huko majimboni kwetu mambo yatakuwa mazuri, nakuhakikishieni kwa sababu ni sadaka nzuri hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mheshimiwa, mmoja alisoma hapa, nasaidia kidogo hapa, kwamba mtu akileta dawati akitia nembo, muhimu nembo ile isije ikakera mpaka pale anapokaa yule mwanafunzi tu akawa hana pa kukaa, lakini nembo ibandikwe kwa kuweka kama ni suala zima la kampuni yako kuwa imechangia hakuna matatizo na inawekwa nembo ndogo au mahala padogo ambapo panaweza pakaridhisha. Lakini ukija ukiweka nembo saizi ya fenesi itakuwa kazi kubwa tena, hata pa kukaa hapaonekani. Kwa ujumla mimi nasema tumpongeze sana Mhe. Rais, kwa hatua hii aliyokuja nayo na tuiunge mkono.

Pendekezo la Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, hatulitolei uamuzi moja kwa moja sasa hivi kwa sababu itabidi tukae kwenye kamati tushauriane zaidi, lakini Mhe. Waziri, mwenyewe atatoa uamuzi akihisi inafaa hakuna matatizo. Lakini tumuunge mkono Waziri wetu wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sababu jambo hili lina maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, tumesema tulikuwa na pendekezo nishauri tu, kuna wengine walisema labda tunasemaje tukatumia Mifuko ya Jimbo. Mifuko ya Jimbo ni mizuri lakini kuna tatizo kuwa kuna baadhi ya Waheshimiwa wengine hawana majimbo hapa, hilo la kwanza. Lakini la pili Mfuko wa Jimbo si kwa ajili ya kununua ma-*desks* tu Mfuko wa Jimbo tuna tatizo la maji, umeme, kilimo, mifugo na mambo mengine.Kwa hiyo, tukasema maamuzi hayo mwenyewe Mwakilishi na kamati yako utaamua, ukiamua katika sehemu yako ya Mfuko wa Jimbo umege kidogo ulete huku ili kuchangia basi hiari yako hakuna matatizo, lakini tunachotaka hapa Barazani sisi tukukate kwenye pesa zako kila mwisho wa mwezi kwa mujibu tulivyokubaliana kama shilingi laki tano au milioni moja utasema wewe mwenyewe, lakini zibakie pesa katika Mfuko na tutazifungulia *account* maalum ambayo haitoingiliwa na mtu mwengine yeyote, itasimamiwa na kamati yenyewe pamoja na ushauri wa Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa nashukuru sana Wajumbe, lakini nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Vile vile, tumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Madawati, Waheshimiwa wenzangu labda niseme tu kwamba mimi na Naibu wangu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tunapokwenda katika ziara zetu maskulini changamoto kubwa sana ambayo tunakutana nayo ni tatizo la madawati. Unapokwenda katika skuli nyingi na skuli nyingi ambazo tumekwenda na bado tutaendelea kwenda, ukifika unaambiwa Mheshimiwa 'darasa letu lione zuri sana limejaa madawati'. Kwa kweli limejaa madawati, maana yake ni kwamba hamna kitu na hamna hata ile meza ya kukalia mwalimu na kiti hamna.

Kwa hivyo, kwa kuona hilo Mhe. Rais, ndio akaona ipo haja ya kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa sana kuunda kamati hii, lakini akiamini kwamba Baraza lake tukufu ambalo lipo linaweza kumsaidia na kumuunga mkono juu ya kadhia hii ambayo inaikumba nchi yetu,lakini kadhia ambayo inawakumba watoto wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa wenzangu niwaombe sana kwamba, kitoa ni moyo si utajiri, tunapochangia hili ni kwamba tumechangia taifa letu lakini tumewachangia watoto wetu. Kumuona mwanao anatoka nyumbani anakwenda skuli anakaa chini sidhani kwamba wewe mzazi unafurahi, unakuja hapa kiti kizuri unazunguka huku na huku, *AC* nzuri, lakini kule mtoto yeye anapokwenda skuli anakaa chini, si jambo la busara sana na hasa kama uwezo huo tutakuwa tunao. Sote ni masikini lakini ule uchache wetu utuunganishe ile 'haba na haba' basi kibaba kikajaa.

Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu tumuunge mkono Mhe. Rais, kwa kuliona hili na umuhimu wake lakini tukizingatia kwamba watoto wetu ndio ambao wao kesho na keshokutwa watakuja kukaa katika viti hivi, tusipowajengea mazingira mazuri sasa kwa kweli ule ufanisi ambao sisi tutategemea wakati huo tushakuwa tuko majumbani watu wazima unaangalia Baraza, unaona watoto kwamba kisaikolojia hawako sawa kwa kweli itakuwa sio jambo la busara.

Mhe. Naibu Spika, sasa tuwarithishe watoto wetu mambo mazuri yakiwemo kuwapa elimu bora, lakini pia katika mazingira salama na mazuri. Mazingira mazuri haya pia yanajengwa na uwepo wa vikalio ndani ya madarasa, mwalimu ukikaa chini, wanafunzi wakikaa chini ufanisi wa elimu hautakuwa mzuri na ufauli vile vile hautakuwa mzuri. Sote tunafahamu kwamba elimu ndio mpango mzima, kila kitu ni elimu, bila ya elimu sidhani kama pengine tungeweza kuandika angalau jina letu. Hivyo, tukilithamini na tukiliona hilo basi niwaombe sana tumuunge mkono Mhe. Rais. Lakini hili sio sisi tu ambao tumo

humu ndani, lakini hata ambao wako nje, kama tulivyoainisha katika ile *paper* yetu ni kwamba wafanyabiashara wadogo na wakubwa wote wanapaswa kuliunga mkono jambo hili. Mtu akisema mimi nina uwezo wa kuchangia dawati moja basi kwa kweli ule utakuwa ni mchango mkubwa sana, si lazima achangie madawati 50, akisema lile moja, mwengine moja na mwengine moja tukichanganya hayo tayari ni 11, sasa 11 na mengine 11 na wengine 11 tayari tutakuwa tuna hesabu nzuri sana.

Waheshimiwa wenzangu Wizara yetu ya Elimu inajitahidi sana na kwa bahati nzuri bajeti tumeipitisha hapa wameona kiwango kilichoandikwa. Wizara yetu ni kubwa, bajeti ambayo tumewekewa haiwezi kutosheleza hata madawati 20 na tukisema tunachonga madawati, ina maana hatuwezi kulipa walimu mishahara, hatuwezi kufanya shughuli nyengine yoyote ambayo itasaidia katika sekta ya elimu kwa kutumia bajeti ambayo tumeidhinishiwa hapa. Lakini ili tuweze kufikia malengo, ili tuone kwamba kizazi chetu kinarithi ile elimu bora na vile vile, kuona kama yale malengo ya *Millennium* pia vijana wetu nao yanawafikia basi tuanze na kuwasaidia angalau kupata madawati.

Kwa hiyo, Waheshimiwa, kwa umoja wetu hili tunaweza sana, nguvu ya pamoja inajenga maendeleo ya nchi, lakini nguvu ya Waheshimiwa kwa umoja wetu na tukiungana na walio nyuma yetu tunaowawakilisha basi 'Elimu Bora Kwanza' tutaifikia. Na ili wale warithi wetu warithi vizuri, akili zao ziwe vizuri, elimu bora waipate basi tuanze na hili. Niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu ni kwamba, tumuunge mkono Mhe. Rais, lakini vile vile tuiunge mkono Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuona kwamba tunachangia kile ambacho tunapaswa kuchangia. Kutoa ni moyo, unapotoa wewe ni kwamba umemsaidia mwanao, mtoto wa ndugu yako, wa kaka yako, lakini vile vile umeisaidia jamii na taifa lako. Kwa yeyote ambaye atakuwa na moyo na kaguswa na hili basi tunamuomba sana achangie madawati ili kuona kwamba watoto wetu wanakaa katika mazingira mazuri na salama.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, malizia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsanteni sana nina imani kwamba tutaungana mkono juu ya hili. Mhe. Naibu Spika, ahsante.(*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii. Najua niliuliza swali wenzangu wote wamejibiwa maswali yao, lakini mimi

mpaka sasa hii sijajibiwa swali langu kuhusu hili suala la madawati. Naomba nijibiwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, sio kama tumelidharau lakini hii taarifa ya kwamba Gavana kachangia pesa hizo, si jambo ambalo naweza nikalitolea uamuzi hapa. Hii kauli nzito na hapa ni Barazani mahala pazito, lakini kama kauli hiyo imetoka nitashukuru sana na tutaifuatilia kama kamati na *in shaa Allah* mgao wetu kama upo tutaupata tukijaaliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na nimshukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Hata mimi nilimsikia Gavana wa Benki Kuu wakati anapewa fedha za mchango kwa ajili ya madawati na kauli ya Gavana alieleza kwamba ziko fedha zitakazotumika kwa Jamhuri ya Muungano na liko fungu litatengwa kwa Zanzibar, lakini alisema Serikali ya Zanzibar ndio itaamua hilo fungu litumike vipi. Kwa hiyo, pia, tutaishauri serikali tuhakikishe kwamba fungu hilo nalo litumike kwa ajili ya ununuzi wa madawati. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea katika orodha yangu nina Wajumbe 32 na tunatakiwa tumalize leo. Sasa ningewaomba wengine waanze kujitayarisha kwa kupeleka kwa waziri kwa maandishi ili tuweze kurikodi na masuala yao yaweze kujibiwa. Nawaomba sana kwa sababu haitowezekana hata siku moja kuwapa nafasi watu wote 32 kutokana na muda wetu tuliopangiwa. Hilo moja.

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabla ya kuanza hili nimeletewa kikaratasi hapa na Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali na katika lile suala letu la madawati amenitaka nitangaze rasmi kwamba ameunga mkono juhudi za Mhe. Rais na kwa hivyo, atatoa madawati 200 kwa niaba ya familia yake. Kwa hiyo, Mhe. Mohammedraza Hassanaali, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuwa mtu wa awali katika kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa siku ya leo. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya kuweza kusimama leo hii katika Baraza lako tukufu ikiwa swaumu ya kumi.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kabisa na kuwapongeza sana watendaji wa wizara hii kwa uwasilishaji wao mzuri sana, uliotukuka, wenye mbwembwe na madaha pamoja na kuwa na kitabu kizuri na mwenendo mzima wa wizara hii, kwa sababu ni wizara ambayo inagusa moja kwa moja maslahi wa wananchi wa Zanzibari wa nchi hii. Sasa niende katika mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 14 juu ya suala zima la Mahakama ya Ardhi. Pamoja na pongezi zilizotolewa juu ya suala zima la Mahakama ya Ardhi inafanya vizuri na inastahiki kupongezwa, vile vile, ina changamoto zake. Ile Mahakama kwa kweli sehemu, ofisi yake haiendani na hadhi ya taasisi ile. Taasisi ya ardhi ni nyeti sana lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu ambayo hayaelezeki; imefika wakati Mhe. Waziri, hata makaratasi ya kuandikia hizo kesi yanashindikana, ni kitengo cha serikali na ni Mahakama ya serikali kwa ajili ya maslahi mazima ya kudhibiti ardhi ya nchi yetu hii. Ardhi ni mali, lakini wale watendaji wa wizara ile kwa kweli sifa zao ziko tafauti.

Sio hilo tu, hata Sheria za Srdhi nyingi zao zimepitwa na wakati ni sheria za muda mrefu sana. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie na hilo ili tuweze kuzibadilisha hizi Sheria za Ardhi ili ziendane na wakati wa sasa wa *globalization* tunaokwendao, *unless*, *otherwise*, kama sio hivyo itakuwa siku zote tuna-*make time* hatuwezi kufika mbele tutakuwa tunajisifu tu kuwa tuna vyombo vizuri lakini utendaji wake unakuwa hauonekani. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri, hilo suala alichukue na alifanyie kazi haraka iwezekanavyo ili tuweze kujua changamoto zake zinakwenda vipi kwa kuja kuwasaidia wale wenzetu wa Mahakama ya Ardhi.

Kuna tatizo la ma-*assessors*, walikuwa na ma-*assessors* katika Mahakama zile lakini cha kushangaza sasa hivi imefika wakati hata wale ma-*assessors* ambao walikuwa wanapewa hicho kidogo siku hizi wamekatishiwa hawapewi na wale ni washauri wazuri tuwajali katika suala zima la ardhi. Namuomba Mhe. Waziri, hilo suala aliangalie na nafikiri sijui imekuwa kuwaje zile haki zao wanazodai wale wa-*assessors* kuwapa wakati ngumu katika zile kesi kutohudhuria kwa sababu wanaona hamna wanachokitapa, kiwango chenyewe

kilikuwa ni kidogo sana lakini hata hicho kidogo kimekuwa sasa hivi hakitoki. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, langu kwa upande wa ardhi ni hilo.

Nitakwenda kwenye *ZAWA*, ukurasa wa 24 katika ukurasa huu tumeona bajeti yao nzuri sana hapa na mahitaji yao makubwa sana ya kukusanya bilioni 5.1 nafikiri mpaka 2015/16. Lakini mpaka dakika hii ndio kwanza wamekusanya 1.9 kuna *difference* kubwa sana ambayo haijakusanywa na haijapatikana na muda wenyewe uliobakia haupo. Nadhani huu ni udhaifu nathubutu kusema, kwa sababu maji ni biashara na hayo mapato yao yalikuwa yanapatikana katika huduma hii ya maji na hii inatokana kwamba katika vitabu hivi tunavyokuja kusomewa hapa tunasifiwa vizuri sana, tunaambia kuwa upatikanaji wa maji katika miji yetu au maeneo yetu asilimia 87 mjini na silimia 70 vijijini, hayana ukweli na ndio manaa hesabu za humu zinakuwa *wrong*, yaani haziendani, haiwezi kufika hapa 50 *percent* ya mapato ambayo wanayokusanya kwa sababu ya maelezo yaliyokuwa hayana ukweli na uhakika wakati mnapokuja kutuelezea.

Mlituelezea kipindi kilichopita juu ya hotuba aliyosoma Mhe. Rais, juu ya suala la maji, *ZAWA* tukaambiwa kwamba usambazaji wa maji katika mji wa Zanzibar ni asilimia 87. Lakini nathubutu kusema mimi kwa hesabu zangu ndogo ilikuwa tuseme tu kwa usambazaji wa maji katika mji wetu haujafika asilimia 50. Kwa sababu mimi nina vigezo na ni Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe na katika jimbo langu nina Shehia zangu 5 upatikanaji wa maji ya *ZAWA* katika eneo lile ni jibu.

Nathubutu kusema nina sehemu moja tu ambayo kidogo ninaweza kujinasibu kwamba napata maji ya *ZAWA* kwa asilimia ndogo sana na hiyo kutokana na juhudi zangu mimi mwenyewe binafsi za kuweza kununua vifaa vile na kuweza kuzibua sehemu ambayo baadhi ya wafanyakazi wako walizifunga kwa makusudi mazima kwamba hawajapewa kitu kidogo.

Kwa hivyo, hizo changamoto za *ZAWA* zipo nyingi Mheshimiwa. Pengine kwenye vianzio vyetu vya maji tunaambiwa kuwa maji hamna lakini pengine si kweli. Maji pengine yapo ya kutosha angalau kufikia hiyo asilimia 87, lakini siyo yanayowafikia wananchi wetu.

Tunajua kwenye maji kuna miradi mingi sana hapa, ulikuwa mraji wa *JAICA* Japani, mlichimbwa mashimo mote humu kuanzia Welezo mpaka mjini, lakini mpaka dakika hii utokaji wake wa maji ndio kama unavyouona haufahamiki. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa, kidogo katika hili uje unieleze kidogo na

unifahamishe na mimi niweze kufahamu juu ya zoezi zima la upatikanaji wa maji katika mji wetu.

Nikienda mbele nitakwenda katika suala zima la *ZECO* katika ukurasa wako wa 34. *ZECO* ni taasisi ambayo inayoshughulika na biashara ya umeme katika nchi hii, ni shirika pekee ambalo linashughulikia na biashara hiyo ya umeme. Lakini shirika lile sasa hivi limekuwa na matatizo, huduma zile za Shirika la Umeme hazitolewi bure, ni shirika ambalo la biashara kwa umeme kwa mujibu wa mahesabu yake tumeyaona. Lakini cha kushangaza kama ni Shirika la Umeme imefika *time* sasa hivi wananchi wetu wanakwenda kulipa umeme kutaka kuunganishiwa umeme wanakaa zaidi ya miezi mitatu au minne hawajapatiwa mita, mita za umeme hakuna ile ni biashara. Sasa kama una biashara na unakwenda kwenye duka unakwenda kununua kile kitu hamna, je, yale makusanyo utayapata.

Kwa hiyo, *ZECO* ni tatizo juu ya suala zima la vitendea kazi kwa masuala ya kuunganisha umeme, ni tatizo la muda mrefu sana. Kama nikienda mimi kutokana na *status* yangu naweza nikapewa. Lakini hawa wapiga kura wetu wananyanyasika sana juu ya upatikanaji wa mita za TUKUZA, watu wameshalipa mita miezi miwili, mitatu mpaka dakika hii Mheshimiwa, bado tatizo hawajapata mita zile. Naomba utakapokuja hapa unielekeze namna gani tatizo hili linatokea na kuna utaratibu gani, basi kama tatizo kubwa sana na wewe Mheshimiwa, uje na wazo kama alivyokuja nalo Mhe. Waziri wa Elimu, ili kuondokana na tatizo hilo. Kwa sababu umeme ni mwanga na tunahitaji na huwezi kuona 'nyota bila ya kuona giza'.

Kwa hiyo, tatizo hilo lipo Mhe. Waziri, naomba sana utakapokuja unifahamishe na si kwa hilo tu, kuna tatizo kubwa sana la Shirika la Umeme la watendaji wake kulalamika juu ya suala zima la maslahi yao. Kuna suala la mafao ya mkataba, kuna watu 67 ambao mpaka dakika hii wanadai mafao ya mkataba wao. Lakini miongoni mwa watu hao kama 67 wengineo wameshalipwa mafao hayo, sijui kwa kipengele gani, sijui kwa sheria gani ambayo hao wengine walipwe na wengine wasilipwe katika shirika lile lile moja, watoto wa baba mmoja lakini wengine wanapendwa zaidi wengine hawapendwi. Kwa kweli hawatendewi haki na hiki kimekuwa kilio cha muda mrefu sana.

Mhe. Naibu Spika, hapa nilipo nina nyaraka juu ya suala hilo ambayo ya ripoti ya madai hayo ya mkataba wa wafanyakazi 67 wa *ZECO*. Kwa hisani ya Mheshimiwa Meneja wa shirika lile aliunda kamati kabisa kuna wajumbe hapa zaidi wa 5 kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, niwataje kama itawezekana:-

1. Mohamed Haji Nassor
2. Zamir Ali Mselem
3. Omar Salim Ali
4. Ahmed Khamis
5. Abdalla M. Juma
6. Abass Juma Khamis

Mhe. Naibu Spika, imeundwa kamati hii kwa kadhia nzima juu ya suala lao hili la mafao yao katika mkataba ambao mkataba huu ulikuwa ni mkataba walioingizwa baada ya kuthibitishwa kazini. Kuna watu wamefanyakazi miaka 7, miaka 6 na 8, lakini walikuwa hawajapa mkataba wa kuidhinishwa kazini kwamba, ni wafanyakazi wa kudumu katika shirika. Mara baada ya kuingizwa kule tu wengine wale hawakulipwa mafao ya miaka ya nyuma.

Mhe. Naibu Spika, Sasa nitaomba Mhe. Waziri, utakapokuja unieleze na hili tatizo si kubwa sana limekwenda vikao si kimoja, wala viwili, wala si vitatu mpaka ukatoka ushauri kwamba, hawa watu walipwe. Kutokana na mtu mmoja tu na *interest* ambaye huyu ni Mwanasheria ndio akaona kwamba, bila ya mimi kujua mustakbali wangu mimi, mimi sitotia saini au ridhaa kwa Meneja mlipwe pesa hizi, ni mtu mmoja anazuia watu zaidi 67 kupata mafao yao ukilinganisha kwamba, lile ni Shirika la Serikali, wana wakati ngumu sana na wanafanyakazi ngumu sana watu wale, hawajali jua, wala mvua, wanapanda maguzo na wanatuvutia waya sehemu mbali mbali. Kwa hiyo, lazima hili suala Mhe. Waziri, uliangalie na uje na majibu mazuri ili mimi niweze kuridhika. Vyengine vyovyote bila ya kupata jibu ya suala hili mimi nitazuia shilingi yako tuweze kuangali mustakabali mzima wa suala hili linaendaje.

Si hilo tu, suala jengine kwa *ZECO* juu ya malalamiko ya watendaji wale wale wa *ZECO*. Kumekuwa na kilema cha muda mrefu sana watendaji wale wanapata ajali mbali mbali; wanapoteza viungo, wanaungua, wanalipwa shilingi laki tatu, tulinganishe kiungo cha binaadamu unakilipa thamani ya shilingi laki tatu kwa sababu gani, kuna wengi wameshapoteza viungo katika shirika lile na wengi wameungua lakini wanalipwa laki tatu kwa sababu gani?

Nafikiri Mhe. Waziri, ungetoa rai maalum kwa shirika lile labda wale wafanyakazi angalau wakapatiwa Bima za Afya na hii haina kikomo cha matibabu. Baada ya hapo nafikiri atapata Bima ya Afya mtu yule hata akipata ajali yoyote itamsaidia na huku shirika litamuangalia kwa upande mwengine.

Vile vile, nakwenda katika suala zima la kuuzwa kwa nyumba ya Sherika la Umeme. Shirika la Umeme lilikuwa na nyumba Mazizini pale, sijui ile nyumba

imeuzwa kwa taratibu gani, zimefatwa taratibu gani za mauziano na serikali. Naomba utakapokuja Mhe. Waziri, unijuulishe hii nyumba imeuzwa na imeuzwa kwa nani. Hizo taarifa za kuuzwa ninazo, kwa sababu katika watu ambao waliokuwa wanatumia nyumba ile nilikuwa nina mawasiliano mazuri na mtu pale na ndie alietoa zile taarifa. Kwa hiyo, imeuzwa kwa misingi gani na kawaida kitu cha serikali kinapouzwa unaambiwa wewe uliekuwa unatumia mwazo unaulizwa, je, hicho chombo unakitaka au hukitaki, kama ilivyokuwa vyombo hivi vya maringi mawili na manne vinapotaka kuuzwa tunaulizwa. Sasa hii nyumba sijui imeuzwa kwa mipango gani.

Vile vile, kuna malalamiko kwa wafanyakazi hawa hawa wa *ZECO* ambao walikuwa na kesi katika shirika lile. Kesi imekwisha, sasa ni mwaka wa nne na Mahakama imeshatoa amri kwamba walipwe lakini mpaka dakika hii bado hawajalipwa. Ni kero ya muda mrefu sana, ni miaka minne sasa kuna watu baada ya kupeleka kesi yao Mahakamani wameshinda lakini mpaka dakika hii bado hawakalipwa pesa zao na hii inaonekana kwamba, itatupa jipu kubwa sana mbeleni kwa sababu hizi siku zitahesabiwa tu mwisho wa siku itaonekana Shirika likatoa fidia kubwa sana. Baada ya kulipwa sasa hivi pesa hizi kidogo, lakini litakuja kulipa pesa nyingi sana Mheshimiwa. Kwa kuziokoa hizi pesa ningeomba Mhe. Waziri, ufanye ufanyavyo juu ya zoezi zima la kulipwa hizi pesa za huyu jamaa alienda Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, Nikiendelea mbele hapa hapa, mimi leo nipo na *ZECO* tu juu ya suala la makato ya mishahara. Mshahara uliopita mwezi wa Mei wafanyakazi wa *ZECO* wamekatwa pesa nyingi sana bila kuongezewa mshahara. Hapo nyuma walikuwa wanakatwa elfu 40, 50, 60 sasa hivi wamekwenda kukatwa mpaka laki moja na nusu na laki moja na thamani, sijui kwa hesabu gani iliyotumia ya kuweza kuwakata pesa hizo, kama *payee* nafikiri hata serikali imepunguza kutoka asilimia 13 kuja asilimia 9. Lakini si kwa mwezi huu litaanza hilo zoezi katika mwaka wa fedha wa Julai. Sasa sijui imeingiaje hapa mpaka hawa watu wakakatwa hizi pesa, nitaomba Mhe. Waziri, ukija unisaiadie katika suala hilo.

Vile vile, Shirika linalalamika kwamba kuna ahadi za Rais alizozitoa juu ya kuwaongezea mshahara wafanyakazi wale. Sasa ni miaka 10 wafanyakazi wa *ZECO* hawajaongezwa mshahara pamoja na ahadi za Rais alizozitoa nathubutu kusema kwamba, alitoa Makongwe katika uchimbaji wa Umeme, Mbuyutende na Kojani mpaka dakika hii imekuwa ni kilio, sijui kwa sababu gani hizi ahadi au anazozitoa Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tunazungumza ni nchi ya Kimapinduzi, ina maana ahadi anayosema Mhe. Rais inakuwa ni

amri, hizi amri hazitekelezwi, inaonesha kuna watu wako juu ya Mhe. Rais, ndio maana wanazipinga ahadi.

Imekuwa kilio cha muda mrefu sana ya kutoongezewa mshahara wafanyakazi wa Shirika la Umeme juu ya ahadi hizo mara tatu ambazo Mhe. Rais wa nchi hii tunamuamini na tunampenda sisi wenyewe kwamba, anatoa amri hii haitekelezwi, imekuwa ni kilio cha muda mrefu kama hapo nyuma tulikuwa tunaona vilio vya ng'ombe ikachukuliwa hatua ya haraka iwezekanavyo na hili suala Mhe. Waziri, nataka utakapokuja unambie je, hizi ahadi zimekuwaje, ni ahadi za muda mrefu, ni miaka 10 sasa hawa watu bado hawajapata nyongeza yoyote ya mshahara. Lakini cha kushangaza wanakatwa makato mikubwa kuanzia mwezi uliopia.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Vile vile, masuala mengi, mengi ambayo yapo katika shirika lile la *ZECO* kuna kadhia kubwa sana. Sasa hivi shirika halina mita, lakini la kushangaza kunajengwa ukuta wa mamilioni ya mapesa, sijui hata kama zimefuatwa taratibu au vipi, au ndio kama tunavyokurupuka tunaamua tu mtu akilala na akiamka anatoa mawazo yake, anafanya hilo suala na mambo yanaendelea.

Kwa hiyo, katika hicho mimi nitakuwa siko pamoja na wewe juu ya suala zima hili la *ZECO* na nitakuwa pamoja na wewe mara tu baada ya kuniridhisha na kunambia utekelezaji wake utaanza lini, hapo tutaendelea na masuala mengine.

Mhe. Naibu Spika, Nitagusia jengine kidogo suala zima la viwanja, viwanja vya nchi hii Mhe. Naibu Spika, imekuwa tatizo kama hujawa "Ibn Kinana, Ibn Mudirikata, Ibn Ilyasa" hupati kiwanja kiwanja nchi hii. Watu wanapewa viwanja wao kwa wao, sijui hawa wenzetu wana vigezo gani na hawa wengine wana vigezo gani wanaokosa. Nathutubu kusema mimi mwenyewe binafsi niliomba kiwanja cha nchi hii 1990 vimeshatoka viwanja si mara moja, wala mbili, wala tatu, sijui mimi nina kasoro gani ikiwa kama ni Mzanzibari wa nchi hii ambavyo nimekidhi vigezo vyote kiwanja kile sipewi, lakini ukienda unakuta wao wao tu siku zote "Ibn kinana, Ibn Mudirikata, Ibn Ilyasa". Je, inakuwaje hili suala? Nitamuomba Mhe. Waziri, uje unitolee ufafanuzi katika suala zima la viwanja.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii, asubiri majibu yangu kutoka kwa Mhe. Waziri. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu nashukuru kupata fursa hii na pia niwaamkie nyote *Assalam Alaykum* na wale ambao wazungu nawaambia pia *good morning*?

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kweli napenda kusema tu kwamba, kwa kweli wizara hii inanigusa sana hasa na wananchi wangu na zaidi nitakuwa na maswali, lakini nitamshukuru Mhe. Waziri, akifanya majumuisho ataweza kunijibu mengi ambayo nataka kuyajua.

Katika mpango mzima wa Jimbo ka Tunguu wa ukataji wa viwanja, ningependa pia ahakikishe tu kuwa kuna mambo mengi ambayo yanawahusu wananchi wangu katika maeneo ya uwanda hasa katika maeneo ya Tunguu, watu ambao wanaishi kwa muda mrefu, kwa hiyo, nitakuja kumuona zaidi katika suala hili.

Lakini pia kuna suala zima la viwanja kwamba kumekuwa na utaratibu Zanzibar wa kujenga kwenye viwanja ambao vinashika katika maeneo ya bahari. Lakini kutokana na ujenzi huu inasababisha viwanja au maeneo ambayo yako nyuma ya bahari kushuka *value* yake. Sasa ningeomba kujua wizara yake inajipangaje katika *planning* nzima ya kisiwa chote cha Zanzibar kwa miaka ya mbele, hivi viwanja ambavyo vinakuwa *devalued* ambavyo viko nyuma ya maeneo. Kwa sababu tunajenga kutokana na bila mpangilio.

Lakini pia ningependa kufahamu kuhusiana na visiwa ya *Prison Island* na Bawe juu ya ulipaji wa kodi. Nikiangalia kuwa sina uhakika kama hizo hoteli bado zina-*operate.* Lakini kwa fedha ambayo inalipwa hasa kwenye kisiwa cha *Prison Island* na pesa ambayo serikali ingeweza kupata hii ada hasa katika tunzo ya *interest fee* ambayo wana-*charge* dola 4 kwa mtu mmoja na ukizingatia na *lease* waliopewa, mimi naamini hichi kisiwa bado kuna mpango na kama inawezekana wangejaribu kufuatilia zaidi ni kitu gani ambacho kina mkwamo.

Lakini mimi mtizamo wangu unaelekea kwamba hichi kisiwa kingependa nafasi ya kuunganishwa pamoja na hoteli ya Park Hyatt ya Bwana Ali Baward ambayo ameekeza pesa nyingi sana katika Mji Mkongwe basi ingekuwa jambo zuri. Kwa hiyo, namshauri Mhe. Waziri, aangalie mkataba wa *Prison Island* kwa sababu mapato yanayopatikana ni madogo sana ya serikali na ikiwezekana aunde kamati ya uchunguzi ili aweze kujua zaidi.

Lakini pia nataka kujua kuhusu kampuni za mafuta ambazo zina-*supply* hapa mafuta Zanzibar. Ningependa kufahamu pia kampuni ambazo zinatumia mfumo mzima wa *BPS* wa kutoka Tanzania Bara ambao unaleta mafuta hapa na kampuni zipi ambazo zinachukuwa mafuta kutoka Mombasa ambazo haziko katika mfumo huu wa *BPS* na ni kwa nini wanafanya hivyo.

Lakini pia nina tatizo la maji katika jimbo langu na hasa katika *pump* kuingizwa na kutolewa. *Pump* yangu iliyokuwepo katika Kaebona Tungu ambayo ilikuwa inapeleka maji Uzi Ngambwa, Ungujaa Ukuu, Kaepwani A na B, Tindini pamoja na Kikungwi, hii *pump* imepelekwa wapi kwa sababu *pump* imekuwa ndogo. Lakini pia wakija jeshi kufanya mazoezi huwa wanapata maji, haya ni katika matatizo niliyokuwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, Lakini pia kwa upande wa Dunga na Bungi nimeshazungumza sana. Hasa haya matatizo ya *pump* bora Mhe. Waziri, ukija utueleze hapa, nafiki matatizo haya Wajumbe wengi wanayo matatizo katika majimbo yetu.

Mhe. Waziri, ningependa sasa uchukuwe kalamu, naingia kidogo katika kifungu cha Katiba. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, inasema kwamba:-

"Zanzibar ni nchi ambayo inaelewa mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyozunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ilikuwa ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar".

Ukienda katika Katiba ya Zanzabar inasema pia;

"Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yote yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo"

Sasa nikafanya utafiti kidogo, kwa sababu hapa nipo katika masuala ya mafuta na gesi nikaifuatilia Katiba ya mwaka 1963 ambayo ni katiba bandia tuliyopewa na Muingereza katika uhuru tuliopata, ukienda katika ukurasa wa 67, inazungumzia mipaka ya Zanzibar, inasema;

"The State of Zanzibar means the Island of Zanzibar, Pemba, Latham including the territorial of water, thereof an any Island with those waters".

Mhe. Naibu Spika, Sasa nikaenda kuangalia kwenye *website* ya *TPDC* katika mfumo mzima wa mafuta na gesi na nikaangalia *activity Map* ya 2014 inazungumza maeneo kadhaa ya mafuta na gesi ambayo hii imekuwa *updated* katika *license in situation May* 2014, nataka kujua *blocks No. 9, 10,*11 na *12* ambazo ziko mashariki ya Unguja na Pemba.

Halafu nataka kujua mpango mzima wa *block* ambayo inaitwa *'Tanga Basin'* ipo Magharibi ya Pemba. Sasa haya yote nataka kufahamu kwa sababu kutoka na sheria ambazo zimetungwa ya *Petrolium Act* 2015 na nataka kujua pia kwa mujibu wa katiba hii ya 63 kabla hatukwenda kwenye Muungano, eneo la *Latham* linaloitwa Fungu Mbaraka ambalo ni mpaka mwisho Kusini mwa Zanzibar. Sasa zile rasiliamali ambazo zitakazopatikana pale na *Latham* Kimbiji ambayo imepewa kampuni ya *Heritage Petrodel according to the website ya TPDC.* Sasa hii *Latham* Kimbiji hapa kitachopatikana kwa mujibu wa sera ya mafuta na gesi tutakapopata sisi, umejipangaje hasa pamoja na *Block* 7, *Block* ya Tanga *Basin* na Block *Latham* Kimbiji.

Sasa napenda niende katika suala ambalo kidogo nitaka nilizungumzie ni kuhusiana na matatizo ambayo nahisi yanatukabili katika Shirika letu la *ZECO*. Mhe. Naibu Spika, hili Shirika la *ZECO* ni shirika muhimu sana kwetu sisi na hasa Wazanzibari wana matumaini mengi. Lakini nataka niwapongeze kwanza. Hili shirika limekuwa linafanyakazi kwa kupeleka umeme vijijini bila ya kuwa na mpangi mzima wa fedha kutoka serikalini. Lakini najua serikali imeanzisha hii *infrastructure tax* ya 2%. Sasa Mhe. Naibu Spika, hii 2% inakwenda Hazina, lakini wenzetu kule Tanzania Bara wameanzisha mfumo wa *REA* (*Rural Electrification Agency*) ambapo zile pesa wanazitumia kwa kupeleka umeme vijijini. Sasa kwa nini serikali isifanye mpango wa kuiangalia kwamba hizi pesa *two percents* zikapelekwa katika Shirika la *ZECO*, ili waweze kutimiza yale matumaini na ndoto za Wazanzibari, kwamba ile *Rural Electrification Agency* iweze kukamilika.

Mhe. Naibu Spika, maana yake kwa sasa ukiangalia vijiji vingi bado nimeangalia katika mpango mzima ambao mumejipanga, kuna vijiji mumepanga ninafikiria thalathini na nane Unguja na kumi na sita vinakwenda Pemba. Na mimi ninakupongeza sana Mhe. Waziri, hapa na kuna vijiji vya Ubago Uwandani, kuna Jumbi Jaani. Ninachoomba Mhe. Waziri, hii Jumbi Jaani, naomba hili jina la 'Jaani' lifutwe, jimboni kwangu mimi hakuna Jaani, kuna maeneo ya kutupa *dump.* Lakini Jumbi Jaani ni eneo zuri na inashusha hadhi ya Jumbi. Kwa hivyo, naomba hawa watu wa *ZECO* wasiite Jumbi Jaani, hili neno 'Jaani' liondoke.

Halafu pia na Timbini na pia Kikungwi Uwandani pamoja na Unguja Ukuu Kae Pwani. Naomba sana hivi vijiji kwa muda mrefu walipewa ahadi na serikali kupelekewa umeme, naomba sana katika *priority* mutakayotupa kwa Wizara yako mutuangalie kwa jicho la huruma na mwaka huu hizo ndoto ziweze kutimizwa. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, hili shirika wanachukua umeme kutoka Tanzania Bara kupitia *TANESCO*. Kwa muda sasa nina uhakika kuna deni kubwa ambalo *TANESCO* wanatudai. Ninaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar kwa kukaa pamoja kama ndugu kwenda nalo na hili deni.

Lakini Shirika la *ZECO* kwa kweli, mimi kama ningekuwa mkurugenzi ningekuwa nishakufa leo. Hili shirika sijui linakwendaje. Maana yake lazima hawa wafanyakazi wanastahiki pongezi za hali ya juu. Yaani tangu Disemba, 2015 mpaka hadi Juni, kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wameweza kulipa karibu bilioni tano kila mwezi mpaka nukta tano wanazipeleka kwa *TANESCO*, kila mwezi, mbali ya deni linalodaiwa. Kwa kweli hili nawapongeza sana na Mungu awajaalie waendelee kuwa nalo na hizo akiba ndogo wanazobakia nazo basi ninaomba sana muende na mujipange mukapambane na Mhe. Waziri wa Wizara hiyo *two percent* iondoke na ingie zake huko.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kidogo nataka niseme tabia ya shirika hili. Kwenye mashirika mengi na taasisi za serikali panakuwa pana watu wengi, kuna fedha na kuna mambo mengi yanakuwa yanatokezea. Shirika hili la *ZECO*, huyu mkurugenzi wake mimi ninamfahamu juu juu, nilikutana naye wakati umeme ulipozimika Zanzibar, nilipokuwa mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji sekta ya utalii. Kwa kweli alitusaidia sana na alikuwa karibu ya sisi. Lakini huyu inaelekea ni mtu katika kitovu cha hili shirika na inawezekana pia ndani ya wizara yako kuna migongano na kutokufahamu baina ya wafanyakazi na huyu mkurugenzi. Na inawezekana huyu mkurugenzi analinda maslahi ya taasisi na wizara yako na inawezekana pia kuwa anapingwa. (*Makofi*)

Sasa ushauri vitu ambavyo vinavuja ndani ya wizara yako, nimetembea sasa hivi karatasi ambazo zinazohusiana kwamba kuna fedha zimepotea, lakini ukifuatilia hakuna fedha iliyopotea, ni *auditing* ndogo ya *junior auditor* kataka kupeleka karatasi juu na haijatoka katika sehemu ya *auditor*. Ninataka nikumbushe sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hatuwezi kufanya kazi kwa kutumia *document* ya *auditor* mdogo ambaye haijapita katika *Auditing Committee*, haijapita kwa Mkurugenzi, haijenda katika Bodi, haikwenda wizara na Katibu na Waziri mwenyewe, haijapita kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, haijapita pia katika Kamati ya *PAC*,

lakini *document* inatoka katika *junior auditor* anayetoa ili kuweka mtafaruku katika shirika lako.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri, katika mambo haya utakapokuja utueleze utajipangaje kuhakikisha mambo haya hayafanyiki, inakuwa ni aibu kuleta tuhuma za mtu hapa wakati jambo halipo. Lakini ni vizuri sisi kama ni Wawakilishi, tukajiridhisha kwamba *process* yote itafanyika hadi tukaletewa katika ripoti ya *CAG*.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, ninataka nizungumze katika masuala ya ardhi na jinsi ambavyo tunajipanga moja kwa moja. Nataka niseme katika upande wa Zanzibar sasa hivi tunayo ramani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ambapo tunajua kisiwa cha Unguja kipo hivi na cha Pemba kipo hivi. Lakini sasa hivi kuna *project* tayari serikali inafanya kwa nia njema kabisa. Mimi nina wasi wasi *project* zinazofanyika za *to reclaim land from the sea*, kama *project* ya Bakheresa ya Mtoni na kama kajenga bandari upande wa Fumba, itabadilisha ramani ya Kisiwa chetu cha Unguja.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri, uangalie sana kwamba ramani yetu je, ipo bado sahihi kama ya zamani au tayari kuna kifungu tayari kimeshaongezeka kwa upande wa Mtoni. Na kama kimeongezeka kwenye *Google Earth* itakuwa inaonekana. Kwa hivyo, mutupangie lini mutatuletea ramani mpya ya visiwa vyetu na kama kuna maeneo tayari mumejipanga kwenye hii masuala ya *land reclamation*, kuongeza ardhi katika bahari basi mujipange kwamba isiwe tunapoteza pesa kila baada fulani tunatoa ramani mpya ya Zanzibar.

Tunajua matatizo haya yaliikuta nchi kama ya Holland walipokuwa wanafanya zile *land reclamation*. Kwa hivyo, *boaders* za visiwa vyetu tuweze kuviangalia. (*Makofi*)

Lakini pia ninataka niulize masuala ya uwekezaji ambao watu wamejenga. Ni vizuri katika wizara yako na watu wa dini na hasa katika uwekezaji, hawa wawekezaji watu wamewekeza pesa zao nyingi. Kuna makampuni ambayo yapo Zanzibar ninayafahamu wana *lease* ambazo zile za *consolidated lease* wamepewa na tayari wengine wamechukua mikopo kutoka benki. Lakini mambo mengine hutokezea katika wizara yako, sizungumzii wewe Mhe. Waziri, lakini wizara yako iliyopita wanafuta hizi *lease* kwa njia ambazo siyo za kisheria. Na inaleta migogoro, kuitea hasara pesa kwa nini yanafanyika mambo haya. Wawekezaji ni malaika, ni wafanyabiashara wanahitaji faida, tuwalinde, tumewaleta huku kwetu. Na ninamnukuu Katibu Mkuu wa Wizara

wa Fedha alipokuwa Mkurugenzi wa *ZIPA*, alisema wawekezaji wanaokuja Zanzibar wanakuja siyo kwa sababu ya Serikali ya Zanzibar inafanya kampeni kuwaita, wanakuja hapa kutokana na kuitana, wanakuwa ni mabalozi wazuri. Kwa hivyo, tuwapende na tuwalinde. Hivyo, matatizo haya uyaangalie sana na uyajue ni kwa nini yanasababisha mambo haya.

Lakini pia suala la Mji Mkongwe. Mhe. Naibu Spika, Mji Mkongwe serikali ina asilimia 35 ya nyumba ni za kwenu. Majumba yanazidi kuanguka na kuporomoka. Munailaumu Mamlaka ya Mji Mkongwe. Lakini Mamlaka Mji Mkongwe kweli haina kosa. Hebu jaribu kuangalia hizi nyumba ambazo munazi-*own* nyinyi kama serikali, zipo zaidi ya asilimia 35. Wanaokaa hawawezi kuzijenga. Historia inaonesha zile nyumba watu wanaokaa walikuwa ni watu wenye kipato cha kati. Lazima mutafute taratibu ambazo muzijenga zile nyumba, muangalie mutafanya njia gani ili muweze ku-*maintain as Swahili Culture, Swahili antiquity* ibakie lakini nyumba zetu zisiporomoke.

Sasa haiwezekani mtu anakaa hatii rangi, hatengenezi, majumba yanazidi kuporomoka kila siku, tutaishi mpaka lini. Na Mji Mkongwe ni lulu, Mji Mkongwe ni hazina, Mji Mkongwe siyo urithi wa Wazanzibari, Watanzania, Mji Mkongwe ni urithi wa watu duniani *is* Th*e World Heritage Site.* Kwa hivyo, lazima tuulinde na elimu izidi kutolewa na jukumu hilo ni la serikali zaidi kwenda kufika. (*Makofi*)

Lakini pia ninataka nizungumzie masuala ya maji na masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mhe. Naibu Spika, hizi mvua zilivyozipiga juzi, hizi mvua siyo mvua za masika. *There is a problem* na upepo huu utaendelea kupiga na mvua zitapiga mwaka ujao zaidi kuliko hizi na kila tunapokwenda mbele. Lazima wananchi wetu tuwatayarishe na serikali mujipange. Yupo mkurugenzi mmoja kule ndugu yangu mmoja ninayemfahamu Dkt. Aboud Jumbe huwa anashiriki sana na namfuatilia kwenye *facebook*, anazungumza mambo mengi na anakwenda katika vikao.

Huyu ni mtu mmoja ni hazina nzuri ya Wazanzibari, tumtumie anafahamu pia wapi hichi kisiwa kinaelekea kwa miaka ya mbele na maji yetu yatakuwa vipi. Kwa hivyo, tujipangeni baina ya mabadiliko ya tabianchi na maji yetu na matumizi tunayokwenda nayo, tuanze kujipanga wapi tunakwenda. *Global warming it is there* na inakuja. Mara nyingi tunasema sisi Waafrika tuna tatizo moja, tunasema; "*don't worry about tomorrow when come tomorrow it will be today"*. Huu ni upotofu na ni ujinga. Lazima tujipange tunakwenda wapi, ardhi yetu ni ndogo, wananchi wetu wanazidi kuzaliana, tupo wengi, tunazidi kubanana.

Mhe. Naibu Spika, tumshukuru Mwenyezi Mungu na viongozi wetu katika huu Muungano, maana yake sijui tungekimbilia wapi kama siyo huu Muungano huko miaka ya mbele. Kwa hivyo, lazima tujipange tuwe tayari. Na haya upepo huu mwaka ujao utakuwa ni mkuwa na watu wengi wanaokaa katika maeneo ya vijijini baharini wataathirika. Wavuvi wengi lazima mutafute njia mvuvi na taarifa zimfikie kama yupo kilomita sita baharini awahi kurudi ili asije akazama apate kuiona familia yake. Mujipange kwa sababu upepo utazidi kuwa mkali. (*Makofi*)

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, ninataka nizungumzie kuhusu masuala ya *pump* na maji. Mhe. Waziri, tangu Mapinduzi tunakwenda masuala ya maji, afya na elimu. Kwa sababu serikali kweli imekusudia masuala haya kuwa bure kwa wananchi wake. Lakini mara hii hebu tafute njia Mhe. Naibu Spika, haya masuala ya *pump* kusukuma maji, tujue ni *strategy* gani munatumie wizara yenu ili liishe tulitokomeze kutoka leo lisizungumzwe mwaka ujao kufika mwaka 2020. Hebu binadamu, serikali na sisi wananchi na Wawakilishi tuone haya kwa wananchi wetu, kila siku *pump* imeharibika, *pump* inasukumwa, *pump* mbovu. Hii *pump* ni kitu gani? Mbona majumbani kwetu maji tunapata kwa kutumia hizi *pump*? Kwa nini serikali inashindwa kuhakikisha hizi *pumps* zinafanya kazi? Kuna matatizo gani?

Mhe. Naibu Spika, kama hawa watu wanaekwa hawawezi kusukuma maji. Tuna vikosi vyetu vya Jeshi, wafukuzeni kazi hawa watu wanaokataa kusukuma maji. Wakikaa wanajeshi watasimamia maji vizuri. Maji ni muhimu, si sehemu ya kuchezea. Wananchi wanahitaji huduma, zisukume maji hasa katika miezi kama hii mtu bado analalamika masuala ya maji. Tunakwenda mpaka lini hivi Mhe. Naibu Spika, haiwezekani. (*Makofi*)

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, katika suala zima nilililozungumza Mhe. Waziri...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Basi na mimi Mhe. Naibu Spika, kidogo leo niwe mtiifu, nisipambane na wewe. Nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na nikupongeze Mhe. Waziri, niwashukuru wananchi wangu na mimi pia naunga mkono hoja asilimia 99.9. Mhe. Waziri, utakapokuja naomba uje maelezo yako mazuri na nitakushauri pia ikiwezekana uipitie Sheria ya Mafuta uliyokuwa nayo vizuri ili niridhike sana kwenye mafuta na gesi, viwanja, wawekezaji,

maji, mabadiliko ya tabianchi, mazingira, haya yote utueleze. Na sitofurahi ukija ukiniambia kwamba ni Waziri lakini wizara ni mpya, aah! Ninataka majibu sahihi, sisi kama *back benchers*. (*Makofi*)

Baada ya hapo ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja asilimia 99.9, hiyo nukta moja nitaisubiri mpaka nipate maelezo.

Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata sasa ni Mhe. Moh'd Mgaza Jecha, baadae ni Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali na baada ya hapo tutampa nafasi Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi siku kwa leo kupata nafasi ya kuichangia Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Kwanza ninapenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa wizara hii kwa utendaji wao wa kazi kama vile Mwenyezi Mungu alivyojaalia. Ninawapongeza sana watu wa *ZECO* kwa shughuli zao za kutupatia umeme vijijini. Na vile vile niwapongeze sana watu wa maji ambao wanatupatia maji kwa ajili ya vijiji vyetu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea sana niwapongeze sana watu wa Jimbo langu la Mtambile kwa kuniwezesha kufika katika Baraza hili na kuweza kusimama hapa leo nikiwa kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, mimi masuala ya maji na masuala ya umeme ninashukuru sana katika maeneo mengine ya jimbo langu. Lakini nina matatizo ya jimbo langu kwenye vijiji viwili mpaka vitatu umeme huo haujafika. Nilikuwa ninamuomba sana tu Mhe. Waziri, vile vijiji vilivyokuwa havijafika katika jimbo langu, ningemuomba safari hii Mwenyezi Mungu akijaalia ufike umeme kama hivi nitakavyovieleza.

Mhe. Naibu Spika, Kijiji kinachoitwa Tangandongoni, Jemele Kangani pamoja na Kangaji Shamiani. Vile vijiji bado havijapata mambo ya umeme ambao kuwa unatakiwa kwa kila maslahi ya Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nende kwenye *tank* letu la maji la pale Kangani. Lile *tank* tokea mwaka lilivyofanyiwa matengenezo ya kutengenezwa, lile *tank* bado halijafanyiwa *service*. Kwa hivyo, maji yake yanakuwa mengine yana

matatizo. Mwengine yanafika na kuna sehemu nyengine bado hayafiki, kwa sababu tokea lipoundwa basi lile *tank* hajafanyiwa matengenezo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea pia niende katika shughuli ya kusimamia mapato. Mimi nimuombe tu Mhe. Waziri, waendelee sana kusimamia mapatao ili serikali ipate mapato yake mazuri. Ningemuomba sana tena Mhe. Waziri, huu Mswada wa Mafuta uletwe hapa Barazani ili sisi Wawakilishi tupate kuujadili ili na sisi Mwenyezi Mungu akitujaalia tuwe ni watu wa mafanikio na Zanzibar izidi kuendelea kwa hali na mali.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mchango mkubwa. Namuomba tu Mhe.Waziri, kama hivyo nilivyozungumza basi anisaidie katika jimbo langu kwa masuala yangu hizo niliyomuomba. Ninampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote ili kuendeleza gurudumu la Zanzibar yetu. Sina zaidi ninachangia na ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia mpaka itakapofika. (*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, ninakushukuru sana kwa kwenda moja kwa moja kwenye hoja. Sasa Mhe. Mohammedraza, kwa bahati mbaya hayupo, anayefuata kwa hivyo, nitampisha Mhe. Asha Abdalla Mussa, baadae atafuata Mhe. Omar Seif Abeid na baadae atakuja Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.
Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii ambayo imebeba mambo mengi ya kijamii. Mambo hayo hususan suala la maji, umeme na mazingira na mambo mengine.

Mhe.Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kwamba maji ni uhai na sisi tumekuja hapa katika chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi ili kuwatetea wananchi wetu kwenye majimbo yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na sisi ni wasimamizi wakuuu kuhakikisha serikali inawafanyia au inawaondoshea changamoto wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwenye sekta ya maji. Kati ya visima vilivyochimbwa ndani ya Jimbo langu la Kiwengwa kuna visima vitano. Visima vitano hivi hakuna kisima hata kimoja ambacho kinatoa huduma kwa wananchi wangu.

Ninamuomba sana Mhe. Waziri, atizame kwa kina kwenye bajeti yake ya mwaka 2016/2017, basi angalau visima viwili vichimbwe na vimalizike ili wananchi wangu waweze kupata huduma hii ya maji safi.

Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo langu hili la Kiwengwa huduma hii ni changamoto kubwa sana. Kwani ukitazama Shehia ya Kiwengwa yenyewe. Shehia ile ni ukanda wa bahari na ukichimba kisima cha kawaida maji yanayotoka ni maji ya chumvi. Sasa hivi wananunua dumu moja shilingi mia tano. Niliwahi kwenda pale Ofisi ya Maji Wilaya kutaka huduma kwa mwezi huu wa Ramadhani. Lakini tulipofika pale hayo mambo waliyotujibu pale kwa kweli hayakuridhisha na siwezi kusema hapa, kwa sababu itakuwa ninawashitaki. Mhe. Naibu Spika, lakini ninakuomba sana Mhe. Waziri, uwatizame sana wananchi wangu wa Jimbo la Kiwengwa kuhusu huduma hii ya maji safi na salama.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikielekea katika masuala haya haya ya maji, ninaambiwa kuwa kuna matengenezo ambayo yamefanyika ya miundombinu ya maji hususan suala la umeme na kununua mota za maji. Lakini nimeona hapa katika Shehia zangu mbili; Shehia ya Kisongoni na Shehia ya Mgambo, kumefanyiwa matengenezo ya umeme kuhusu suala zima la maji. Lakini cha kushangaza na kusikitisha huduma hii hazipo katika Shehia hizo. Mhe. Naibu Spika, naomba wizara husika isipokee tu taarifa ya kwamba tumetekeleza, tumetekeleza, naomba mufuatilie kwa kina ili kujua kwamba haya mambo yametekelezeka kweli. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimeona hapa mwaka 2016/2017 kutajengwa vibanda vya kuhifadhia mashine za kusukuma maji. Vibanda hivi vipo lakini kuna watu ambao wanajitolea kuvilinda vibanda hivi na kufanya zile huduma pale. Lakini cha kusikitisha ni muda mrefu sasa na wengine wanafika hadi kufariki hawajapata posho. Naomba wizara husika iwatizame kwa kina kwani hawa nao wanaacha kazi zao wanahudumia wananchi kwa kuendesha shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, naomba wizara husika iwatizame kwa kina watu hawa wanaojitolea. Kuna tangi moja ambalo limejengwa katika eneo la Kipandoni juu karibu na Kiwengwa kwenye mlima mkubwa pale. Katika matangi sita nadhani moja ni lile pale, nawaombeni sana wizara husika mlifanyie kazi kwa haraka ili wananchi wa kule wapate yale maji. Kwa sababu tangi lile ukimalizika mradi ule shehia karibu tatu zitapata maji.

Mhe. Naibu Spika, kuna migogoro mingi ya ardhi katika jimbo langu ikiwemo katika maeneo mazima ya Kiwengwa, kwa sababu Kiwengwa ni eneo la

Ukanda wa Pwani. Lakini kuna migogoro ambayo inajitokeza baina ya wawekezaji pamoja na wananchi wenyewe, inafika pahala mwekezaji anapokwenda pahala anauziwa eneo dogo tu, lakini baada ya miaka mitano au sita mwekezaji yule anasema na eneo lililobakia ni eneo lake. Hatimaye wananchi wakipeleka kesi mahakamani basi kesi zile zinacheleweshwa na hatimaye hukumu inatolewa kwamba, mwekezaji ndiye mwenye eneo hilo husika na kumbe mwekezaji kauziwa na wale wananchi waliokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe.Waziri, kuna kesi moja iliyokuwa Kiwengwa, kuna *restaurant* inaitwa Chakula Chema, sasa ni mwaka wa tatu wenyewe familia hiyo wanapata tabu wanafungiwa na kesi haijasikilizwa na wala haijatolewa hukumu. Naomba sana tutashirikiana pamoja na wizara yako ili kuhakikisha wananchi wale ile kesi inamalizika.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuomba jambo jengine kwenye wizara hii. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, ilipima viwanja katika eneo la Mfenesini Kwa Gube na hatimaye waliwahi kuchukua pesa za hati kwa wananchi wale. Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha mpaka sasa viwanja vile hawajapewa wenyewe. Kila tunapokwenda pale kwenye mikutano basi wananchi hawataki kuhudhuria vikao hivi kwa sababu wanadai haki yao katika kesi ile ya viwanja. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, alitizame kwa kina suala hili na baadae uweze kututolea ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sina mengi, lakini ninachokiomba ni kwamba wizara husika itutizame kwa kina katika suala zima la maji safi na salama. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa. Sasa nimwite Mhe Mohammedraza Hassanali, aliniomba alikuwa na dharura, kwa hivyo, ametoka kidogo. Baada ya hapo atachangia Mhe. Omar Seif Abeid, halafu atakuja Mhe. Nassor Salim Ali (Aljazira) na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf. Mhe. Raza karibu.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Naibu Spika, niipongeze Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Vile vile, nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii. Pia, nimpongeze waziri, mwenzangu Mhe. Salma Aboud Talib.

Vile vile, nimpongeze kaka yangu kwa hekima zake na hotuba yake nzuri aliyoweza kuitoa katika taarifa hii ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na

Mazingira ambayo inaongozwa na kiongozi wangu Mhe. Hamza Hassan Juma, maarufu Komredi, kwa utulivu na usikivu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni yetu na mimi nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, pamoja na uongozi mzima wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ni nzito na inahitaji mambo mengi, na hasa suala la maji. Suala la maji halina mjadala, sio kwa binadamu tu hata kwa wanyama ambao tunawafuga. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri, nataka niseme leo namshukuru sana Mhe. Rais, kwa kumteua Mhe. Salama Aboud Talib, tumesoma Kidutani ndogo, kuanzia chumba cha kwanza mpaka chumba cha saba. *Alhamdulillah*, namshukuru Mhe. Rais. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa namuambia Mhe. Waziri, kwa kuwa tulikua sote wanafunzi wa *desk* moja, basi nataka awe msikivu, mvumilivu na kile anachoweza kukisema basi akiseme. Mimi kwa kushirikiana na wananchi wafanyabiashara na wenzangu tutaisaidia sana wizara hii.

Mhe.Naibu Spika, katika wizara hii Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibari imeshafanya mengi. Kama maji, barabara na mambo mengi tu. Lakini mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, natakiwa vile vile kushirikiana na wizara hii katika kuondosha matatizo kwa wananchi wangu wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitamke rasmi kumuambia Mhe. Waziri, nikiwa mwakilishi wa Jimbo la Uzini kwa kupitia Chama cha Mapinduzi, niko tayari kushirikiana na wizara hii ili tukasaidiana. Maana yake Mhe. Naibu Spika, kuna kitu mashirikiano, tukasaidiana kuwaondoshea matatizo wananchi wangu wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Naibu Spika, niko tayari kwa Jimbo zima la Uzini kushirikiana na wizara kuhusu umeme na maji kwa gharama zote kwa kushirikiana na kuweza kutatua matatizo hayo. Wakiniambia kuna *pump* milioni 10,000,000, Mhe. Raza tunataka milioni 3, basi nitatoa kesho.Wakiniambia kunahitajika umeme zinahitajika milioni 50,000,000 wanataka milioni 10,000,000 kesho nitazitoa. Hayo ndio mashirikiano.

Mhe. Naibu Spika, niseme mimi nimeifanyia nini Uzini au nimeifanyia nini nchi yangu. Mhe. Naibu Spika, Mapinduzi ndio yaliyotufikisha hapa na mimi ni mtoto wa Kimapinduzi, nimesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bila ya Mapinduzi nisingefika hapa, na walionifikisha hapa ni

wananchi waliokua chini.Kwa hivyo, ni vizuri serikali yangu inayoongozwa na Dkt. Shein tukaeni kwa pamoja. Kila mwakilishi na mbunge akae katika jimbo lake, tuwe na utaratibu wa kufanya vikao, kati ya Rais, waziri anayehusika na viongozi, ili tuone kila jimbo tunasaidiana vipi.

Sasa mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, haya sio mageni kwangu. Mhe. Naibu Spika, wakati naingia matawi ya Manzese Miwani, wakati ule nilitakiwa kuchangia milioni 30. Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu atupe uhai na uzima, wewe ulikuwa shahidi, ulikuwa mmoja kati ya waalikwa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan. Katika siku ya Manzese pale na Rais mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi alikuwa mgeni rasmi, nilitakiwa kutoa shilingi milioni 30 *cash*, nikazitoa. Nilitakiwa kutoa *transformer* Bambi ya shilingi milioni 15,000,000, haya ndio mashirikiano.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie tuna watendaji wazuri sana katika wizara hii, kuanzia Katibu Mkuu na watendaji wote, lakini tatizo Mhe. Naibu Spika, hai hoi, yaani unachokipata ndicho unachokitumia. Serikali yetu ina huruma, lakini inataka kila mtu apewe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niliambie Baraza hili pamoja na Wazanzibari wote, nina zaidi ya miaka 20 ninakaa Kibweni sijaona mfereji kutoka maji nyumbani kwangu, hiyo natamka wazi, mimi Raza, Kibweni pale kwa zaidi ya miaka 20 sijapata kuona maji yanatoka nyumbani kwangu. Lakini nikikumbuka na kurudi, kuna watu Bambi Kijibwemtu toka kuzaliwa dunia hawajayaona maji, *Innalillah Wainna Illayhirajiun*. Serikali yetu imefanya mengi, lakini sikuwa napiga kelele.

Mhe. Naibu Spika, mimi nyumbani kwangu zaidi ya miaka 20, na hii Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, nilitumia zaidi ya milioni 28, ili nifanikiwe kupata maji. Lakini sikufanikiwa nikasema *Alhamdulillah Innallah Maaswabirina*, lakini watendaji ni waungwana. Kwa hivyo, taasisi zote hizi zilizokuwa chini ya wizara inayoongozwa na Dkt. Khalid Salum pamoja na watendaji wote. Mheshimiwa, wakati mwengine zana za kufanyia kazi, imeharibika *pump*.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nilikua nataka kutoka kwa Mhe. Waziri, ninachoomba mawasiliano ni jambo la muhimu, panapotokea hitilafu ya *pump* au yoyote, basi tuitaneni, wafanyabiashara wananchi. Lakini leo *pump* imeharibika eneo moja na *pump* thamani yake ni milioni tano (sh.5,000,000), wananchi 4,000 wanakosa maji kwa *pump* ya milioni tano (sh5,000,000).

Lakini wewe Mkurugenzi unakwenda kutizama ile *pump* una gari ya milioni 200, *Innalillah Wainna Illayhirajiun*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hili ni letu sote, Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wenyewe, kwa hivyo, mawasiliano ni jambo muhimu. Lakini *pump* ya shilingi milioni tano (sh.5,000,000) imekaa miezi sita, wananchi wanyonge na wakulima ndio wanaoteseka. Kwa hivyo, ningeiomba wizara hii Mhe. Salama Aboud Talib, tuwe na *communication.* Mimi nasema Wakurugenzi wote wizara nzima ina uadilifu mkubwa, ardhi, upimaji na Mji Mkongwe kote huko. Lakini wakati mwengine *communication* ni muhimu, wakati mwengine tukae kwa pamoja, tuwe na tabia ya kufanya vikao.

Mhe. Rais, mimi namuomba huwa na watendaji wake wanaita sijui Bangokitita, na sisi tushirikishwe wakati mwengine katika sehemu yetu. Kiswahili changu cha Kihindi nisameheni jamani. Wakati mwengine na sisi wawakilishi, Mhe. Rais pamoja na wizara tuiteni. Jamani eeh, au Raza eeh, hapa Jimbo la Uzini panahitajika shilingi milioni 100, lakini uwezo hamna bado hali ngumu basi angalau changia shilingi milioni 10 au milioni 20, lakini hiyo inasababishwa na mawasiliano. Mimi nafikiri tatizo hili tutaweza kulitatua kwa nchi nzima.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakupa mfano ya Mwenyekiti, Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na Waziri. Nataka kuiambia Zanzibar nzima kwamba, *In shaa Allah* kwa kushirikiana na kiongozi wetu Mhe. Rais, suala la *desk* haifiki mwaka 2020 basi itakuwa ni hadithi kwa Unguja na Pemba. *In shaa Allah* uwezo tunao, nia tunayo, tutafanya Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasema tukaeni pamoja jamani, haya ni yetu na tumekuja hapa kwa niaba ya wananchi, basi tuwatumikie wananchi. Mimi Mhe. Raza, mtumishi na boi kwa wananchi wa Jimbo la Uzini, ndio ninavyojua mimi kwa Mwenyezi Mungu, sio nakuja nazungusha kitu tu hapa halafu kazi yangu imeshakwisha. *No*! Tunataka kutatua matatizo ya wananchi, wananchi wanashida na shida yao ndio hayo maji na mengine, basi tushirikianeni tupeane. Mimi niko tayari kushirikiana na sehemu zote na majimbo yote, kwa sababu naipenda nchi yengu, nawapenda watu wangu, wanyonge wananchi. Mhe. Naibu Spika, bila ya wananchi basi tusingelifika humu ndani, Dkt. Ali Mohammed Shein asingeliapishwa bila ya wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka niiambie dunia kwamba, Jimbo la Uzini ndilo lililoongoza kwa kura kwa nchi nzima Unguja na Pemba *Alhamdulillah*. Sasa nataka nimuombe waziri, tutaendelea kushirikiana kutatua matatizo. Lakini

tufike pahala tuweke mbele maslahi ya wananchi, tusifike kwenye umimi na umimi, hatutafika. Wazanzibari lazima tujiulize tunataka nini.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho ni kuhusu Kisiwa chetu cha Mfungu Mbaraka wanaita 'Lamsa'. Mhe. Naibu Spika, Mfungu Mbaraka ni kisiwa cha kihistoria na ni kisiwa kilichokuweko Zanzibar, na mimi katika kipindi cha mwaka jana Baraza lako tukufu hili la wawakilishi kwa kupitia serikali ilitoa kauli ya kusema Mfungu Mbaraka ya Lamsa ipo ndani ya Zanzibar. Mhe.Naibu Spika, kauli hii imetolewa na Baraza la Wawakilishi, imetolewa na serikali, lakini kwa bahati mbaya au nzuri tulipokua tunajadili suala hili ikaundwa kamati ya wanasheria pande zote mbili. Nashukuru Mwenyezi Mungu amjaalie Mwanasheria aliyekuwemo humu ndani alishiriki kikamilifu ndani ya kamati hiyo. Mwenyezi Mungu ampe nguvu na ampe na pumzi vile vile, alishiriki katika kamati hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kumuambia Mhe. Waziri, kwanza aje atuambie, nataka kusema hivi, aliyekuwa Waziri Mkuu Mhe. Pinda, aliandika maneno mawili tu, kwamba taarifa tuliyokuwa nayo kisiwa cha Mfungu Mbaraka ni cha Tanzania Bara au ni cha Tanganyika. Mhe. Naibu Spika, Baraza hili limetuhakikishia. Sasa nataka tupate kauli na taarifa nilizokuanazo kwamba, vitalu vya mafuta namba saba na namba nane vimeshachukuliwa na Watanganyika, ndio Tanzania Bara.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nataka kauli ya serikali na serikali ilikuwa imeshatoa kauli. Nataka niwaambie wawakilishi hapa kwamba, Mfungu Mbaraka ni kisiwa kilichokua na historia zaidi ya milioni 100 na kamandoo Rais mstaafu Dkt. Salmin Amour Juma, tulikwenda kupandisha bendera. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nikuchukuweni, wengi hamuijui Mfungu Mbaraka tutakwenda, na Mheshimiwa, tuliitolea taarifa hapa kwamba wawakilishi wote mimi nilidhamini tukale biriani na sisi tukapandishe pendera yetu ya Zanzibar pale Mfungu Mbaraka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasema lazima tuheshimiwe Zanzibar. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni nchi mbili huru zimeungana na maneno haya aliyasema Dkt. Salmin Amour Juma Darajani, nchi mbili huru zimeungana. Tunaita Zanzibar na Tanganyika tuipate Muungano. Kwa hivyo, katika Muungano wetu hakuna bwana, hakuna Rais mdogo wala mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukikaa hapa kesho watatuambia na hii Chumbe yao wakiona mafuta na gesi pale. Kwa hivyo, nataka serikali kwa hili, na halafu kuna kikao kilifanyika watuambie ripoti, lakini ripoti haikupatikana, hekalu saba, nane ndugu zetu wameshachukua. Kwa hivyo, kesho Chumbe, kisiwa cha Pemba, *Prison Island* watasema yao.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naliambia Baraza, kauli hii tumepewa ndani ya Baraza na ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mhe. Dkt. Salmin...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika 4.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe Haya. Mhe. Rais Mstafu Dkt. Salmin, Dkt. Aman Karume aliyekuja alikua chini ya Dkt. Salmin Amour Rais mstaafu. Mhe. Dkt. Shein alifanyakazi na Dkt. Salmin Amour na alikua Rais wa Zanzibar na Dkt. Shein alikua Naibu Waziri wa Afya. Sasa leo inakuaje tunataka kukaa kikao na wenzetu kwa kitu gani? Tunakaa kikao na wenzetu kwa kutafuta kitu gani? Kisiwa kile hata Tanganyika haikuzaliwa kisiwa hiki kiko Zanzibar, sasa nashangaa! *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nazungumza haya kuna ushahidi tunaweza kwenda hata kwenye Umoja wa Mataifa tukapeleka malalamiko yetu. Lakini nawaambia wajumbe tuacheni tu suala la Zanzibar tusichezewe. Tuna Muungano wa serikali mbili tunaupenda na sisi ndio Wazanzibari tunaipenda hasa serikali hii, lakini tuheshimiane, tuvumiliane na tujadiliane, ni lazima, haiwezekani. Haiwezekani hekalu namba saba na nane zichukuliwe na Watanganyika. Waheshimiwa Wawakilishi nitawasihi, leo mimi nipo, keshokutwa hichi kiti cha CCM kinarejea CCM, lakini tuitizame Zanzibar, tuwe na uchungu na nchi. *(Makofi)*

Juzi wawakilishi waliniambia hapa wanataka kumuona Dkt. Salmin Amour, nani aliyekua tayari. Tukutaneni na Dkt. Salmin Amour akuambieni historia ya Zanzibar. Tuiteni vyombo vya *BBC* Ujerumani akakuambieni sisi ni watoto wa Wapinduzi, tuko tayari. Walinijia wawakilishi Raza eeh! Tunataka kumuona baba yetu Kamandoo, na nilimuendea akaniambia niko tayari. Tufanyeni mukathibitishiwe hicho kisiwa cha Mfungu Mbaraka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa mambo yote hayo naunga mkono kwamba, nitashirikiana na suala la maji, ardhi, nakadhalika. Nataka itakuwa ni mara yangu ya kwanza leo humu kupiga buti ama nijuwe mbivu na mbichi. Nataka kauli ya Serikali kwamba ekari saba na nane ziko Zanzibar au zimechukuliwa na Tanganyika, halafu atuhakikishie Serikali kwamba kama walivyotoa kauli

yao *Hansard* ipo, Serikali imeshatoa kauli mara tatu hapa au tusemeni tuna mgogoro Chumbe watasema yao kweshokutwa ile.

Mhe. Naibu Spika, nataka kauli ya Serikali kuhusu kisiwa cha Mfungu Mbaraka haiwezekani Komandoo Dkt. Salmin Amour kasimama tukapandisha bendera leo tunakuja tunakaa tunafanya ndivyo sivyo.

Mhe. Naibu Spika: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Mhe. Mohammedraza Hasssanali Mohammedali: Mhe. Naibu Spika, nashukuru naiunga mkono niko tayari kusaidia nchi yangu na masuala yote ya maji, barabara na vitu vyote. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono asilimia robo tu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia Wizara hii na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uzima wa afya tukaweza kukutana hapa asubuhi tukajadili mustakabali wa nchi yetu, ni jambo la kufurahisha na la kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki nipoteze muda wangu najua kuutumia kwake, mimi kinachoniuma ni maendeleo, hata nikisimama hapa nachangia jinsi gani tupate pesa tuweze kuendeleza nchi yetu. Mimi moja kwa moja kwanza nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Rais kwa kumteua Mhe. Bi Salama. Mhe. Bi Salama, muda mfupi niliofanya nae kazi kumtambua kwake nimemuona ni mtu mahiri sana kwa sababu unapompelekea kitu unapompelekea suala ana-*take action* mara moja, kwa hivyo, mimi matumaini yangu kwake ni makubwa kwamba, Wizara hii inaweza ikafanya mambo mazuri kwa muda mfupi. Mwenyezi Mungu ampe hikma na uwezo na sisi tunamuahidi kama tutashirikiana nae kwa hali na mali kuhakikisha kwamba tunafikia malengo tuliyoyakusudia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niende kwenye kilio cha wananchi wangu wa Konde eneo la Makangale, Jimbo hili Mhe. Naibu Spika, ni kilio cha siku nyingi cha watu wa Makangale kwamba, Serikali pamoja na nia nzuri ya kuiendeleza Makangale ilitenga eneo hili kwamba liwe eneo la wawekezaji kwa maana ya ujenzi wa mahoteli, maeneo ya mahoteli yamepimwa kutoka Kusini Magharibi mwa Shehia ya Makangale iliyopakana na msitu wa Ngezi, mpaka Kaskazini kwenye mnara wa Kigomasha ambao ni mnara maarufu sana Afrika ya Mashariki. Maeneo haya yakatengwa kwa ajili ya uwekezaji hasa kwa ujenzi wa mahoteli, kuanzia mwaka 1994.

Lakini jambo la kushangaza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mahoteli ni mengi, lakini mpaka leo ni maeneo sita ambayo yamejengwa mahoteli, jumla ya hoteli ziliopo pale ni sita tu na maeneo ni zaidi ya hamsini, kilichofanyika pale maeneo yale yamepimwa, yamechukuliwa na watu wameyadhibiti, mengine yamejengewa makuta bila ya kuyaendeleza. Wananchi wa jimbo langu ambao ni wakulima na wafugaji hawapati fursa ya kulitumia eneo lile limezuiwa na watu kwa ujanja ujanja, maana yake mimi nasema kwa ujanja kwa sababu lengo zuri la Serikali ni kuliendeleza ili serikali ipate maslahi na wananchi wake wafaidike, lakini leo wananchi wa Makangale hawafaidiki na eneo hilo.

Kwa hivyo, mimi namuomba Waziri mpya aliyekuwepo, mimi najua ni mchapakazi alifuatilie suala hili kwa kina akishirikiana na Idara ya Uwekezaji ya Vitegauchumi na watu wa Utalii kulipatia ufumbuzi wa haraka suala hili, kwa sababu sheria tunazo, muda wa matumizi ya ardhi kwenye sheria imeelekezwa kwamba, unaposhindwa kuliendeleza eneo kwa muda maalum unatakiwa libadilishwe umiliki, hati yako inayo, Mhe. Waziri, anayo mamlaka ya kuifuta akishirikiana na wenzake na kuwapa watu wengine wenye nia sahihi ya kuleta maendeleo ya nchi hii.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, suala hili alichukue na alishughulikie kwa haraka na kulipatia ufumbuzi, hichi ni kilio cha muda mrefu, kimekuwa ni kilio kwa watu wa Makangale, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, suala hili alichukulie uzito ili mwakani nikija niweze kulizungumza kama ninavyosema kama anachukua maamuzi ya haraka, yaani anapopewa kazi anaichukulia maamuzi ya haraka.

Lakini pia nakuja kwenye idara hiyo hiyo kwenye upande wa viwanja vya ujenzi wa makaazi katika maeneo ya Tumbe, Chwaka, Mhe. Naibu Spika, maeneo yale yamepimwa, naishukuru Wizara kwa upande wa Pemba wameyagawa Tumbe/Chwaka *Phase I* wameigawa na *Phase II* sina uhakika kama wameigawa lakini Tumbe tatu naona hawajaigawa, sasa naiomba Wizara ichukue hatua ya kuvigawa viwanja hivyo ikiwezekana na sisi Wawakilishi tupatiwe angalau na sisi tujisikie kidogo.

Nikitoka kwenye hilo nakuja kwenye suala la maji, Mheshimiwa, ninakwenda mbio mbio nisije nikazuiwa, suala la maji ni suala ambalo nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri na Naibu wake, mara mimi nilipopeleka kilio changu walikisikia, wakaniahidi kwamba watakifanyia kazi na dalili zinaonyesha kwamba, tatizo hilo liko njiani kutatuliwa.

Lakini nataka nipate uthibitisho ili na wananchi wangu waridhike, nawajue kwamba kweli tatizo hili linashughulikiwa na Serikali, nataka nijue ni lini Waziri aniambie tatizo la maji la Mkia wa Ng'ombe na kijiji cha Kifundi litatatuka kuwaondolea dhiki wananchi wale, kwa sababu kimekuwa ni kilio cha muda mrefu kijiji cha Kifundi kuna sehemu mbili; kuna sehemu iliyopita bomba iliyokwenda Mgogoni kwenye mradi wa *TASAF* hao wanapata maji kwenye laini mpya, lakini laini kongwe ambayo ina wakaazi wengi wa Kifundi *pipes* zimezikwa tokea 1964 au wakati wa mkoloni mpaka leo *pipes* zile ni mbovu na hazijabadilishwa.

Kwa hivyo, naiomba Wizara iliangalie jambo hili na ilichukulie hatua za dharura ili iwandolee kero wananchi wangu kwa ajili ya kilio hichi kimekuwa cha muda mrefu tokea mwaka 1964, tunapata maji kwa shida ma-*pipes* ya chuma yaliyozikwa enzi hizo yameshajaa kutu, hayawezi kupitisha tena maji kuwafikia wananchi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, nalo alipe kipaumbele na nataka nijue lini tutaweza kufanikiwa kuwaondoshea kilio hiki wananchi wa Kifundi na Mkia wa Ng'ombe, angalau wa Kifundi wamepata hayo ma-*pipes* makongwe lakini wa Mkia wa Ng'ome ndio hamna kabisa, nataka nijue lini utaratibu wa kupatikana maji kijiji cha Mkia wa Ng'ombe ili na mimi niridhike Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka kwenye maji, nakwenda moja kwa moja kwenye suala la umeme. Katika jimbo langu kuna skuli moja maarufu sana aliyoianzisha Waziri Mstaafu wa Elimu Mhe. Haroun Ali Suleiman, kwa bahati nzuri hata hiyo skuli yenyewe inaitwa Skuli ya Haroun Ali Suleiman, skuli hii ni nzuri na ya kisasa ina kila kitu mpaka kompyuta ziko ndani, lakini cha kushangaza ambacho ni kilio cha watu wa Ungi na mimi mwenyewe Mwakilishi kwamba, katika skuli hiyo hakuna umeme, vifaa viliopo pale vinaharibika.

Kwa hivyo, naiomba Wizara ilichukulie suala hili kama dharura ilipe kipaumbele ili skuli ile ikafungiwe umeme, kwa hivyo, naliomba Shirika najua bajeti ni ndigo, mimi nakubaliana nao ni ndogo lakini namuomba Mhe. Waziri pamoja na watu wa shirika la umeme waangalie kwamba hili ni jambo la dharura, tumejenga skuli kwa gharama kubwa, tumepeleka vitu (vifaa) kwa gharama kubwa. Je, kama havitumiki faida yetu itakuwaiko wapi, kwa hivyo, naomba Wizara ilichukulie suala hili na ilipe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, sasa naingia kwenye mabadiliko ya tabia nchi, yaani mambo ya mazingira. Katika jimbo langu katika kijiji cha Msuka nimebahatika mimi nimejengewa kituo cha KMKM kituo hichi ni kikubwa ambapo kwa

Kaskazini sisi nchi yetu imepakana na Nchi ya Kenya, Serikali kwa kuona uzito wa jambo hili na umuhimu wake ikajenga kituo cha KMKM kikubwa katika jimbo langu. Lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi bahari imekula eneo hilo kwa kiasi kikubwa sana, jambo ambalo linasahabisha kituo kile sasa cha KMKM kuwepo hatarini, miaka kumi na tano iliyopita bahari ilikuwa umbali wa mita mia tatu, sasa hivi imebakia mita thalathini au arubaini.

Naiomba Wizara kulichukulia hatua jambo hili kama dharura kwamba bandari ya Msuka au Diko la Msuka bahati inakula kwa kasi sana kiasi ambacho kwamba inakihatarisha kile kituo cha KMKM wakati wowote kinaweza kikaanguka, kikavamia maji kwa sababu tulikuwa na soko, zamani tulijenga limeondoka, kulikuwa na kisima cha KMKM kimeshaondoka, bahari bado inaendelea kula eneo hilo. Kwa hivyo, naomba sana sana kwamba suala hili lipewe kipaumbele na liangaliwe kwa jicho la huruma, bahari inakula sehemu kubwa imeshakula sehemu kubwa na inaendelea kuimalisa.

Kwa hivyo, naiomba Wizara pamoja na uchache wake wa bajeti lakini ilichukulie jambo hili kama jambo la dharura, Mhe. Naibu Spika, nataka niseme mabadiliko ya tabianchi ya bahari kula sehemu ya ardhi si kwamba kwa Kaskazini tu ya Pemba, lakini hata ukiangalia maeneo ya Mashariki ya Unguja, maeneo ya Paje, Michamvi na maeneo yote ya Kaskazini bahari inakula sana eneo la ardhi, kwa hatua za dharura zinatakiwa ikiwa pamoja na upandaji wa miti na wataalam wetu watumie muda mwingi wa kufikiria jinsi gani tunaweza tukalihifadhi eneo hili lisiendelee kuliwa na bahari Mhe. Naibu Spika.

Mwisho, nataka niende kwenye eneo la Mipango Miji. Serikali kama tunavyojua inapata gharama sana kutengeneza mipango miji, inatumia wataalam wake wa ku-*plan* mambo, ku-*plan* miji jinsi gani itumike maeneo ya makazi, haya maeneo ya watoto ya kuchezea, lakini cha kushangaza pamoja na kwamba sheria tunazo, lakini ujenzi holela umezidi kwenye miji. Jambo hili si kama linaathiri tu jamii, lakini linaitia sana hasara Serikali Mhe. Naibu Spika, na ni jambo la kusikitisha kuona miongoni mwetu jambo hili tunalifumbia macho. Mimi naiomba Wizara juu ya jambo la uharibifu wa ramani za miji iwe kali sana, isimuonee haya mtu kwa cheo chake, kwa utajiri wake, wala kwa chochote, iangaliwe sheria inasemaje. Wenzetu Bara wameweza kulisimamia hili na matokeo yake tumeyaona kwamba. wamefanikiwa kuweka miji yao katika mazingira mazuri.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri kupitia Idara yake hii ya Mipango Miji ifike katika jimbo langu iangalie ni jinsi gani Serikali ilipata gharama ya kupanga namna ya majezi katika Mji wa Konde, na jinsi gani ya

uchafuzi wa majengo unavyokwenda, watu wanajenga kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya barabara za mitaa, barabara zile watu wengine wamezijenga viwanda, wengine wamezizuia kwa mambo yao ya binafsi, haieleweki Wizara inayaona haya na watendaji wanayaona. Kwa hivyo, natoa wito kwa watendaji wa Wizara hasa upande wa mipango miji wapite kwenye miji waangalie na wasione haya kwamba mtu kapewa maeneo yake maalum ya kujenga, kawekewa *bicornes* zake za kujenga, mtu anavuka anakwenda kwengine, wasione aibu, wamvunjishe na wachukue hatua kwa sababu sheria zipo.

Vile vilem kwa watu wanaojenga kwenye njia kubwa za umeme, mimi shahidi katika eneo langu kuna watu wamejenga kwenye njia kuu za umeme, Serikali inatakiwa iangalie watendaji waangalie kwamba ile si hasara kwa mkaazi tu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika moja.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante, Mheshimiwa, sitaki nimalize hiyo dakika moja nikaja nikaonekana kama nimepinga, lakini kwa heshima na taadhima nawaomba wawakilishi wenzangu tuiunge mkono hotuba hii mia kwa mia ili tuwawezeshe hawa tuliowapa majukumu watekeleze kazi zao ili mwakani na sisi tupate tena kuja kuwahoji, kwa yale waliyoshindwa kuyatekeleza kwenye bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Ali Salim: Asante, Mhe Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, na nampongoze sana Mhe. Waziri, kwa hotuba yake nzuri ambayo ina mipangilio mizuri kwa faida ya maendeleo ya wananachi wetu. Lakini vile vile nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa kusoma hotuba yake ya kamati kwa umahiri mkubwa sana, nianze kwa kupongeza Mhe. Rais, wetu wa awamu ya saba Mhe. Dkt. Ali Mohamedi Shein. kwa kweli kwa kusimamia ipasavyo sekta ya nishati ikwemo uchimbaji wa mafuta na gesi ambayo tunatarajia kwa muda mfupi unaokuja kuweza kupata mafuta hayo pamoja na gesi.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu hivi karibuni tunategemea kuletewa Mswada wa Sheria ya mafuta na gesi na tunavyojua baada ya mswada huo kupitishwa na kuwa sheria ndio itatoa muongozo wa namna gani wa suala zima la uchimbaji wa mafuta na gesi, suala hili la uchimbaji wa mafuta na gesi

linahitajika kusimamiwa vyema na sote tunajua kwamba namna gani wananchi wanavyokuwa na hamu kubwa ya kuona sekta hii mpya ambayo ya kiuchumi itakavyokuwa inaendelezwa. Mheshimiwa, lakini hayo yote hayawezi kutokea bila ya kuwa na sheria imara na taasisi itakayosimamia vyema mafuta na gesi asilia ambayo ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, tunakumbuka kwamba katika miaka ya nyuma suala hili limekuwa likizungumzwa sana ndani ya Baraza lako Tukufu, lakini halikuwa na mishiko kwani huwezi kuzungumzia au kupeana mikataba bila ya kuwa na sheria na sera imara ambayo ya kusimamia mafuta hayo na ndio maana nikaanza kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein, kwani ameonesha uwazi na utekelezaji wa ahadi zake na usimamizi ambao uko makini katika serikali yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sekta hii pindipo haitasimamiwa vyema inaweza ikazusha migogoro mikubwa sana na niiombe sana kuhakikisha kwamba, mambo haya yanasimamiwa vyema kuanzia serikali na wizara husika ili kuondokana na migogoro mbali mbali ambayo ishawahi kuzikumba nchi mbali mbali ambao zimechimba mafuta haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe wizara ili kuweza kutoa elimu kuanzia Kamati, Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, wadau na wananchi kwa ujumla ili kuepukana na mambo mengi ambayo yanaweza kutokea bila ya kupata elimu kuhusiana na elimu ya haya mafuta na gesi.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kubwa kwa Mhe.Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii watatekeleza haya kutoa elimu kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Kamati ikiongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini vile vile kwa wadau ili na wananchi waelewe vyema. Mhe. Salama Mhe. Waziri, tumefanya kazi nae katika kipindi kifupi, lakini tumemuelewa na tunamuamini, uwezo wake tumeuona. Mhe. Naibu Spika, jinsi ambavyo ninaona kwa kweli ni mategemeo makubwa kwa wizara hii kupiga hatua katika kuleta maendeleo kwa wananchi wote.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nililokuwa nataka nilizungumze ni uundaji wa Shirika la Nyumba, ingawa shirika hili limehamishiwa katika wizara nyengine, lakini mwanzo wake umetokea katika wizara hii. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kwa miaka mingi tumekuwa hatuendi sambamba na wenzetu wa Tanzania Bara, wenzetu wameanzisha Shirika la Nyumba takriban miaka 30 nyuma na hili Shirika la Nyumba sio Tanzania Bara hata katika nchi za Afrika Mashariki wameanzisha Shirika la Nyumba na kuweza kupata kubwa.

Kuanzishwa kwa Shirika hili la Nyumba, Mheshimiwa, litaipa uwezo wa kuweza kukopa katika mabenki mbali mbali au na Taasisi mbali mbali ambazo za kutoa mikopo za kuweza kuendeleza masuala zima ya Shirika hili la Nyumba.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Shirika la Nyumba linatekeleza majukumu yake ipasavyo, kibiashara na kuinua mbinu mpya ili kuachana na utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea. Ni tegemeo letu kubwa sana na nina imani kwamba Shirika hili linaweza likaipatia serikali na Wazanzibari kwa ujumla faida kubwa ya kuweza kuinua uchumi wetu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sekta ya umeme hususan *ZECO*. Shirika la Umeme *ZECO* pamoja na changamoto nyingi ambazo zinazikabili shirika hili, lakini shirika hili limeweza kupiga hatua kubwa sana hasa kwa kuweza kuondoa changamoto kubwa za wananchi wetu vijijini. Mheshimiwa, kama tunavyoambiwa na kama tunavyoona hivi sasa takriban asilimia 86 wananchi wetu wa vijijini wameweza kupata umeme na hizi zote ni juhudi kubwa za serikali yetu inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein, lakini vile vile na uongozi mzima wa shirika hili la umeme la *ZECO*.

Mhe. Naibu Spika, Shirika limejitahidi sana na niwapongeze kwa kuweza kuondoa tatizo la umeme katika maeneo mbali mbali hasa katika visiwa, kama vile kisiwa cha Makoongwe kule Pemba pamoja na kisiwa Panza, wananchi wetu walikuwa wanapata matatizo makubwa sana lakini kwa kweli wamefaidika na haya ndio matunda ya serikali yao ya Mapinduzi. Hii ndio sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuondolea wananchi wake matatizo mbali mbali. Kwa hivyo, ni wajibu wangu au ni wajibu wetu sote kuipongeza serikali yetu lakini vile vile kulipongeza Shirika kwa kufanya kazi yake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ili shirika liweze kuongeza mapato, napenda kutoa ushauri mmoja Mheshimiwa, kwamba wajitahidi kuwafungia wananchi wale ambao hawajapata mita, lakini mbali na wananchi, jana tulikuwa tunazungumza katika kamati yetu Mhe. Hamza, alizungumza hilo kwamba, wizara zote zifungiwe mita ili shirika liondokane na matatizo ambayo wanayapata. Mheshimiwa, Shirika lina matatizo makubwa, lina madeni makubwa, tusiwe tunakaa tunalilaumu shirika tu, hapana. Tulishauri kuweza kuongeza mapato ili serikali ipate mapato ili kuweza kujenga uchumi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nimezungumza haya nikiwa kama mjumbe na nimesimama angalau kuzungumza mawili, matatu kuhakikisha kwamba tunaiunga mkono wizara yetu, tunaiunga mkono hotuba ya waziri ili tuwape waende wakafanye

kazi ili kuhakikisha kwamba wizara na mashirika yetu yanafanya kazi vizuri ili kuweza kuwaletea maendeleo wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kwa sababu mengi yameshazungumzwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati, lakini na mimi nizungumze kuhusu suala zima la matatizo ya maji, Mamlaka ya Maji. Kweli Zanzibar tumepiga hatua kubwa katika kuondoa matatizo ya maji hususan katika maeneo ya vijijini. Lakini bado kuna tatizo kubwa la maji Mkoa wa Mjini hususan Wilaya ya Mjini. Hata katika Jimbo langu la Kikwajuni, bado kuna maeneo yana matatizo makubwa ya maji na nimshukuru Mhe. Waziri, kwa kazi nzuri aloifanya, amenipa ushirikiano mkubwa pamoja na watendaji wake kuweza kutatua angalau tatizo la maji kidogo hususan katika kipindi hichi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Lakini tatizo hili lisiwe kwa muda, niiombe sana Mhe. Waziri, kwamba matatizo haya yaondokane kabisa katika wilaya yetu ya mjini. Mheshimiwa, ni aibu, ni aibu kuona kwamba mji wetu unakuwa na mapungufu ya maji katika mji wetu wa Zanzibar.

Katika maeneo ya Jimbo la Kikwajuni hususan katika maeneo ya Jumba la Mjerumani, ni eneo ambalo huwa lina matatizo makubwa ya maji, eneo la Kikwajuni bondeni na nimuombe Mhe. Waziri, ili kwa kuweza kufanya kazi kuweza kuangalia mbinu na mipango ambayo inaweza kuondoa kabisa tatizo la maji katika Jimbo la Kikwajuni na majimbo mengine katika Wilaya ya Mjini.

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana wajumbe wenzangu ili tumpe nafasi Mhe. Waziri, akafanye kazi katika kipindi hiki ambacho kwa kweli anastahiki kupewa pongezi, ni kipindi kifupi ameonesha na sote tunajua hapa kazi ambayo anaifanya ni nzuri na nina imani kwa Katibu Mkuu aliyonayo, Mhe. Hamza, wamemwita *Alhaj* ni *Alhaj* kweli, *Ali Khalil Mirza*, ni imani yetu kwamba viongozi wetu hawa wakuu katika wizara hii watafanya kazi nzuri na katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 tutakuja kuona hapa mambo mazuri ambayo yamefanywa na viongozi wetu hawa.

Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuweza kumuamini Mhe. Salama, kwa kweli ameonesha ni kiongozi wa mfano katika mawaziri. Kwa hivyo, niwaombe wajumbe tuiunge mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Waziri, ili aende akafanye kazi.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi kunijaalia nikiwa mzima wa afya na kuweza kusimama

hapa kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe.Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri walioiwasilisha mbele yetu na mimi naomba kuchangia hotuba hii machache niliyonayo. Moja kwa moja nakuja kwenye suala la maji. Katika maeneo yetu bado kwa kweli tatizo la maji lipo na bado ni kubwa sana, lakini ukiangalia katika visima vyetu vya maji vinavyochimbwa mara kwa mara kunatokea uharibifu wa *motor* na *pump* na kwa kweli huchukua muda mrefu sana kuweza kupatikana *motors* hizi au kupatikana hizi *pumps* wananchi wakaweza kupata maji. Nimuombe Mhe. Waziri na niiombe serikali kwa ujumla tujipange vizuri kuhusiana na suala hili angalau ziweko *motors* za akiba ilikitokezea tatizo kama hili tuweze kulihami.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 30 wa hotuba hii ulizungumzia matengenezo hayo ya *motors* na hizi *pumps* kwa kisima cha Kidanzini Bumbwini. Niishukuru sana wizara yako kweli waliweza kutuletea *pump* katika kipindi cha mwaka 2015/2016, *pump* iliyoharibika pale ililetwa na wizara ya maji. Lakini ndani ya kipindi hiki kumeharibika *motors* mbili 2015/2016. Kwa mashirikiano ya viongozi walioko ndani ya Jimbo la Bumbwini baada ya usumbufu mkubwa kukaa kwa muda mrefu wananchi basi tumeamua kutafuta *motors* zile maji yakaweza kupatikana mpaka hivi leo japo kuwa baadhi ya vijiji maji yale hayafiki.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hapo hapo nakumbuka kwamba kuna tangi la maji lilijengwa katika eneo la Michungwa miwili. Tangi hili baada ya kujengwa kulisambazwa mabomba na mabomba haya ya maji yalifika mpaka Bumbwini. Siku ya ufunguzi wa bomba hili maji yalipatikana kote mpaka vijiji vya Bumbwini mpaka vijiji vya ndani. Lakini cha kushangaza baada ya kumaliza tu ufunguzi ule kuanzia siku ya pili maji yale hayakupatikana tena mpaka hii leo.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, aniambie ni sababu gani iliyopelekea hata ikawa haya maji hayafiki tena Bumbwini? Lakini pia nimuombe aniambie Mhe. Waziri, hawaoni kwamba serikali wameisababishia hasara kutandaza mabomba yale kuanzia Michungwa miwili mpaka Bumbwini na wakati wananchi hawafaidiki kupata maji na pia ni hasara kiasi gani ambayo serikali imepata kwa kutumia mabomba yale usambazaji wa mji mpaka kufika Bumbwini.

Mhe. Naibu Spika, pia, naiomba wizara hii kuna visima viwili ambavyo vile vilivyochimbwa na Ras al Khaimah katika eneo la Bumbwini ambavyo bado

havijamalizika. Naomba itakapopitishwa bajeti hii, wizara kwa kushirikiana na mimi Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini basi niko tayari kushirikiana nao tuvimalize visima hivi ili tuweze kuondosha tatizo la maji kwa maeneo mengi ndani ya Jimbo letu la Bumbwini.

Mhe. Naibu Spika, katika vituo hivi vilivyojengwa vya maji kina Kituo cha Bumbwini Makoba, hiki kituo Mhe. Waziri, hakina uzio na kwa hali tuliyonayo sasa kwa kweli inakuwa hali yake sio nzuri kama kile kituo hakina uzio kikazungushiwa kikawemo ndani. Ninamuomba Mhe. Waziri, aje aniambie tu lini kinaweza kuzungushiwa uzio kituo kile cha maji kiliopo Bumbwini Makoba.

Sambamba na hilo kuna wafanyakazi wa kujitokea wapo kwenye kituo kile tokea mwaka 2000 hadi hivi sasa vijana wale hawajaajiriwa. Tokea walikuwa vijana mpaka wanazeeka wako pale lakini hawapati posho la aina yoyote. Kwa hivyo, niiombe wizara yako na niiombe serikali kwa jumla vijana hawa au wazee hawa, maana washakuwa wazee sasa wafikiriwe wawweze kupatiwa posho ili wawze kuwa na moyo wa kuifanya ile kazi.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye suala la mazingira. Kwenye suala la mazingira kwenye eneo letu kuna uchimbaji mkubwa wa mchanga, lakini watu wanapopewa vibali vya kuchimba mchanga naomba kuangaliwe sana lile eneo ambalo linachimbwa ule mchanga. Kuna maeneo yanakuwa yana minazi na minazi inakatwa watu wanachimba mchanga na wanaharibu mazingira.

Lakini pia hao wanaopewa vibali basi waambiwe kwamba wakimaliza kuchimba mchanga yale mashimo wapande miti ili ile ardhi iweze kurudi tena. Lakini badala yake mashimo yale yanaachwa, yanabakia kuwa mashimo hatima yake yanaleta madhara kwa wananchi na kwa watoto wetu. Kwa hivyo, naomba sana hawa watu wanaopewa kazi hii ya kuteka mchanga mkae nao na muwaelimishe kumaliza hii kazi basi wapande miti ili ile ardhi iweze kurudi tena.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la uharibifu mazingira kuna Kiwanda cha Sukari pale kipo Mahonda, kiwanda hiki kinapozalisha yale maji yake machafu yanamwaga kwenye mito na mito ile ukiangalia wananchi wetu ndimo wanamolishia mifugo yao. Lakini pia wananchi wetu hao ambao wanashughulika na kilimo maji yale wanatumia kwa kumwagilia vilimo vyao. Na maji yale kama tunavyotambua ni sumu kubwa sana yakianza kuingia kwenye mito ile hata majani yote yanakufa. Kwa hivyo, niiombe serikali,

niiombe wizara kukaa na muekezaji huyu kutafuta njia mbadala ya kupitisha yale maji yasiweze kuharibu mazingira ndani ya mito ile.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe pamoja na Mhe. Waziri, naamini kwamba Mhe. Waziri ni mama yetu na siku zote mama ni mtu mwenye huruma, mwenye imani na hulea watoto wake vyema. Ninaamini kwa vilio vyetu hivi sisi watu wa majimbo basi ataweza kutusaidia kwa kupitisha huruma zake hizo.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu huu kwa kusema kwamba baba wa taifa alitwambia kwamba, kama tunataka tuendelee tunahitaji mambo manne. Tutahitaji siasa, ardhi, watu na uongozi bora. Mimi nimwambie Mhe. Waziri kwamba, ardhi inabaki kama ilivyo lakini jamii inazidi kuongezeka. Ardhi inachukuliwa na maji, ardhi inajengwa kiholela, ardhi inaharibiwa. Nimuombe mama tu anambie kwa kauli yangu hii ana mpango gani wa kuitekeleza kauli yangu hii niliyozungumza hapa.

Baada ya kuzungumza ardhi, nije katika masuala ya usajili. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri, kwamba suala la usajili wa ardhi bado wananchi wa vijijini hawajapata elimu ya kutosha kusajili ardhi zao. Na nimuombe waziri kwamba afanya juhudi zozote ili afikikishe elimu hii vijijini ili wananchi wa vijijini wapate elimu ya kusajiri ardhi zao, hususan ardhi za watu waliorithi shirika. Hii inatokana kwamba watu wengi waliorithi ardhi hizi hawana nyaraka. Kwa maana hiyo wanapotaka kusajili ardhi zao hutokea mgogoro kati yao kutokana na kukosa elimu, kwa maana ninamuomba Mhe. Waziri, apeleke elimu hii vijijini ili wananchi wapate elimu ya kusajili ardhi zao.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri kwamba hivi sasa limetokea kundi la watu ambao wanadai kwamba ardhi ni zao, na huyu ana nyaraka bandia kudai ardhi hizo, na pale ambapo wananchi wale hawana usajili wa ardhi au hawana nyaraka, basi huwa ni kishindo kikubwa na ardhi hizo huchukuliwa na kundi hilo.

Mhe. Naibu Spika, mfano mzuri wa kundi hilo limenijia mimi katika kijiji changu kinachoitwa Mkamandume, wamekuja watu hawapungui 50, wanadai kwamba ardhi hiyo ni yao na wana nyaraka kamili. Kwa maana hiyo wale waliokuwa hawana nyaraka pale walihitajika waondoke.

Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri, hivi mtu kumiliki ardhi ili iwe yake pale anatakiwa akae miaka mingapi katika ardhi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika Mahakama ya Ardhi. Mheshimiwa namuomba Mhe. Waziri kwamba Mahakama ya Ardhi niipongeze kwamba inafanya kazi zake vizuri sana, lakini pia naiomba Mahakama hii iangalie zaidi kwa mashamba yanayokwenda pale yaliyokuwa hayana nyaraka. Mashamba ambayo hayana nyaraka kuchukuliwa na wachache, na huku ardhi ya watu wale wamezimiliki kutokana na urithi huo walionao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atapokuja katika masuala haya anambie hao watu waliokuwa hawana nyaraka huwa hawana haki? Kwa sababu watu hutengeneza nyaraka bandia, wakazipeleka Mahakamani na matokeo yake ardhi zile huchulikuwa na watu hao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika matumizi ya ardhi. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ardhi inaanza kupungua na watu wanaongezeka kama nilivyozungumza mwanzo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri asiweke mipango mengine tu na vijijini pia apange masuala ya matumizi ya ardhi, kwani tayari ardhi ya mjini inamalizika, na wanaotaka kutumia ardhi tayari wameshaanza kuja vijijini, kwa maana hiyo wataivamia na ardhi ile itamalizika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anapopanga matumizi ya ardhi basi na matumizi ya vijijini nayo apange vile vile.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika Mamlala ya Maji. Kwanza niipongeze mamlaka katika jimbo langu nasema nakaribia asilimia 97 au 98 kwamba vijiji vyangu vimebahatika kupata maji, lakini nimuombe Mhe. Waziri kwamba matangi yale yanayopitisha maji yale hayasafishwi. Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba matangi yale angalau apange muda basi wafanyakazi wake au hata kama sisi Wawakilishi tushirikiane nao katika kuyasafisha matangi yale, kwa sababu tunataka maji safi na salama, hatutaki maji tu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika suala la umeme. Mhe. Naibu Spika, suala la umeme ni muhimu katika maisha ya binadamu, na vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwamba katika Jimbo langu la Chonga kuna vijiji kidogo sana ambavyo bado havijapata umeme. Lakini nimuombe Mhe. Waziri kwamba anapopeleka umeme vijijini basi na nguzo zake apeleke mpaka katika nyumba, kwa sababu watu wetu ni masikini, hawana uwezo, uwezo wao ni mdogo lakini nguzo Mheshimiwa huwepo mbali na nyumba za watu. Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri angalau nguzo zake zifike kwenye nyumba tano basi angalau asifikishe nguzo moja, kwani

wananchi huwa ni mbali, karibu ya nguzo mbili mpaka tatu huwa wanahitaji nguzo. Kwa hiyo, Mhe. Waziri namuomba anapopeleka umeme vijijini basi na zile nguzo angalau nyumba tatu ziweze kufikiwa na wananchi kwa ajili ya kupata mahitaji ya umeme.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu ni masikini hawana kitu, kwa hiyo angalau kupata ule umeme huwa inawasaidia. Lakini wanapokosa umeme huwa matumizi yao ni madogo lakini pia nguzo huwa mbali na matumizi ya umeme huwa hawayapati.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika mazingira. Mhe. Naibu Spika, suala hili katika ukanda wa mashariki wa Kisiwa cha Pemba namuomba Mhe. Waziri alitilie mkazo, kwa sababu tayari mazingira katika ukanda wa mashariki wa Kisiwa cha Pemba umeanza kuathirika.

Mhe. Naibu Spika, mazingira ya Kisiwa cha Pemba suala hili limekuwa ni gumu na linaanza kuathiri. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kama alivyozungumza mwenzangu kwamba kuna watu wanachimba mawe, mashimo hayafukiwi, ni hatari kwa maisha ya binadamu, kuna watu wanakata miti ovyo, hivyo tayari bahari imefumuka, kwa maana hiyo kila kinachopandwa katika ukanda huo wa mashariki huwa hakioti na hakimei. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri afanye lolote lile lakini ukanda huu auangalie ili mahitaji ya wananchi yaweze kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu kwa leo ni huo, nimuombe tu Mhe. Waziri kwa hayo niliyoyazungumza basi baadae anipe maelezo kidogo, na mimi niridhike na hotuba yake naipitisha kwa asilimia mia kwa mia.

Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, na mimi nichangie kidogo katika hotuba ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Kwanza nimpongeze sana kwa hotuba yake, nimpongeze na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ardhi Mhe. Hamza Hassan Juma kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yetu ya Kamati.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, niungane na nyinyi kwa kunipa afya njema kama tulivyokuwa tupo hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nitoe pongezi kwa wizara zote kabisa zilizopo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mawaziri wake, lakini pia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira niipongeze kwa kila juhudi zinazochukuliwa, kwa sababu kila siku tunasonga mbele sio kama tunarudi nyuma.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wetu wa wizara hizi wanajitahidi sana, hawana usiku wala mchana, hawana Jumamosi wala Jumapili, hawa ni askari, kusema kweli wana kigezo cha askari, maana yake hata saa nane za usiku basi umeme ukikukatikia unajua ukimbilie wapi.

Kwa hivyo, hili kwanza nilishukuru sana, pamoja na malalamiko ya watu na matatizo mengi, lakini niwashukuru kwamba tunafanya kazi kweli kweli kwa jitihada za wananchi kwa kuwaondolea matatizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme kidogo kwamba tuna matatizo katika wizara zetu hizi hasa wizara za maji na wizara ya umeme.

Mheshimiwa tumetoa nafasi kwa mafundi ambao wanakuwa mara nyingi wanatengeneza vifaa kwenye nyumba, wanafanya *fitting* za mabomba kama mifereji, wanaunganisha kwenye mabomba makubwa haya pengine hata nafasi sio zao. Lakini hawa watu ambao tumewapa nafasi hizi wanatuletea matatizo, kwa sababu mimi ningeishauri wizara sana, kwamba watu wataruhusiwa kuweka fitting za umeme na wale ambao wataweka *fitting* za maji kama kuna kibali cha wafanyakazi ambao ni watu wa kawaida, basi wangelitambulika. Sio kila mtu anayejua kukaza *pipe* akatoboa bomba, sio kila mtu anayejua kuweka *switch* akaunganisha umeme, matatizo haya yanatufanya tuunganishe matatizo makubwa na lawama zinawajia serikali.

Mhe. Naibu Spika, tunaunguza nyumba kwa matatizo ya ufundi, tunaharibu miundombinu ya maji kwa matatizo ya ufundi wa kawaida. Kwa hiyo, mimi ningemshauri sana Waziri, suala hili akalitizama kwa kina pamoja na watendaji wake, kama kutahitajika mafundi wa nje, basi wawe kidogo waliokuwa wamepata kibali cha kufanya, sio kila mwenye *pipe* yake akafanya tu hili jambo ndio matatizo mengi yanatufikia.

Kwa hivyo, ningeshauri sana waziri katika masuala haya mawili ya afya na Wizara ya Maji wakajitahidi kadiri ya uwezo wao kuhakikisha maji na umeme hauchezewi ovyo ovyo ukatuletea matatizo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ningeshauri zaidi masuala haya ya ardhi ambayo mwenzangu mmoja alizungumza kuhusu habari ya Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ya Ardhi ina kazi kubwa sana, kwa sababu miundombinu yake hasa katika kuhukumu inahusisha vitu vingi sana, na Majaji kwa kweli wanastahili sifa wanaohukumu kesi hizi. Maana yake Mheshimiwa kuna vipengele vingi vinavyofanya mpaka kesi ikasimama au kesi ya kushinda. Mhe. Naibu Spika, pengine mtu ana shamba tokea enzi za 1800 huko hata halijulikani linakwenda kwa mdorongo wa watu na kwa mipango tofauti, nyaraka za kiarabu, mambo mengi, mvutano mwingi mpaka inafikia mtu yule kupata haki yake. Kwa hivyo, kwa kweli Jaji hawa wanaohukumu Mahakama hizi za ardhi wana mahangaiko makubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia watu hawa wanachukua vigezo kutoka Kamisheni sijui za Wakfu, watu wengine ni waongo wanaleta visingizio vyengine na matatizo mengine inabidi Jaji akae kulitazama jambo hili kwa upeo sana.

Kwa hivyo, ningeshauri sana hawa watu wa Mahakama ya Ardhi wakajengewa uwezo, baadhi ya mambo mengine wanapewa ushahidi uliokuwa hauna maana, na unatoka katika vikundi tofauti tofauti. Kwa hivyo, ningeshauri sana suala hili, sisi hapa tuna *system* kama ya upande wa magari, upande wa magari mtu ana nyaraka zake, ana makaratasi yake tokea gari ilikotoka mpaka inapomfikia. Lakini mwisho Zanzibar ikiingia hapa inapata kadi maalum na namba yake maalum na ile huwezi tena ukaipata pahali pengine zaidi ya *ZRB* kwa jina na kwa vitambulisho maalum.

Kwa hiyo, mimi ningeshauri kuondoa mzozo huu kwa Wizara ya Ardhi badala ya kupima na kuhakiki nyumba hii ni ya nani, kiwanja hiki ni cha nani, maelezo haya tusichoke Mheshimiwa kuongeza upeo wa kwamba tuanzishe tena hata kama ni *ZRB* nyengine.

Mtu apewe hati zake, apewe na kitambulisho kile iwe kama ndio kitambulisho cha nyumba, ndio kama kitambulisho cha gari yake, mtu akikitoa kile ndio ametoa nyumba, sio mtu makaratasi mnatiliana saini huku mitaani, hivyo ndio inakuwa kesi hazishi na matatizo hayaishi. Lakini kama tutatafuta ile *identity card* maalum ambayo inakuhakikishia kwamba hiki ndio kitu dhamana hawezi kukipata zaidi ya *ZRB* basi hatutofanya masuala haya ya nyumba kuuzwa mara nne, kuuzwa mara tano, unamwambia kadi iko wapi, kwa hivyo akikupa kadi unajua hiyo nyumba ni yake. Mimi ningeshauri ili kupunguza hayo matatizo na *ZRB* mtambo wanao hapo watatusaidia tu tutaunganisha huko huko kwenye maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, ningeshauri zaidi katika hali tunayokwenda nayo Wizara ya Ardhi ikajitahidi kutafuta pesa kwa njia yoyote.

Mheshimiwa Zanzibar siyo kubwa, kwa hiyo ikatengwa maeneo maalum ukanda huu mpaka hapa hautojengwa, ukanda huu mpaka hapa ni maeneo ya viwanda, ukanda huu mpaka hapa ni mabonde ya kulima tena ya mpunga, ukanda huu mihogo, mpaka tukafikia kwamba mtu anakwenda wapi, lakini Mheshimiwa leo utamkuta mtu kwenye shamba anajenga anakwambia pangu.

Mhe. Naibu Spika, ardhi ni mali ya serikali na lazima akubali masharti. Nchi za wenzetu yale maduka tu yanafungwa saa sita, utafunga saa sita, ukitaka funga saa ngapi hairuhusiwi. Lazima serikali ichukue mkondo wake, isifate tu watu mpaka wakawa tena hakuna hata *discipline* ya nchi, kila mtu anafanya anavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, uhuru ukiwa mwingi unakuwa ujinga na unazidi, lazima tutizame kwamba serikali inaweka mipango gani na hii inafuatwa, kwa sababu serikali kila siku inaweka mipango mizuri mtu mmoja asichafue kwa sababu ya kitu chake.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi unamkuta mtu ana bomba lake la mfereji ndani ya nyumba yake analiachia maji anakwambia yangu wala huthubutu kwenda kumwambia kitu wala wizara haichukui hatua yoyote.

Mhe. Naibu Spika, maji yale yakimwagika kama nina utaalamu wangu tu ninaoufahamu basi *pressure* ile inamalizika pale haiwezi kusogea kwengine. Kwa hivyo, utakuta nyumba tatu zinamwaga maji ina maana nyumba za mbele hazitopata maji. Kwa hivyo, ningeshauri Mheshimiwa kwanza nikwambie hawa wenzetu wa Wizara ya Maji wanapotaka kwenda kufungua maji katika maeneo fulani basi wafuatilie, kwenda kukagua mabomba gani yanavujisha, kitu gani kinatoa na hata kutoa *offer* ya zawadi atakayetoa maelezo yoyote kuhusu uharibifu wa maji sisi tutamzawadia kitu kwa siri.

Mhe. Naibu Spika, maji ni miundombinu na inalalamikiwa na ndio matatizo, kama huna maji ofisini hukai, nyumbani hakupikiki na maji ndio uhai. Kwa hivyo, ni lazima maji yalindwe, serikali hapa inatafuta kila mbinu ya kutafuta maji ukiyapata unayachezea. Hata Mwenyezi Mungu atakuwa hayuko radhi na sisi, lazima maji tuyalinde. Kwa hivyo, ningeshauri sana ikawa maelekezo kama hayo yana upeo zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka nizungumze na suala la matumizi bora ya ardhi. Mheshimiwa tunazungumza sana masuala haya kwamba Zanzibar ni ndogo ikiwa ina uwezo wa maeneo ya kufukia tukaweza kuongeza ardhi bahari ni kubwa, hivi vigezo vyengine vya wenzetu hawa wazungu mbona wao kwao wanafukia, sisi ndio tushindwe, watwambie kuna mikoko, watwambie kuna kitu gani.

Mhe. Naibu Spika kila siku tunaambiwa hapa kwamba akili za kuambiwa changanya na zako, hivyo masuala kama haya tunaona yana umuhimu tuangalie, na wewe kwa sababu waziri wangu ardhi ni mtu wa Chake-Chake asilimia kama 50 umesoma pale, unapajua vizuri. Mhe. Naibu Spika, Chake-Chake ina upeo na iko juu ya kilima ambayo haina maeneo mengi ni mlima na bonde.

Mhe. Naibu Spika, eneo letu la Tibirinzi limekaa vizuri sana kuanzia pale Qatar mpaka kwa Makamu wa Pili wa Rais, ni eneo ambalo limekaa vizuri sana. Kwa hiyo, ningekushauri wewe kabla ya kufanya, wala sitaki nizungumzie neno lolote, nakuomba uje pale tuangalie na wataalamu wako nini pa kuweza kutafuta mji wetu tukaweza kuuweka wa kisasa, wa Qatar, kama jina lilivyo.
Juzi nilikwambia hapa miji ya Chake-Chake yote imepewa majina lakini pale ni Qatar, soko kubwa limehamia, watu wameshajenga na bado watu wana upeo.

Mhe. Naibu Spika, na sasa hivi nataka nikwambie kwamba watu wale wa mikononi Chake-Chake wamekuwa wengi, hivyo tukiitengeneza Qatar tukawafungulia maduka basi mapato yataongezeka. Lakini kitu cha mkononi hupati pato zaidi ya kumfukuza mtu kwa polisi na kumuhangaisha atakwambia nikakae wapi.

Sasa ningeshauri kwa suala hili la Qatar sitaki nilisemee sana, nakuomba wewe waziri njoo Chake-Chake mimi nipo na miundombinu iwepo na ikiwezekana Mhe. Haji Omar Kheri awepo, Waziri wa Mawasiliano awepo tuje tuangalie Chake-Chake tutaifanya nini.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hivi sasa tukimaliza bajeti hii ni kwamba barabara inayotoka hospitali ya Chake-Chake kuelekea Tibirinzi itaanza kujengwa. Eneo la Qatar ndio litalojengwa, tunaweza tukatengeneza miundombinu ya barabara baadae miundombinu ya kujaza na kurekebisha tukahitilafiana tukaharibu pesa za serikali. Kwa hiyo, ningeshauri kabla ya barabara haijaanza na wewe ukawepo na Mhe. Haji Omar Kheri akawepo, na mawaziri wanaohusika wakawepo tukatizama Qatar inapangika vipi,

tusichokore chokore tu, tuujenge mji uwe wa kisasa na maeneo mazuri sana. Kwa hivyo, ningeshauri sana katika masuala hayo.

Mhe. Naibu Spika, nirudi tena mwenzangu mmoja alizungumza kwamba watu wetu wa Shirika la Umeme hawa watu wanatakiwa lazima kwa hali yoyote wakatiwe bima ya afya, ikiwa ni mchango utatoka kwake, ikiwa ni tatizo litatoka kwake, lakini kuna haja ya watu hawa kupatiwa bima ya afya kwa sababu ya mashaka yao, wanapanda juu na umeme ni hatari, wanakwenda usiku, wana mashaka mengi.

Kwa hiyo, ningeshauri sana watu hawa wakafanyiwa bima ya afya haraka iwezekanavyo, kuwalinda maisha yao na kukulinda hata wewe, kwa sababu haitokuwa tena fulani yuko hospitali, bima itakuwa inamlinda, ningeshauri sana hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme tu hata Mkurugenzi wetu huyu wa umeme anajitahidi kusaidia umeme sana.

Umeme hasa maeneo ya Pemba hili shirika nataka tulipongeze sana, shirika hili linafanya kazi kisiasa, shirika hili linafanya kazi kibiashara lakini shirika la umeme ndio shirika linalokopwa kweli kweli, tunalivuta kila upande.

Mheshimiwa Shirika hili linapeleka umeme kwa nguvu za kisiasa, wakati mwengine hata watu watano hawatimizi kutia nyumba, lakini mabilioni ya pesa yanapotea kuvuta umeme na Shirika halikatai linapeleka umeme; wananchi wanapiga kelele hatupati umeme na wala wao hawautumii.

Kwa hivyo ningeshauri kwamba Shirika kwa sababu linaisaidia Serikali, Shirika kwa sababu linafuata biashara, Mheshimiwa Shirika na Serikali na vyanzo vyengine Mheshimiwa hili Shirika wanalikopa sana, walilipe liendelee, wanalikopa sana Mheshimiwa hili Shirika, nalo linakopesha, lakini nalo linakopwa sana, madeni Mheshimiwa yanakuwa mengi, tujitahidi Wizara hizi tulipeni madeni Shirika liende mbele tutaliua, nguvu yake ndogo, kwa hivyo ningeshauri sana.

Mhe. Spika, halafu Shirika hili lina mashaka mengi, linanunua umeme Bara, linashusha gharama za *units* kwa kuwasaidia wananchi, tuliangalie kwa kina Shirika hili, wewe unanunua kule *unit* karibu shilingi mia tatu sijui mia ngapi, unamuuzia mtu mia moja hamsini, *fifty percent* unamshushia tena, bado Shirika wewe unalikandamiza, tena na wengine wanaiba umeme he! Mheshimiwa hilo

Shirika si litakuwa ng'ombe unamkamua mpaka damu, tutaua, tujitahidini kulisaidia.

Mhe. Naibu Spika, halafu Shirika hili hili la umeme ndio Shirika la dharura hasa usiku, ukizimwa umeme unatukana, joto hamkaliki kila kitu.

Ningeshauri kwanza Shirika hili la umeme na la maji lakini sana la umeme lipatiwe vipando vidogo vidogo vya Vespa, hakuna ulazima wa magari sehemu zote, sehemu nyengine anatakiwa fundi mmoja lakini lazima itoke gari, linatoka tu *Land Cruiser* linatoka gari gani kwa kupeleka kitu kidogo tu, lakini kina umuhimu, sasa Vespa inasaidia kufanya haya mambo ambayo ya dharura. Kwa hivyo ingeisaidia sana zikanunuliwa Vespa ili kuweka habari hizo sawa.

Mhe. Naibu Spika, lakini sasa nije kwenye habari za mazingira, naelekea tena Mheshimiwa mazingira yetu mimi nasema Mheshimiwa tumejenga sana.

Katika miaka ya 1970 miaka ya 1980 mpaka miaka ya 1990 Zanzibar haijakuwa na mafuriko na mito tunayo, maziwa tunayo, mabonde tunayo, sasa haya mabonde na haya mashimo ya maji na haya Mheshimiwa hii nasema tena ni hazina, Mwenyezi Mungu akikupa mito akakupa na maziwa haya Mheshimiwa ni hazina, tusikimbilie kuyafukia, tusikimbilie kwamba maji tuyapeleke baharini, Mheshimiwa maji yakikusanyika pahala sijui nyie wataalamu mna *means* gani inayovuta kati ya juu na kwenye ardhi maji yanavutana baina ya ardhi, unatoa hewa baridi, ina afya fulani ya binadamu, ndio ukakuta sasa hivi sisi hatuna afya, likitoka moto linakuja mwilini moja kwa moja halipozwi, tunafukia mashimo, tunayaondoa haya mamito.

Mheshimiwa hapa lazima tutafute utaalamu nyumba tuzivunje zilizokuwa ziko karibu na mashimo, tuache maji yasambae yatulie.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Dakika tatu Mheshimiwa ongeza mbili ziwe tano Mheshimiwa kwa hisani yako.

Halafu Mheshimiwa kidogo nizungumzie habari za mazingira. Mheshimiwa wewe ni Waziri wa Mazingira, kuna taarifa nyingi nyingi hutokea za kijingajinga mimi naziita, watu wanazosambaza sambaza, hebu kuweni *up to date* watu wa mazingira, ukisikia limetoka Waziri toa kwenye vyombo vya habari neno hili la uongo likiwa kweli tutalijua.

Sasa watu wanakaa wengine wanahama mbio, wengine wakiambiwa kesho kuna *el nino*, matokeo ya kipumbavu pumbavu wanayazungumza kwenye mitandao, muwe makini sana kuwapasha habari, watu wanakuwa na khofu, wengine bahari kesho hameni watu wanahama mbio wote, wanasema kesho bahari inapanda juu, ingawa mambo haya ni ya Mwenyezi Mungu lakini kama kutakuwa kuna habari maalumu iliyokuwa ya uhakika Serikali iseme haraka iwezekanavyo, tusiwaachie watu wakaitawala mitandao halafu wakawapa *panic* watu wakawa wanasumbuka.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine ninataka niseme Mheshimiwa usafi; ingawa huu anao Mhe. Haji Omar Kheri mambo ya miji. Mheshimiwa kuna viwanja humu mjini kiwanja utafikiri pori la wapi, kiwanja chako mwenyewe halafu hakina mazao, mwenyewe hayuko kakisahau ni pori humu humu mijini, mi-mbu mnafuga mbu, mnafuga majoka, Mheshimiwa mjini kutoka nyoka aibu, mji kama wa Zanzibar tumeshafanya mipango chungu nzima ya kufukuwa mbu hawafukuziki, mgomba uko Malindi, tokea lini mgomba ukakaa Malindi, migomba bwana akalime huko shamba, ng'ombe washahamishwa na migomba ihamishwe.

Mheshimiwa hapa mjini uwe mji, tunasema tu kila siku sijui hii Indonesia, sijui Srilanka itakuwaje na sisi hatutaki, hebu tukubalini iwe Srilanka, tukubalini iwe Indonesia, Seychelles, tukubalini kwanza sisi wenyewe, unasema mgomba wangu ukiukata si radhi Mungu atanilipia, mgomba gani huo si ukalime huko.

Mhe. Naibu Spika, lazima mji usafike, hapa kati kati barabara ilikuja huku barabara ilikuwa inaniuma ndio imekatwa juzi majani, mtu ana nyumba yake ametia uzio ameacha barabara hata nje ya barabara halimi anaisubiri Serikali ije imlimie, Mheshimiwa mlime ki-*memo*, watangazie watu wote kwenye majumba yao wasafishe, nje ya hilo tunajua sisi tukufanye nini, Mheshimiwa ni Serikali hii lazima...

Mhe. Naibu Spika: Mheshiwa muda wako umeisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: *Laa haula walaa quwwata,* la! Mheshimiwa, nashukuru nitapata wakati mwengine.

Mimi naiombea dua Wizara yetu ya Maji, jamani msipige mabuti hii Wizara Mheshimiwa Waziri amejitahidi vya kutosha kwa asilimia mia ipitisheni mumuamini, muaminini yeye, mumuamini na Ramadhani na mwanamke.

Mheshimiwa atatutendea haki, atawatendea wananchi, Mheshimiwa naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Viwe Khamis na baada ya Mhe. Viwe Khamis atapata nafasi Mhe. Said Omar Said na baada ya hapo atafuata Mhe. Shamata Shaame Khamis na ajitayarishe vile vile Mhe. Ali Suleiman Shihata.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Umeme.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo hii kusimama katika Baraza hili tukufu tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wake wote kwa ujumla kwa jitihada zao wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao yanayowakabili katika Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii ya pekee nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua mama yetu mlezi wetu Mhe. Salama Aboud Talib, kuwa Waziri wa Wizara hii. Nina imani kubwa kuwa mama yetu huyu zile changamoto ambazo zipo ataweza kuzitatua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko makubwa sana. Tokea nilipoingia ndani ya Baraza hili tukufu nilikuwa nikipiga kelele kuhusu tatizo la maji linalowakabili wanakijiji wa Kiuyu Kigongoni, lakini mpaka leo tatizo lile bado linaendelea, na ushahidi wa kutosha ninayo *Hansard* yangu niliyochangia tokea nilipoingia ndani ya Baraza hili. Na Mhe. Waziri, aliyepita aliniahidi kuliondosha tatizo hili, lakini mpaka kufikia usiku wa jana tatizo hili lipo.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kabisa, haiwezekani kisima kile kipo lakini kisima kile hakitoshelezi, na baadaye wanaopata maji ni wananchi wa Shehia nyengine, wananchi wa Shehia ya Kiuyu Kigongoni hawapati maji.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa ya wananchi wa Shehia ya Kiuyu Kigongoni, nimesimama hapa ili Mhe. Waziri, atakapokuja aje anipe maelezo ya kutosha kuhusu tatizo hili la maji lililopo ndani ya shehia ya Kiuyu

Kigongoni. Ndani ya Shehia ya Kiuyu Kigongoni wananchi hawapati maji na Shehia hii ni kubwa sana, ina watu wengi.

Mhe. Naibu Spika, zamani wananchi hawa walikuwa wanapata maji kutoka katika kisima ambacho kipo Ole. Baada ya kuchimbwa kisima ndani ya Shehia ya Kiuyu Minungwini bomba zile ambazo zilikuwa zinatoa maji zinasambaza katika Shehia ya Kiuyu Kigongoni zilifungwa ili wananchi wale waweze kupata maji katika kisima chao kilichopo ndani ya Kijiji cha Kiuyu Minungwini, lakini hichi kisima Mhe. Waziri, hakikidhi, maji yaliyopo pale hayatoshelezi kutokana na wana kijiji wale walivyokuwa wako wengi na shehia hizi ni mbili na hivi juzi tu nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza, kutokana na mashine ile ilivyokuwa iliharibika, lakini baada ya siku mbili mashine ile ilitengenezwa, tatizo lile liliendelea la kukosekana maji kwa wanakijiji wale wa Kiuyu Kigongoni, maji yanatoka usiku saa 7 mpaka 8.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa usiku ni wakati wa kupumzika, si wakati wa kuchota maji. Namuomba Mhe. Waziri, aje anambie ni lini tatizo hili litaondoka ndani ya Shehia ya Kiuyu Kigongoni, aidha kwa kuchimbiwa kisima chao au kwa kuruhusiwa bomba zile ambazo zilikuwa zinasambaza maji kutoka kisima kilichopo Ole ili ziweze kusambaza maji katika Shehia ya Kiuyu Kigongoni.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Shirika la Umeme. Niwapongeze watu wa Shirika la Umeme kwa jitihada zao ambazo wanazichukua usiku na mchana, tatizo lolote linalotokezea wanakuwa mstari wa mbele kulitatua.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Shirika la Umeme wana utaratibu wa kuwakopesha wananchi umeme.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake aje anambie ni taratibu gani ambazo zinatumika ili mwananchi aweze kupatiwa huduma hii ya umeme kwa kupitia mkopo, na baada ya kukopeshwa na baada ya kupatiwa umeme huu kuunganishiwa ni kiasi gani cha fedha ambazo anakatwa kila mwisho wa mwezi au baada ya kulipia umeme.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Idara ya Ardhi. Sasa hivi Zanzibar kuna migogoro mingi ya Ardhi, na migogoro hii ya Ardhi wanayosababisha ni Masheha pamoja na viongozi.

Mheshimiwa, migogoro hii ya ardhi wanaopata matatizo makubwa ni wananchi wetu ambao ni wanyonge, wananchi wana malalamiko, wanapokwenda ardhi mtu ana kiwanja chake tayari amekitegemea au ana shamba lake amelitegemea baada ya muda unaambiwa shamba hili tayari ameshapatiwa mtu mwengine, ukiulizia unahangaishwa kila siku unapanda ngazi mara huku mara kule. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nakuomba utakapokuja uje uniambie, ni lini migogoro hii ya ardhi itamaliza hapa Zanzibar, kwa kuwa migogoro hii imechukua muda mrefu, wananchi wetu ni wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anipatie maelezo na baada ya hapo naunga mkono asilimia 95 bajeti hii, asilimia tano nitaziweka mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kunihakikishia ni lini tatizo la maji katika kijiji cha Kiuyu Kigongoni litaondoka, kwa vile limechukua muda mkubwa.

Mhe.Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa, sasa basi tumpishe Mhe. Said Omar Said na baadaye atafuata Mhe. Shamata Shaame Khamis na Mhe. Ali Suleiman Shihata. Muda ukitosha kwa muda mdogo kabisa nataka nimpatie nafasi Mhe. Hamad Abdalla Rashid.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kwa kunijalia uhai na uzima na kuniwezesha katika kikao chako hichi kitukufu.

Nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ambayo ni nafasi nyeti kwa leo, kutokana na Wajumbe waliokuletea barua, nishukuru na mimi kuwemo katika Wajumbe hao.

Nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kumteua Mhe. Salama Aboud Talib kumkabidhi Wizara hii. Mhe. Rais hakubahatisha tu, Mwenyezi Mungu amjaalie aweze kutekeleza majukumu yote ya Wizara yake.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa hotuba aliyotuhutubia hapa jinsi alivyoiwasilisha, lakini pia nisiwasahau waliomsaidia walioko Unguja na Pemba ili kufikia kuwasilishwa hapa kwa umahiri mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambayo imebeba Wizara mbili, mchango wangu utakuwa mdogo sana, kwa sababu michango yote tuliitoa na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Mhe. Hamza Hassan Juma aliwasilisha kama tulivyoichangia, nimshukuru na yeye pia kwa namna alivyoiwasilisha hotuba hiyo tuliridhika sote, yale yote ni matakwa na maoni ya
wana kamati.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na suala la maji. Kama tunavyoelezwa kwamba maji ndio uhai, maji ni muhimu mno kuliko chochote duniani, yule mtoto mdogo ambaye hajaweza kula lakini maji anayahitaji kunywa.

Kwa hivyo, maji ni muhimu sana ulimwenguni, hivyo niipongeze wizara hii kwa jinsi ilivyofanya juhudi kubwa na bidii ikasambaza maji nchi nzima Unguja na Pemba, mijini na vijijini; niipongeze sana imefanya juhudi kubwa sana. Tulikuwa mbali sana hususan sisi kule Pemba, tulikuwa maji tunayasikia tu, tunatumia visima vya ndoo, tunasikia tu mifereji labda sehemu za mjini baadhi ya sehemu, lakini leo ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii tuliyopewa.

Mhe. Naibu Spika, lazima tuishikuru hii neema ndogo, ukishukuru neema ndogo basi utapata nyongeza, lakini neema ndogo ukiikufuru utapata dhiki. Mbali na kwamba tunapata maji ya kawaida, lakini naiomba sana serikali iongeze *speed* ya haya maji ili iweze kutusaidia kwa ajili ya kilimo. Kwa sababu kama tunavyoona misimu yetu wakati huu tafauti sana na tunakotoka huko, leo tukipata mvua siku tatu wakulima tunaingia kwenye makonde yetu tunalima haraka haraka kunaroa mashambani kule, baada ya kupanda vipando jua moja kwa moja. Sasa hapa panahitaji maji kutoka katika wizara yake Mheshimiwa.

Hapa maji ndiyo yatakayowawezesha wakulima wa vilimo vya muda mfupi ambavyo vinatusaidia kuliko vile vya muda mrefu. Hapa tunakuomba sana maji yawe ni mengi, ili yaweze kuwasaidia wakulima hawa kwa faida yao na faida ya taifa.

Pia, nishauri Mhe. Waziri kwamba kwa muda huu wa Mwezi wa Ramadhani maji tunapata, lakini zoezi hilo lisiishie mwezi huu wa Ramadhani tu, kwa sababu litakapoishia mwezi huu wa Ramadhani itakuwa umewapa wananchi mada mpya, mada gani, kwamba ah, kumbe ikimaliza Ramadhani mtu basi, Ramadhani ndio mwezi wa ibada tu, ikimaliza kila mmoja afanye analotaka unaona hata maji yalikuwa vururu wakati wa Ramadhani leo hayamo tena

yashafungwa kwa sababu basi ibada ishapita. Kwa kuwa yeye amepewa *switch* mbili na Rais wa Zanzibar, *switch* ya kwanza ni kutuwashia taa nchi nzima, na *switch* ya pili amepewa ya kutupelekea maji nchi nzima. Kwa hivyo, yeye ndiye kigezo kwa Wazanzibari, sasa atakalolifanya yeye na wao watakuwa wanafuata kwa sababu mtoto hufuata kichogo cha mlezi wake.

Kwa hivyo, hili zoezi liliopo sasa hivi la vururu ya maji, namuomba sana Mhe. Waziri alidumishe kwa muda uliobakia miezi 11 mpaka tufikie Ramadhani ya pili ijayo iwe hakuna watu waliokuwa na shida ya maji, ili tuweze kuwafahamisha wale wenzetu kwamba viongozi wa Chama cha Mapinduzi ndio wanaowapenda wananchi wa Zanzibarn pasiwe na ile fitina ya maneno begeje begeje. Namuomba sana Mhe. Waziri tuweze kufaidika kwa maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri afanye ziara ya kwenda Pemba, kule naamini atakuta wananchi wengi wanatumia maji ya visima vya ndoo. Sasa maji ya visima vya ndoo ni maji safi lakini sio salama, na watu wanatumia maji hayo kwa kuzowea tu. Unaweza ukaukuta mfereji hapa na kisima cha ndoo, lakini akakosa kwenda kuchota kwenye mfereji akachukua ndoo akachota kwenye kisima cha ndoo kwa sababu mwenyewe anayapenda zaidi yale, ni safi lakini usalama wake ni mdogo sana. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri aandae mazingira ya kuwapelekea dawa za kutia mule kwenye visima ili yale maji safi yaambatane na usalama.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ulipaji wa maji. Mimi siiti kulipa lakini ni kuchangia, hapa panahitaji taaluma ya hao wanaolipa maji wengi wana migogoro, watu wanaotumia maji ndani ya majumba yao au katika mitaa yao wanakwepa sana malipo au wanatoa malipo kwa shida sana, wanapofika maofisa wahusika wanaweza kuwakimbia au wakaleta mgogoro pale. Kwa hivyo, pale panahitajika elimu, wajue umuhimu wa ule mchango wa yale maji.

Nadhani elimu hii ilitolewa lakini kwa masheha tu, na sidhani kwamba masheha wamewakabili watu wote wakawapa taaluma hii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atoe taaluma katika kila shehia.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika nne.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante, nikitoka hapo kwa kuwa muda wangu umebakia dakika nne nije katika suala la umeme.

Niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuleta umeme kutoka Tanga mpaka kisiwani Pemba. Sasa Pemba tunaweza tukasema umeme ni bomba, tunajisifu kwa kila aina kwa serikali yetu baada ya kutuona muda mrefu tunahangaika.

Pamoja na kwamba umeme ushafika Pemba, lakini kuna baadhi ya maeneo katika jimbo la Wingwi bado wananchi hawajafaidika kwa umeme. Kwa mfano, Kinazini.

Mheshimiwa Kinazini baada ya Mapofu kuelekea Finya pana mji pale barabarani, hapo waliwekewa nguzo za umeme za *line* kubwa tokea Ramadhani iliyopita mpaka ya leo. Muda wote huo ilikuwa hakuna mteteaji wao pale, ndio nikaletwa mimi kuja kukupa hii taarifa Mheshimiwa. Kwa hivyo, naomba sana hapa atoe tamko lake kuwa wananchi wa Kinazini wamsikie. Je, anawaambiaje kama ndiye mwenye *switch?* Namuomba Mhe. Waziri awaeleze kwa tamko lake watu wa Kinazini lini watapata huduma za umeme, kwamba sasa hivi wanayatizama tu maguzo ya *line* kubwa mwaka mzima hatujui kwa nini tumekwama.

Katika kijiji cha Mianzini, Mapofu, Mapofu umeme umepita tu barabara kuu lakini ndani ya vijiji bado. Pia Mliani katika Shehia ya Sizini wenyewe wanaita Mikoani, Mnazi Mmoja katika Shehia ya Sizini ambapo pana kijiji kina nyumba kama 60 mpaka 70 hapana hata nguzo moja ya umeme. Namuomba Mhe. Waziri wenyewe wamsikie huko anawaambiaje.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Mheshimiwa nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa anayefuata ni Mhe. Shamata Shaame Khamis baadae ningemuomba Mhe. Ali Suleiman Ali asubiri kidogo kwa sababu nataka kumpa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi anataka kuchangia na yeye kidogo ili aweze kuendelea na shughuli zake nyengine.

Kwa hiyo ameomba muda huo aweze kuchangia yeye. Baada ya hapo atachangia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Awali ya yote na mimi napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na nikiwa mzima wa afya pamoja na Waheshimiwa wengine tukiwa tunaendelea na jukumu letu ambalo tumepewa na wananchi majimboni kwetu na maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja naomba kwanza kwa nia njema kabisa kwa moyo wangu wa dhati nimpongeze sana Mhe. Waziri mwenye dhamana ya wizara hii na Naibu waziri na watendaji wake wote, kwa jinsi ambavyo wamejituma kwa kipindi kifupi na tumeanza kuona kuna mwelekeo wa mafanikio makubwa.

Vile vile moja kwa moja leo katika uchangiaji wangu nianze kwa kupongeza juhudi ya serikali yangu tukufu, serikali sikivu kwa kazi kubwa nzuri ambayo imeifanya ndani ya nchi yetu katika dhana hii kubwa ya kupeleka huduma za maji na umeme na huduma nyengine hasa nikichukulia katika jimbo langu la Micheweni.

Jimbo la Micheweni nishukuru sana kwamba huduma hii ya maji inapatikana, na miundombinu ya maji katika Jimbo langu la Micheweni ipo inapatikana kwa kiwango kikubwa.

Vile vile suala la umeme nalo pia katika jimbo langu la Micheweni, umeme upo na huduma nyengine ambazo zinahusiana zaidi na wizara hii. Nathubutu kusema kwamba mimi katika jimbo langu zimefika.

Leo moja kwa moja nataka nichangie na kwanza kuinukuu wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa shirika kujenga kilomita 33.1 ya umeme na kwa umeme mkubwa. Vile vile katika kilomita 83.9 za *line* ndogo ya umeme vijijini na uwekaji wa *transformer* 35 na kusambaza umeme katika vijiji 36 kwa Unguja na Pemba. Ni jambo zuri sana na ni jambo ambalo la kupigiwa mfano.

Vile vile naipongeza wizara pia kwa kuweza kuthubutu katika kupeleka huduma ya umeme katika kijiji cha Sebudawa na kijiji cha Tupwe katika jimbo la Wingwi kwa sasa, lakini kwa hapo awali ambapo ilikuwa malalamiko makubwa ilikuwa ni jimbo la Micheweni.

Kwa hiyo, napenda niishukuru sana wizara kwa kazi kubwa nzuri iliyoifanya na wananchi wa pale sasa hivi wanaendelea kufaidika na huduma hii ya umeme.

Pamoja na pongezi hizi Mhe. Waziri naomba nimwambie kwamba Pemba katika Shirika hili la Umema naomba tuangalie sana katika maeneo ya Pemba kwa huduma zinazotolewa kwa wananchi wetu vijijini. Kuna malalamiko mengi mengine yana ukweli na mengine yanatafutwa kupatiwa ukweli zaidi kuweza kujithibitisha na kujiridhisha mapungufu ambayo yapo.

Juhudi za serikali na nia njema ya serikali imeweza kuonekana, serikali imetoa fursa ya kuwakopesha wananchi huduma hii ya umeme kwa njia ya mkopo, huduma hii inatolewa na tumeshuhudia lakini kwa watendaji ambao si waaminifu ambao sijui kama wana malengo yao wamekuwa wakiitumia fursa hii vibaya na kuendelea kuipaka matope Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pasi na kuwa na aibu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ambayo sitopenda kwa siku ya leo kumtaja mtendaji lakini ni mambo ambayo nina ushahidi nayo yamenifika mimi na nimeyashuhudia.

Kwanza niseme katika suala hili la utoaji wa huduma hii ya njia ya mkopo kumekuwa na madudu mengi yanafanyika ndani ya Shirika la Umeme.

Moja, elimu inayotolewa kwa wananchi wetu vijijini. Vijijini watu wana uelewa mdogo sana na mtendaji wa serikali au taasisi yeye ana dhamana ni moja katika jukumu lake kutumia fursa hii katika kuwaelimisha wananchi ili waweze kuelewa, lakini miongoni mwao kwa nia mbaya na kwa malengo yao binafsi hawawaelezi wananchi ukweli na badala yake wanaitumia fursa ya kutokuelewa kwao kuwaibia au kuweza kuwanyang'anya na kuchukua rushwa, au kupata fedha ambazo haziko kwenye utaratibu.

Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka uliopita au miaka miwili iliyopita mwaka 2014 kuna wafanyakazi ambao wanaitwa vishoka, ambao sio rasmi hawatambuliki na shirika kisheria. Watendaji hawa kwa kweli wamejitahidi, lazima mimi niseme hivyo, licha ya kwamba wao ni ajira binafsi wanajisaidia katika maisha yao lakini wamekuwa wanafanya kazi nzuri wakati mwengine ukilinganisha na wale ambao wamepewa dhamana wanalipwa mafao na serikali hii.

Kuna kijana mmoja katika jimbo langu la Micheweni ni maarufu sana, huyu ni kishoka, yaani ni mtu ambaye hayuko rasmi katika shirika, lakini wananchi wengi wamekuwa na imani ya kumtumia kijana huyu kwa kuwarahisishia kupata umeme kwa muda muafaka, na vile vile kuweza kupata huduma zinazostahiki kwa vile ambavyo labda wanaona wenyewe inafaa. Sisemi kwamba na yeye pengine haitumii hiyo fursa lakini anavyokubalika yeye na anavyofanya kazi imeonekana ni bora kuliko wale watumishi wa shirika lenyewe.

Sasa hili ni jambo la aibu, iweje serikali inalipa fedha kwa watumishi hawa na hatimaye aonekane mtu ambaye yuko nje ya *box* aonekane anatoa huduma nzuri, inakuwa kidogo ni jambo ambalo halitupendezi kama sisi miongoni mwetu.

Huyu inafika wakati kila eneo watu wanamtafuta yeye ndiye anayekuwa kama wakala wa kuwatafutia yeye huduma, yeye anatengeneza miundombinu ya kutengeneza daraja na wale watendaji wa wizara sijui kuna kitu gani hapa siwezi kukisema sina ushahidi nacho, ndivyo inavyokuwa wanafanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, yeye utakuta kwamba anaungana nao na unakuta siku moja, mbili, tatu anakuletea; lakini kuna mtu aliyefuata *procedure* anaweza akachukua muda mrefu sana hawezi kuipata huduma hii. Mtu masikini kakusanya fedha zake kutoka baharini kavua miaka mitano au miaka mitatu, leo inafika wakati kuitafuta huduma ile inakuwa ni kazi ngumu na badala yake wakati mwengine akiipata analazimika unaambiwa sijui uchangie gari. Huyo mwananchi wa kijijini Micheweni unamwambia achangie gari au mafuta ili aje apimiwe eneo lake, ili aweze kupelekewa huduma ya umeme kwa kweli ni jambo moja ambalo linasikitisha sana.

Wakati mwengine unaharakishwa hasa kama unataka haraka basi, hapo awali inaweza kuchukua labda miezi mitatu haya ni mambo yanatokea na yananung'unikiwa sana, ningeomba sana.

Vile vile na baada ya suala hili kukamilika kuna fomu za mikopo wakati mwengine zinatolewa ama kwa njia hiyo ya ujanja ujanja lakini mwananchi anaambiwa tayari ushaanza kupata *process* za mikopo, anaambiwa utakopeshwa, kweli umeme ule anaungiwa lakini akishaunganishiwa umeme sasa subiri katika malipo.

Yule wakala anakwenda kijijini kule kuwaona wahusika, jamani tayari hebu harakisheni zile fedha kwa sababu kuna ile mita itabidi mkopo lakini si

taratibu mikopo hazikuwa vizuri ujanja ujanja tu. Hatimaye anatoza fedha, zikipelekwa haziingizwi kwenye *account* unakuta kwamba sasa yeye huduma kashaipata anakuta analipia madeni tu.

Hivi ninavyokwambia katika shehia ya Maziwa ng'ombe, kuna watu watatu ambao nimewaunganisha mimi mwenyewe binafsi, nikenda kwenye shirika, nilipofika kwenye shirika nikaambiwa bwana kuna mtu hivi aaa! hao wanaweza kufanya haraka haraka. Lakini kumbe ilikuwa ni ujanja ujanja pia wanajuana wenyewe, nikaenda kuwaunganishia baadae watu wana fomu zao pale wakapeleka picha wanakopeshwa hatimaye siku mbili tatu anasema jamaa yule alikuja kutwambia bwana mpaka sasa hivi mita zimechelewa ili mnataka kuwahi.

Sasa wananchi kwa vile hawaelewi na hutuelewi watu wamekopa fedha na fedha zile hazikuingizwa kwenye *account* halafu sasa wanaendelea kulipishwa na sasa hivi wao wanaendelea kukatwa madeni.

Ni jambo la aibu kwa watumishi wa serikali kufanya jambo kama hili ambalo kwa kweli linapelekea kuitia madoa serikali, na ikaonekana serikali haina nia njema kwa wananchi wake, hili liko kwenye umeme.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri aandae kitengo maalum yaani iwe wanapita vijijini kwenda kusikiliza malalamiko ya wananchi katika suala zima la huduma hizi za umeme. Huko ndiko ukweli ambao ataupata, huko utawasikia watu wanavyolalamikia Shirika la Umeme.

Sasa naomba sana mimi nazungumzia hili kwa Jimbo la Micheweni na hayo nina ushahidi nayo. Kwa hiyo, sitaki kumtaja ni fulani lakini waziri naomba ichukuliwe kama ni changamoto tuboreshe huduma zetu. Serikali imetoa huduma kwa moyo safi, lakini iweze kuleta tija kwa wananchi wetu ili lile tatizo la kupunguza umasikini liweze kufanikiwa kwa kutumia huduma hii ya kupatikana kwa umeme vijijini.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la upangaji wa miji. Jimbo la Micheweni katika eneo la Micheweni mjini au Micheweni katika maeneo ambayo ndio taasisi za Serikali ambapo kuna maofisi.

Kwa mujibu wa historia ambayo tumepewa na wazazi wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alipofika Micheweni aliweza kufanya *appointment* au kuonesha *direction* kwamba wapi pafanyike nini na wapi pajengwe hospitali, wapi pajengwe nyumba za maendeleo. Lakini mote mule alimomutaja yeye au

alielekeza yeye kwamba mfanyike kwamba mumeenda vizuri na muko katika *site* ambazo ziko sawa.

Ni jambo la kushukuru sana kiongozi huyu Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi kwa nia njema aliyoionesha nchi hii basi aendee kumfariji huko aliko kwa kweli alionesha muanga mzuri.

Lakini sasa watendeji naweza kuthubutu kusema kama si waaminifu, hatutumii fursa hii kuzielimisha jamii zetu katika kuona kwamba jambo hili linaenda kama vile ambavyo *plan* ya mji inatakiwa ifanyike, na badala yake wamekuwa wakijenga holela pasi na kupata maelekezo yoyote, kweli fedha za kimasikini lakini kungekuwa kuna kitengo maalum cha kuweza kuwaelimisha.

Mimi wananchi wa Jimbo la Micheweni siwalaumu kwa sababu wao huyo mtu wa kuwashauri yuko wapi na jambo hili limekuwa wakilalamika. Kwa hivyo, nadhani kwamba imefika wakati sasa kutokana na ongezeko la idadi ya watu inayoongezeka katika visiwa vyetu vya Zanzibar Unguja na Pemba, ni dhahiri kwamba sasa tuchukue hatua za makusudi kuitumia ardhi yetu vizuri iweze kuleta tija na iweze kuona kwamba hilo ongezeko linalokuja basi tuone kwamba tunaelekea wapi.

Hivi tutakuwa tunasababisha migogoro mingi, ukienda maeneo mengine yamejengwa na ukiangalia haistahiki kujengwa, ukienda katika mengine vile vile unakuta kwamba migogoro na migongano mingi, wengine wamenyang'anywa ardhi zao pale zimejengwa na kuuziwa wananchi pasi na kuwepo kwa ridhaa zao wenyewe, hilo pia katika eneo la Micheweni limetokea.

Mhe. Naibu Spika, vile vile mimi pia naomba niseme kwamba kwa sasa katika Jimbo la Micheweni au Wilaya ya Micheweni iko haja sasa kuweko na afisi maalum ya kuratibu shughuli za ardhi na shughuli nzima za mambo ya Shirika la Umeme, kwa sababu ukiangalia jiografia ya Micheweni mtu atoke Micheweni fedha ya baharini aliyoipata hiyo shilingi mia tano tano halafu aunganishe nauli aende Chake chake akaifate huduma, hili jambo wakati mwengine unaweza ukahisi kwamba tunawatia adabu wananchi wetu.

Sasa maeneo ya afisi tunayo Micheweni pale, nadhani ni vyema sasa zile afisi ambazo ziko pale tuziboreshe na ule uratibu wa shughuli za ardhi, kwa sababu hata huko ardhi nako kuna mashaka hivyo hivyo unapotaka kupimiwa ardhi yako mwananchi wa kijijini haelewi afisi iko wapi.

Sasa wale wanaobahatika waende Chake chake nako ni hivyo hivyo, unaambiwa uchangie mafuta kwa ajili ya kufuatwa wewe kijijini uje upimiwe ardhi yako, hii inapelekea wananchi kujenga kiholela, kujenga maeneo ambayo huwezi kuruhusiwa, serikali baada ya miaka mitano uje usikie sasa inafanya operesheni ya kuvunja majengo. Itakuwa ni jambo moja hatujalitendea haki ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika tatu.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Zinanitosha hizo Mheshimiwa.

Kwa hiyo, mimi nadhani sasa hivi iko haja, na katika hali hii tuweze kuiangalia.

Nikienda haraka haraka katika masuala ya maji katika Jimbo la Micheweni kama nilivyosema maji yanapatikana lakini kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hivi Mhe. Waziri aangalie miundombinu ya maji iliyoko Micheweni ni ya muda mrefu mno tokea enzi za ukoloni na hatimaye sasa unakuta kwamba *stand* zipo za maji lakini maji kuna baadhi ya maeneo hayatoki kabisa.

Kwa hiyo, ninachoomba Mhe. Waziri tuangalie miundombinu ya maji ya Micheweni imekuwa chakavu, maeneo mengi watu hawapati maji kwa mfano kama Micheweni katika maeneo ya Uzunguni, ukija Shehia ya Majenzi, Shumba Mjini, Maziwa ng'ombe, Kiuyu kwa mfano kote huko Kijogoo, kote watu hawapati maji kwa ufanisi ambao unatakiwa.

Mimi nadhani kwamba tuiboreshe huduma yetu, wananchi waweze kuona kwamba kuna umuhimu na wao yale ambayo watapaswa kuyafanya basi na wao waweze kuyafanya kwa ufanisi zaidi.

Naomba sasa Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba mimi wizara hii kwa haraka haraka naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, kwamba kuona kwamba na mimi nakubaliana na hayo. Lakini pamoja na kwamba nimekubaliana na hayo kwamba bajeti ipitishwe, lakini ni vyema nipate maelezo na mkakati wa makusudi kuona haya ninayoyasema katika Jimbo la Micheweni hayaendelei kutokea tena. Wananchi wananung'unika sana na waone hizo hatua nilizozisema basi nazo ziweze kuchukuliwa ili kuona wananchi waendelee kuwa na imani na serikali yao. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shamata sasa tutampisha Mhe. Waziri wa Kilimo aweze kujibu baadhi ya hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru na wewe, nimshukuru Waziri na Naibu Waziri na timu yao yote kwa kazi nzuri sana waliyoifanya katika kipindi kifupi, wizara kubwa, nzito lakini wanaonekana kabisa wamepata viongozi mahiri na inaongozwa vizuri.

Nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati mimi namwita Kamanda Hamza Hassan Juma kwa sababu ni mzoefu sana katika nyumba hii, kwa kazi nzuri sana kamati waliyoifanya.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka kuzungumzia suala zima la Gesi na Mafuta ambalo limezungumzwa hapa ndani ya Baraza kwa ukali sana. Kwanza niseme tu kwamba Wazanzibari wote na viongozi wote ni jambo ambalo wamelisimamia sana, ni kuona Mafuta na Gesi yanaondolewa katika Muungano.

Nakata nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mhe. Rais Ali Mohamed Shein na Rais Jakaya Mrisho Kikwete waliahidi kwamba jambo hili litaondolewa ndani ya Muungano, na katika mazungumzo katika mapendekezo ya Katiba liliondolewa. Lakini bahati mbaya mchakato wa kumalizika na hatimaye Bunge likapitisha sheria ya kuliondoa mafuta na gesi katika Muungano.

Kwa hiyo, ni kweli kabisa *TPDC* kabla ya Muungano kuna maeneo mengi sana walikuwa wameyatenga, kwamba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu yako kwenye sheria ya Muungano. Si kwa sababu walikuwa wanakusudia kupora, ndio sheria ilikuwepo na ndio utaratibu uliokuwepo na ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Dkt. Ali Mohamed Shein na chini ya wizara inayohusika imetayarisha sheria tayari na tunategemea katika Baraza hili hili itakuja sheria ya kuweza kusimamia Mafuta na Gesi, ambayo na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwanza naomba tuipitishe sheria na hatimaye tumpe nguvu waziri na taasisi zitakazoundwa chini ya utekelezaji wa sheria hii ili waweze sasa ku- *identify* maeneo yetu ambayo yako kwenye mipaka na yale ambayo ni ya Zanzibar peke yake.

Hivi ni vya kwetu, na wala tusiwe na wasi wasi na hakuna nia mbaya kwenye Jamhuri ya Muungano kwamba jambo hili lisitendeke hata kidogo. Ndio maana tukapitisha sheria baada ya Katiba kukwamwa likapitishwa na likaondolewa, na mimi nilishiriki sana ili kuhakikisha kabisa Zanzibar inapata haki zake na Jamhuri ya Muungano upande wao wanapata haki zao.

Kwa hiyo, kwanza nataka niwatoe wasi wasi huo Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar, kwamba kinachongojewa sasa ni sheria tu ambayo tayari kwenye Baraza la Mapinduzi imeshapita, taratibu zote zimeshakamilika, na tunategemea baada ya shughuli za Baraza hili litapitishwa hapa na hatimaye utekelezaji uanze na maeneo yetu yatatangazwa rasmi, yatajulikana fedha itakayopatikana katika utafutaji wa Mafuta itakuja Zanzibar.

Mimi ninachoomba tu katika hili Wazanzibari tusije kuingia kwenye maradhi yale ya ***'Dutch Disease',*** kwamba mnapojua kunachimbwa mafuta tena mnaacha kulima, kufuga, kuvua mnangoja mafuta, hapana. Tuendelee na shughuli zetu za kawaida, tulime, tuvune, tuvue, tuchonge, tufanye shughuli zetu zote za kawaida. (*Makofi*)

Haya matumizi ya rasilimali hizi nchi nyingi sasa hivi wanaziweka kwa ajili ya vizazi vinavyokuja na ndio hasa hesabu zake zinatunzwa katika skuli maalum hazitumiki ovyo ovyo katika bajeti ya kawaida ili zisaidie vizazi na vizazi vinakuja. Kwa sababu ni rasilimali inayomalizika, hizi rasilimali zinazomalizika ni vizuri ukahakikisha vizazi na vizazi vinavyokuja vinafaidika. Itakuwa *percent* fulani inakwenda kwenye bajeti, lakini sehemu kubwa itajitahidi kwa sehemu kwamba wananchi wanaokuja mbele yetu wanafaidika nayo.

Nawaomba sana Wazanzibari pamoja na nia nzuri ya serikali tuiunge mkono tujitahidi sana kuungana na wawekezaji watakapokuja tusiwafanyie *sabotage* ya aina yoyote, tushiriki kikamilifu katika kuona kabisa Zanzibar nayo inabadilika katika kutumia rasilimali zake vizuri.

La pili Mhe. Naibu Spika, ni suala zima la uvamizi katika maeneo yetu ya kilimo na maeneo mengine ambayo yamekatwa eka. Hili jambo limekuwa tatizo kubwa sana.

Nataka nimpongeze sana Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" amefanya utafiti na ametoa orodha ya eka ambazo tayari zimeshavamiwa kwa kujengwa nyumba na kukatwa viwanja. Hili ni tatizo kubwa sana, ni tatizo linahitaji sana kuangaliwa, kwa sababu kama walivyosema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nchi yetu ni ndogo sana, na haikui inapungua kila siku, na watu wanaongezeka. Lakini watu wanaongezeka sasa hivi Mhe Mwakilishi suala la Msuka kwamba bahari inakula kituo cha KMKM diko linaondoka hasa hayo ni mazingira tunayoishi nayo.

Sasa ni vizuri na wananchi wakaelewa kama tuna mazingira hayo, tusipoelewa hivyo tukafikiria kwamba kukata mti kuvamiwa eka mabonde tukavamia kwamba inatusaidia sana .

Leo Mhe. Naibu Spika, tuna maombi zaidi ya 41 watu wanataka kuchimba mchanga, ukisoma kila bonde kila mtu anaomba ama kuna minazi 50 itakatwa au miti mengine mikubwa itakatwa au yuko karibu na bahari au yuko katika mazingira ya wakulima.

Sasa hayo ndio matatizo ya msingi ambayo yapo, naomba sana wananchi tuelewe tunalo tatizo kubwa sana la ardhi, tunahitaji kuungana na waziri na serikali kwa ujumla namna gani ardhi yetu tutaitunza vizuri kwa leo, kesho na kesho kutwa.

Vinginevyo hatuna ardhi inayoendelea, ardhi inaliwa na bahari, maeneo mengi yameharibika kwa sababu ya mazingira, wataalamu wanaita *man-made disasters* yamekuwa kweli kweli, hali ni mbaya sana, nenda kaangalie machimbo yaliyochimbwa, mashimo yameachwa pale miti haijapandwa ndio utaona athari ambayo inapatikana .

Tusisahau kisiwa hichi *level* yake na bahari ni ndogo sana, unapompa mtu idhini ya kuchimba mchanga mita 3 maana yake unakirudisha kisiwa chini mita 3 zaidi, na unayaambia sasa maji karibuni muingie mmalize kisiwa.

Yote hayo ni mambo hayo nataka yaeleweke, na ndio maana wizara naishukuru sana katika Idara yake ya Upimaji wamewaka utaratibu wa kuweza namna gani wataweza ku-*control***.** Inahitaji ushirikiano wetu, waziri na timu yake wamejipanga vizuri, tunachohitaji ni ushirikiano wetu

La tatu Mhe. Naibu Spika, ni suala zima alilozungumza ndungu yangu Suleiman Sarahan suala la mabonde haya, mito na maziwa ambayo yapo.

Jambo jema sana alilolizungumza tunahitaji sana hivi ni vianzio navyo vya maji vile vile, pamoja na kwamba yametuama pahala lakini ni vianzio. Ukivitunza vizuri unaweza pale pale ukapanda samaki, na kwa sababu sasa hivi tunaanzisha *hatchery* sasa hivi ya kutoa vifaranga vya samaki ni maeneo ambayo yanahitaji kutunzwa. Lakini lazima wananchi wenyewe wajue kama haya maeneo yanataka kutunzwa, kwa sababu unakuta mwananchi huyo huyo anajua kama ni eneo muhimu anakwenda kujenga karibu na eneo lile au anakwenda anavuruga mto kabisa uliopita pale, mito mengine imefungwa.

Pale kwetu Wawi Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na mito 7 ikitembea pale, sasa hivi kuna mito 3 inayotembea minne imeshakufa yote, kwa sababu watu wameingilia katika vyanzo vya maji wamevurunga kabisa mazingira, hali imekuwa mbaya sana. Kwa hiyo, naomba na sisi tunakubaliana naye kabisa tutaendelea na utafiti katika maeneo hayo tuangalie vipi vianze kutumika vizuri. Lakini na wananchi tunapowaambia jamaa tunataka tuhame sasa tutengeneze jambo fulani wasiwe wabishi, waelewe kwamba kuna nia nzuri kabisa ya serikali hii kutunza ardhi, ardhi tulinayo ni ndogo sana.

Nilikuwa namwambia, Mhe. Waziri hapa wa Tawala za Mikoa jana nilimkuta mtu na gari yake ya punda Maruhubi pale anatembea na punda pamoja na kelele zote za kutangaza hata habari hana, hatuoni tu binadamu walivyo, bado hawajataka kuelewa nia ya serikali katika kuweka mazingira yetu mazuri, mazingira yetu yakiwa mazuri watalii watapenda kuja, Zanzibar inauzika bila ya kitu chochote chengine, kinachotakiwa ni usafi na mipango mazuri tu ya Zanzibar. Mimi nafikiri tukishirikiana hatua hiyo tunaweza tukafanya kazi vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tulizungumza sana kuhusu kiwanda cha Mahonda na maji machafu yanayotoka pale baada ya uzalishaji.Tutashirikiana na Idara ya Mazingira na Wizara ya Viwanda na Biashara, na tuna vikao vingi sana tunafanya juu ya hili tutakwenda kukaa na wahusika tuone haya maji kwa kiasi gani yanaathiri mito yetu na hatua gani zinachukuliwa ili kuondosha matatizo yale ya taka. Nawashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niombe sana ardhi ni rasilimali muhimu sana. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipotoa eka 3 kuwapa watu ilikuwa ina madhumuni kabisa tuhakikishe kabisa vizazi na vizazi vinafaidika na ardhi hiyo. Kwa bahati mbaya eka nyingi sana zimeuzwa, nyengine watu wamejenga sasa waliouza bahati mbaya walouziwa hati zao zina matatizo vile vile, ukitizama orodha ya kesi tulizonazo sasa hivi watu ambao wameuziwa maeneo haya ya eka 3 yule aliyeuza siye hasa aliyepewa.

Kesi nyingi utazikuta hivyo, yule aliyeuza siye ambaye amepewa, sasa hili ni tatizo kubwa la msingi litakuja, tunaomba sana lisigeuzwe la kisiasa, ni suala la kisheria na kitaalamu tutalifanyia kwa mujibu wa sheria tuhakikishe utaratibu wa kutunza eka 3 unarudi ili vizazi na vizazi vifaidike mbele ya safari hii (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe Naibu Spika : Ahsante sana Mhe. Waziri wa Kilimo, sasa tumpishe Mhe. Ali Suleiman (Shihata) na baada ya Mhe. Ali Suleiman nitampa muda mchache sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid, na baada ya hapo kuna Mhe. Makame Said Juma ameniomba anataka dakika 5. Kwa hiyo, huyo atakuwa ndiye mchangiaji wa mwisho kwa upande wa Wajumbe.

Mhe Ali Suleimani Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji Nishati na Mazingira.

Mheshimiwa nakupongeza kwa kunipa nafasi hii lakini pia nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri na Naibu wake kwa kazi zao nzuri wanazozifanya hasa wanapotaka mashirikiano mazuri na Wajumbe wa Baraza hili nampongeza bila ya kuchoka.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitazungumza kwanza Mamlaka ya Maji niipongeze serikali kupitia wizara husika kwa wakati tuliokuwa nao wa mwezi wa Ramadhani kuwapatia wananchi wetu wote wa maeneo mbali mbali ambao hawapati maji kabisa au wanapata maji kwa upungufu.

Naipongeza serikali yetu hasa na rejea kauli ile ile kwamba serikali ina imani na wananchi wake, lakini pia nalaumu Mamlaka kwa utaratibu mbovu walikuwa nao katika utekelezaji wa kazi zao. Naweza kusema tu kwamba Mhe. Naibu Spika, baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Maji hawana uzalendo na nchi yao sababu nitazitoa .

Mhe. Naibu Spika, katika jimbo langu la Kijitoupele kuna visima kama 4 au 5 Ras al Khaima vipo 2, na serikali ilichimba kisima chengine Mwanakwerekwe hapa wanapoita Mwenge au Mwanakwerekwe "C", lakini pia Magirisi, Kwarara, Tomondo na Madina, lakini hadi leo visima hivi havijapata mabomba ya kusambazia maji.

Ninasikitika kwenye wizara hii au katika Mamlaka ya Maji taarifa yake iliyotoa katika ukurasa wa 30 kwenye jadweli Nam.6, "matengenezo ya miundombinu ya maji". Kazi zilizotekelezwa wametaja hapo katika namba moja utaikuta Mkunazini, huko siingilii, Elimu Mbadala siingilii lakini na Kwarara.

Nitamuomba sana Mhe. Waziri huko Kwarara walipotandika mabomba hayo wanipeleke ili tuyajue na wananchi wanasikia kwamba hili si kweli, ninakataa kata kata.

Mhe. Naibu Spika, jengine Mamlaka ya Maji hii hii, kama panatokea matatizo ya watu kukosa maji baadhi ya maeneo tunataka mpira mmoja, gharama yake haizidi shilingi laki tano au sita. Wanaweza kukwambia sisi hatuna pesa moja hata ya petroli hatuna. Lakini wakati wa mwezi wa Ramadhani ninawashukuru na nimeishukuru serikali kuchangia kwa wananchi wetu kwa ajili ya kuwapelekea maji, wanamiliki mamilioni ya fedha, wanazipata wapi fedha hizi, kwa mwezi mmoja wa Ramadhani gharama wanayotumia kusambaza maji kwa maeneo ambayo hayapati maji wanaopata maji machache. Hilo ninaliunga mkono lakini hizi pesa zinatumika nyingi sana. Kumbe wangekusanya pesa zile wakaandaa mikakati mizuri kuelekeza mambo yao kwenye maeneo mbali mbali hata visima ishirini au thalathini katika nchi yetu tungepata.

Naishauri serikali kupitia wizara hili waliangalie, hapa pana mchezo mchafu ninaweza kusema hivyo. Siamini, kwa sababu visima vimeshachimbwa vinakosa mipira mitatu minne, haizidi milioni tatu au milioni mbili. Lakini kwa usambazaji wa maji wanakodi gari kadhaa ambayo hayatambuliki yanatoka wapi. Hapa ninaweza kusema labda pana kitu kinatumika kwa maslahi ya wengine. Ndiyo nikatanguliza kusema kauli yangu nimefunga na huu ni mwezi wa Ramadhani, baadhi ya watendaji si waaminifu, ninamuomba Mhe. Waziri awe makini sana juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, katika vituo vya maji kuna eneo la Kijitoupele. Eneo hili limekuwa la biashara kubwa ya maji. Mimi nasema sikatai Mamlaka inataka fedha, lakini wananchi wa maeneo mbali mbali kama Meli Nne Uzi, unakwenda Taveta na kwengine mpaka Tomondo huko hawapati maji kutokana na maji yanayouzwa pale wanakuwa wanayazuia makusudi.

Nataka nijue Mhe. Naibu Spika, kupitia Mhe. Waziri huyu mtendaji anayetoa maji katika Kituo cha Kijitoupele ni kaajiriwa au kaajiriwa kibodaboda, kwa sababu haileweki. Lakini kwa taarifa ya wananchi wetu wanaotupenda na wanaoipenda nchi yao, wanasema yule anafanya kazi pale kwa kila gari moja anapata shilingi elfu mbili na mia tano kama sikosei. Hili nitataka nijue na tujue kama ni muajiriwa wa serikali ama muajiriwa wa kupitia kitu ambacho hakifahamiki. Nikasema ndiyo hayo labda pana mchezo ambao katika maeneo ya Mamlaka ya Maji.

Mhe. Naibu Spika, yakikatika maji baadhi ya maeneo hata ukipeleka ripoti, inaweza kwenda wiki moja, wiki mbili au mwezi hawatoki wafanyakazi wale kwenda kushughulikia maji yale, lakini kwenye kukusanya mapato ijapokuwa maji hayatoki wanakwenda. Hivyo nawapongeza wanapokusanya mapato lakini

mapato yale yalikuwa yaingie katika mahitaji ya wananchi hayawafikii. Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri Mamlaka ya Maji aiangalie.

Visima nilivyokuwa navyo ambavyo vinangojea matengenezo, ninamuomba Mhe. Waziri hili alichukue, Kisima cha Mwanakwerekwe Mwenge, Magirisi, Tomondo, Kwarara Madina, visima hivi vikipatikana vikiwezeshwa mabomba na *pumps* zake, ninaamini tatizo la maji Kwa Meli Nne, Mwanakwerekwe, Meli Nne Uzi, unakwenda zako mpaka Magirisi, Kijitoupele, Kwarara mpaka Tomondo itakuwa historia katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri madhali visima hivi vimechimbwa na vyengine na Ras al Khaimah hivi, vimekaa havina kazi vifanyiwe kazi hiyo. Katika vituo vya kuuzia maji hata sehemu za shamba, yaani vijijini ninaweza kusema, Koani kipo kituo kizuri kinahudumia Dunga na kwengineko.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wake pia waangaliwe kwa sababu hawana ukweli. Unakwenda kulipa umeme umekatiwa maji unataka kuungiwa, wanaweza kutumia wiki tatu nne hawaendi. Kwa hivyo kuungwa umeme ndiyo kupata kwa Mamlaka ya Maji, kwa sababu itakuwa na mashine yao inafanya kazi ili manufaa yapatikane.

Mhe. Naibu Spika, jengine niingie kidogo kwenye Shirika la Umeme. Mhe. Naibu Spika, shirika hili mimi kwa dhati nawapongeza kutokana na kazi, nguvu wanazozifanya na kazi za hatari kuliko kazi zote kwenye nchi yetu hii, ukiacha mwanajeshi na maaskari wetu wa vikosi vya SMZ na Mapolisi. Maana yake wale wapo *front line* kwa kuokoa nchi yao na usalama wa raia wetu.

Mhe. Naibu Spika, watu wa umeme halikadhalika wapo kama majeshi. Kazi zao ni ngumu na za hatari. Ukikatika umeme wakati wowote hata saa saba za usiku, ukiwapigia watatoka na watakwenda kuifanya kazi ile. Mimi nawapongeza pamoja na juhudi hii wanayoifanya, nawaomba wenzangu hili tuwasaidie kwa hali na mali kwa yale mambo wanayoyataka wayafanye kutokana na wakati.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika kuboresha vijiji vilivyopata umeme, Pemba vipo 20, Unguja vipo 17 nimevihesabu. Bahati mbaya narudia tena kauli yangu Mhe. Naibu Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi na mimi nazungumza katika Kijitoupele ni mjini ninaweza karibu, lakini bado umeme maeneo haya hakuna.

Namuomba Mhe. Waziri nishatoa kauli mbele yake. Mimi na Mbunge Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na wanaoishi hapa, tutachangia nguzo 15 hata leo tupo tayari. Na tunasema nguzo 15 hizi tunaisaidia serikali yetu, lakini namuomba Mhe. Waziri akimaliza bajeti yake, fedha za nguzo akachukue na Shirika tunawaambia hapa wanasikia wakachukue, zipo tayari watupelekee nguzo, wawapatie umeme wananchi wetu wa Madina ambao umeme toka kuwepo katika nchi hii hawajauona, wanauona katika maeneo mengine tu. Wanataka kuona *TV*, wanataka kupata maji safi na bila ya umeme hawawezi kupata mambo hayo. Hivyo Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri hili aliangalie. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jengine la mwisho kwa kuokoa muda niseme tu kwamba pamoja na matatizo tuliyokuwa nayo, Beit el Ajaib ni rasilimali kwa Zanzibar yetu. Bila ya Beit el Ajaib mtalii hata anayetoka nje ya nchi ambaye haijui Zanzibar, akifika pale atauliza iko wapi. Ni jengo, ni la historia, lina manufaa kwa nchi yetu na vizazi vyetu. Naiomba serikali kwa uwezo wake wote jengo lile lifanyiwe ukarabati unaofaa. Ufanyiwe ukarabati wa muda, siyo unafanyiwa ukarabati wa miezi mitatu jengo linaanguka tena. Fedha zinapotea nyingi, utendaji unakuwa mbovu.

Kwa hivyo, niseme tu Mhe. Naibu Spika, Beit el Ajaib liangaliwe kwa jicho la huruma na ufanywe ukarabati wa haraka, wakija wageni wajue wapi wanatembea na kupata historia ya nchi yetu. Lakini pia wataalamu wanaotoa historia kwenye maeneo ya ndani wawe wazalendo na wanaoijua historia ya nchi yetu, wasiende pale wakaondoshwa njiani wakaenda zao, kumbe wamepewa jengine kuliko yale waliyoendea pale.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, na haya niliyoeleza naomba yatekelezwe, sina tatizo na bajeti hii naipitisha kwa asilimia mia moja.

Na nitamuomba ushauri tu Mhe. Waziri tukimaliza tufuatane katika maeneo niliyomwambia akavikague visima, akakague mabomba yale tuliyoambiwa yametandikwa hapa na mimi nikayaone. Sina pingamizi naunga mkono hoja katika hotuba hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Hamad Abdalla Rashid na baada ya hapo atachangia Mhe. Makame Said Juma ambaye ameomba dakika tano. Naomba iwe hivyo dakika tano.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa ya kumpongeza Mhe. Waziri kwa kitabu chake kizuri ambacho amekipanga na wataalamu kwa vizuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwa sababu sitaki nipoteze muda kama ulivyoniambia nitumie muda mfupi.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye upande wa mapato kwa sababu ndiyo lengo kuu la serikali kuweza kukusanya mapato.

Mimi napenda nimwambie Mhe. Waziri wizara yake ina sehemu kubwa ya mapato kwa sababu ina umeme na maji. Lakini mapato ya wizara hii yanachangiwa kupotea kutokana na muhali, udugu na woga wa wafanyakazi wake wanaokusanya mapato hayo. Kwa sababu pengine mfanyakazi anaona tabu tu kwa sababu ni rafiki yake, ndugu yake kumwambia lipa maji. Na hiyo inasababisha watu kukatiwa maji kwa sababu hawalipi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza serikali kwa juhudi kubwa ya kuhakikisha kwamba wananchi wake wanataka wapate maji safi na salama. Na ningewaomba wananchi wajitahidi kulipa maji na umeme ili huduma hii ipate kukua katika maeneo mengine.

Mimi nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwenye jimbo langu nina asilimia labda niseme 99.9 tayari wananchi wangu wanapata huduma ya maji na umeme. Naipongeza wizara kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, ila ninamuomba Waziri nina vijiji vyangu vitatu tu, navyo ni Misufini, Mgogoni na Ditia kidogo. Hawa wana tunu ya maji na kwa sababu wapo nyuma miaka ishirini hawakuwa na mkombozi, walikuwa wakitumia juhudi za serikali tu. Kwa sababu serikali inawajali wananchi wake kuwapelekea maji. Sasa yule mkombozi wa kuvisemea vile vijiji ambavyo havijapata walikuwa hawana kwa muda wa miaka ishirini.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa Mhe. Waziri akija ku-*wind up* hapa anipe taarifa au anijuulishe, na nimefurahi kwa sababu ninafuatilia Afisa Mdhamini kaniarifu kwamba kuna kisima kipya kimejengwa *special* kwa wanavijiji hawa, vijiji hivi vitatu. Tatizo bado ni umeme tu. Namuomba Mhe. Waziri ikifika

sikukuu, leo hata unipe muda mimi, nataka sikukuu hawa wananchi wetu wapate maji safi kwa vijiji hivyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende kwenye huduma za mbali kidogo na kama Mhe. Waziri wa Afya yupo anasikia naomba ashirikiane vyema na Wizara hii ya Maji, ili mahospitali yetu yote ya Unguja na Pemba tuhakikishe kwamba yanapata maji masaa 24. Kwa sababu nimeangalia mahoteli mengi ya Unguja na Pemba yana tatizo la maji. Hospitali bila ya maji haiitwi hospitali. Operesheni hauwezi kufanyika bila ya maji. Muuguzi hawezi kumuhudumia mgonjwa yeyote mwengine bila ya kupata maji, kunawa kutoka mgonjwa mmoja kwenda mwengine.

Ningeomba Wizara hii ya Maji na Wizara ya Afya zikae pamoja ziandae mikakati maalumu, ya kuhakikisha mahospitali yetu yanapata maji ya mtiririko masaa 24 yote. Mfano hai kuna Hospitali ya Vitongoji pale mimi nilikuwa nafanya kazi pamoja na ya Chake Chake.

Hospitali ya Vitongoji pale hospitali hasa pana kisima, kwa kweli kile kisima kilikuwa kinatoa maji masaa 24 ukiwaka umeme tu maji pale tayari, lakini sasa hivi mtandao huu mpya wa maji uliopo pale wa Mchina, kila wakati yale maji saa nyengine yanakuwa hayatoki, na ukizingatia ile hospitali ina kambi ya kipindupindu mara nyingi na mara zote mpaka sasa hivi.

Ningeomba Mhe. Waziri wa wizara hii na Mhe. Waziri wa Wizara ya Afya tuhakikishe kwamba hospitali ile inapata maji. Kile kisima kifufuliwe, kiwe *special* kwa hospitali ile tu, ili maji pale yatumike masaa 24. Tumeshapoteza wafanyakazi wetu pale wa Wizara ya Afya kwa kipindupindu, yaani baada ya kuuguza wao na wao wameugua sasa. Hii inapoteza nguvu kazi na kuwavunja moyo wafanyakazi wetu.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana Mhe. Waziri washirikiane kabisa kuhakikisha hospitali ile inapata maji, na si ile tu hata Hospitali ya Chake Chake. Mfumo wake wa upatikanaji wa maji siyo mzuri. Mara nyingi ukienda pale jamaa za wagonjwa wanasononeka kweli kweli kwa kukosa huduma ya maji.

Mimi ningeomba tulizingatie hili, na hili sitolikubali nitahakikisha na mimi ninashirikiana na Wizara ya Afya na Wizara ya Maji kuhakikisha mahospitali yale yanapata maji masaa 24.

Kwa sababu moja katika huduma kuu ya nchini mwetu na wananchi wetu wapate huduma safi za afya na maji safi. Sasa tusipiganie wananchi wetu tu, wananchi tayari asilimia kubwa ndiyo wameshafika, lakini na mahospitali yote ya Unguja na Pemba, hata ya Mnazi Mmoja mifumo ya upatikanaji maji pale lazima yawe ya uhakika na ikiwezekana vichimbwe visima kila hospitali.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri vile vile narudia tena kwamba wenzetu miaka ishirini wamekosa wakombozi. Mimi natoka Wawi ninakwenda Mtambwe sasa.

Mtambwe kuna vijiji Mhe. Naibu Spika, tayari nguzo za umeme zipo, kisima tayari kipo. Tatizo bado ni umeme tu kufikishwa wananchi wale wakapata huduma zile za umeme na maji safi. Kwa mfano kuna Kijiji Mpaka Njia hadi Mtambwe Mkuu nguzo tayari zimelala zaidi ya miaka mitatu sasa, kuna vijiji vyengine vya Makoengeni, Kinazini vile vile nguzo tayari zipo lakini na kisima cha maji kipo kwenye Kijiji cha Kivumoni pale, ili wananchi wa Kokota, Makoengeni, Kinazini nao hawapati huduma hii ya maji safi.

Ningeomba kuwaombea wananchi hawa nao wasaidiwe kupelekewa umeme na maji safi ili nao wanufaike na matunda haya ya mapinduzi. Kwa sababu mara nyingi wenzetu wanachangia walizorotesha hizi huduma za kuwapelekea wananchi ili wapate kuilaumu serikali. Sisi tunasema sasa miaka hii inayoendelea wakombozi wao tumekuja. Tunataka tuhakikishe wananchi wetu wote wanafaidi matunda ya mapinduzi bila ya kubaguliwa, akiwa Mmakonde, Mnyamwezi, Mwarabu, Mhindi, popote pale habaguliwi. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuipongeza wizara na napenda kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri asilimia mia kwa mia ipite haraka ili wananchi wetu wafurahi na matunda haya ya mapinduzi. (*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mhe. Makame Said Juma.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho, lakini niombe radhi na mwili wangu bado haujaniruhusu kusimama vizuri. Kwa hivyo naomba nikae kama nilivyo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa inaeleweka hiyo. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi niingie katika wizara hii na nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inalenga kwa kila sehemu katika nchi yetu ambayo sasa hivi imekuwa ni zungumzo katika majambo. Iliyobakia sasa ni kuboresha tu katika sehemu mbali mbali, lakini niulizie tu kidogo au nilete na mimi mawazo yangu kuhusu jambo hili la ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi niende huko ardhi bado ina changamoto na inaweza kufika wakati hatutajua tunakwenda wapi, kwa sababu tunakotoka hatujui tunakwenda wapi.

Nikija miundombinu ya upangaji miji. Mhe. Naibu Spika, hii imekuwa ni changamoto kubwa sana na itakuwa ardhi yetu hatujajua kwamba ardhi yetu ni ndogo, na tunakokwenda, kwa sababu ardhi tunaigawa vibaya na tutafika wakati Waziri baada ya kuwa kugawa viwanja sasa itabidi apunguze viwanja vinavyopimwa. Kwa sababu sasa hivi kuna watu wengine wanapewa ardhi kupita kiasi. Kwa sababu mtu mmoja anaweza kupewa mita hazipungui mia moja au zaidi, ambapo kuwa mtu mmoja anatoshelezwa na mita ishirini au chini yake. Lakini mtu mmoja anapewa mita mia moja na zaidi. Mtu huyu anapanda minazi, mtu huyu anapanda miembe, mtu huyu anapanda miti ya kina aina almuradi kumkosesha mwenziwe ardhi.Itafika wakati nyumba mia moja hapa zitafika mwisho wa Pemba au mwisho wa Unguja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa ile ardhi ya mtu mmoja ambayo anapewa kiasi kilichokuwa atamkosesha mwenziwe ambaye yupo nyuma yake. Tutasahau ambao tulikuwa ni watu mia moja, lakini sasa hivi tunakwenda watu elfu moja na sote tunategemea ardhi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi ninatumai tutafika wakati mbaya kwa sababu ardhi sasa hivi tunavyoivamia zile ambazo tulikuwa tumelima, sasa hivi ndiyo sehemu ambazo zimejengwa majumba. Utafika wakati halafu tunang'ang'ana sisi kwa sisi. Hatujajua kama tunakwenda wapi lakini wenzetu wa Tanzania Bara tayari washaanza kushituka. Aliyekuwa ana shamba kubwa sasa hivi linapunguzwa ili kukidhi haja za watu ambao wanaokuja, lakini sisi wenzetu bado ardhi hii tunaitumia vibaya tutakuja juta baadae.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika Wizara hii ya Maji. Kwanza niipongeze wizara hii ambayo mimi mwenyewe nipo mbali Pemba, maana yake nipo Kojani ambacho ni kisiwa.

Wizara hii naona imefanya vizuri sana. Mimi nimebahatika katika Kisiwa changu cha Kojani visima viwili vya maji ambavyo vyote visima hivi vina nguvu zaidi. Sasa hivi usumbufu wa maji Kojani ni mdogo sana, hakuna kabisa isipokuwa tu wanadamu hakuna ambaye atatosheka kwa jambo lolote. Maana yake tukiisema kwamba serikali imefanya jambo zuri na ukawaambia watu ambao hawafahamu kama serikali imepiga hatua kwa jambo hili, basi atakwambia maji si jambo, yale maji watasema si kitu, si jambo, ukiwaambia umeme upo kwetu sasa nao pia watakwambia si kitu na wala si jambo, sijui jambo lipi ambalo kuwa kwao wanasiasa wameliweka kama ni jambo la kutumia katika nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika suala la umeme. Kwanza na mimi nishukuru wizara hii kama na mimi Kojani nimefaidika katika huduma hii, ni kisiwa kiko mbali lakini sasa kimepata umeme wa kutosha na tunaipongeza Serikali, lakini tu katika kuipongeza Serikali tunaomba Mhe. Waziri afanye utaratibu, kwa sababu mambo ya kisiwa ni kisiwa, tupate mtu ambaye anaweza kufanya kazi mule mule, ili tatizo la umeme likitokea iwe tunaweza kumtumia kwa wakati ule ule uliopo kwa sababu tulikuwa naye lakini Mwenyezi Mungu akamuhitaji kwa muda mfupi akafariki. Lakini bado wako vijana wanahitaji kufanya kazi naomba Mhe. Waziri atusaidie angalau tupate kijana mmoja au vijana wawili ili huduma zetu zikae vizuri kwa sababu tuko kisiwani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia muda wako mfupi sasa niende tu katika huduma yetu ya maji nirudi nyuma kidogo, kwa sababu mwenzangu hapa amezungumzia katika matatizo ya maji Kiuyu/Kigongoni kweli hili suala lipo. Mhe. Waziri naona ipo haja kulisimamia vizuri tu, kama kuna tatizo la mashine kama ni ndogo basi tushirikiane tuitafute mashine ilimradi tuondoe tatizo hili katika maeneo ya majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nikushukuru tena na nimshukuru Mhe. Waziri pia nitautumia muda wako kwa kukwambia tu Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwashukuru sana kwa michango yenu tangu tulipoingia hapa asubuhi na sasa hivi nitampisha Mhe. Spika, aje aendelee na nafikiri nimebakisha watu kama watatu Mhe. Said Soud, Mhe. Mohammed Aboud pamoja na mwenyewe.

(Hapa Mhe. Spika, alikalia kiti)

Mhe . Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuanza kwa kushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia nimshukuru sana na nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara hii katika kipindi kifupi alivyoweza kutekeleza wajibu wake vizuri. Kwa kweli amefanya kazi nzuri na yale maneno yanayosema kwamba kinamama wanaweza kweli kweli.

Pia nimpongeze Naibu Waziri na uongozi mzima wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wameifanya inaonekana wazi muelekeo wa kupiga hatua kubwa zaidi katika sekta hii sasa umeonekana mwanga wake mzuri sana, kwa hivyo tuwashukuru na Mungu awawezeshe kutekeleza wajibu wao vizuri.
Mhe. Spika, mimi nilikuwa na mambo matatu moja lilikuwa linahusu ahadi za Rais na utekelezaji wake hasa hasa kwenye suala zima la nyongeza za mishahara.

Tuseme ukweli kwamba kipindi cha uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa awamu yake ya kwanza na hii ya pili ameweka mkazo mkubwa kwenye maslahi ya wafanyakazi, kajenga misingi imara itakayowezesha wafanyakazi kupata haki zao lakini vile vile kutimiza wajibu wao, ameanzisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma msingi wake mkubwa ni kuweka msingi imara kwa utendaji kazi lakini na haki za msingi za wafanyakazi. Kaweka sera, sheria na miundo ya utumishi Serikalini ili iwe miongozo kwa kila mmoja kupata haki zake vizuri na kwa wakati.

Mhe. Spika, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein katika kipindi kifupi cha uongozi wake ameweza kutoa nyongeza ambayo kila mmoja ameiona katika taasisi zetu za umma, na sio tu kwa upande wa Serikali moja kwa moja lakini pia Kamisheni imetoa miongozo kwa mashirika na taasisi zinazojitegemea kuhusu nyongeza za mishahara kupitia bodi zao, kwa hivyo hapana shaka yoyote pale ambapo bodi ya ushirika husika imeshindwa kutekeleza wajibu pengine kwa mazingira tofauti yaliyo juu ya uwezo wao ni wajibu wa ushirika husika au taasisi inayojitegemea kurudisha lalamiko hilo Serikalini kuona uwezekano wa utekelezaji wake.

Kwa hivyo kimsingi serikali imetoa nafasi kubwa kwa ajili ya utekelezaji wake katika sekta mbali mbali ili wananchi ama wafanyakazi waweze kupata haki hii ya nyongeza.

Sote ni mashahidi hivi karibuni tu Rais alielekeza suala zima la kupandisha kima cha chini kutoka laki moja na nusu hadi laki tatu, na *in shaa Allah* mwakani mwezi wa nne utekelezaji utaanza rasmi.

Mhe. Spika, serikali tayari imeshatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuorodhesha ahadi zozote zile ambazo hazijatekelezwa katika Mikoa na Wilaya zao ili hatua ziweze kuchukuliwa, hivyo hivyo kwa taasisi na mashirika ya umma na taasisi zinazojitegemea. Kwa hivyo kwa ufupi nia ya Serikali ni kutekeleza ahadi zake kila inapohitajika kufanyika hivyo, na nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba hiyo ndio nia na madhumuni ya Serikali kuona ahadi zinatekelezwa vizuri kwa maslahi ya watumishi.

Mhe. Spika, pia ilitokea hoja ya uuzaji wa nyumba ya Mazizini ya Shirika la Umeme na ikasemekana kwamba utaratibu haukufuatwa, lakini kwa ufupi Mhe. Spika, utaratibu wa kiserikali kuna njia mbili, uko utaratibu ule wa kuuza kwa mnada, lakini upo utaratibu wa maombi, na maombi yale yanapopelekwa Serikalini yanazingatiwa na baadae tathmini inafanyika kwa nyumba husika, na baada ya kwisha kutafakariwa na Serikali ikaona basi maombi hayo yakubaliwe na kuchukuliwa hatua kwa muhusika kuuziwa nyumba hii. Kwa hivyo, hicho ndicho kilichotokea, nyumba ya Mazizini imeuzwa kwa kufuata utaratibu, na naamini kabisa kwamba imefanya vile kwa maslahi yetu sote ili kuhakikisha na viongozi wetu wanapoomba nyumba hizi waweze kukaa, basi wanapatiwa kwa ajili ya kazi nzuri waliyoifanya katika kulitumikia taifa letu. Kwa hivyo, kwa ufupi utaratibu pale umefuatwa na nyumba iliuzwa kwa baraka za Serikali ili iweze kutumika kwa huyo aliyeuziwa.

Kwa upande wa Fungu Mbaraka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hapa ametoa maelezo mazuri sana kuhusu suala la Fungu Mbaraka, lakini mimi niseme tu Mhe. Spika, kwamba serikali zetu mbili ziliwaagiza Wanasheria Wakuu wa pande mbili kutafakari kwa kina juu ya masuala haya kwa upana wake hususan kwenye sekta hii ya mafuta.

Kwenye suala la Fungu Mbaraka hakukuwa na utata wakati wa mazungumzo haya jambo hili limekwenda vizuri na hakuna *dispute* ya aina yoyote, Fungu Mbaraka ni sehemu ya Zanzibar, kwa hivyo hakuna mjadala wowote. Na haina haja kila mara kurudia rudia, jambo hili limeelezwa kwa kina sana katika vikao mbali mbali.

Kwa hivyo nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba ile ni sehemu yetu, na taratibu zinafuatwa kutokana na sheria kama Mhe. Waziri wa Kilimo alivyoeleza hapa, karibuni tutaisoma kwa mara ya kwanza katika Baraza letu hili tukufu la Wawakilishi na baada ya hapo basi taratibu nyengine zitaendelea na tutakuja kupitisha sheria yetu kwa pamoja, na ndio itakayotoa muongozo wa namna gani ya kutafutwa mafuta na namna gani mafuta

watapewa hawa watakaokuja kujitokeza katika suala zima la kusaidiana katika uchimbaji wa mafuta.

Kwa hivyo, suala hili lisiturudishe kila mara tukadhani kuna utata, hakuna tena utata wowote, suala la Fungu Mbaraka ni sehemu ya Zanzibar na hakuna yeyote aliyesema ni sehemu ya Bara.

Mimi nafikiri hoja hii Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe waielewe, sasa la msingi tushirikiane tujenge nchi yetu kwa manufaa yetu na vizazi vinavyokuja. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja ya Wizara hii na nawaomba Wajumbe wenzangu muipitishe vizuri, kwa sababu ni Wizara muhimu yenye maslahi ya watu wetu, na kwa sababu wameonesha mfano mzuri wa utendaji kazi, hapana shaka yoyote *mcheza kwao hutunzwa*.

Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, na kabla ya yote kwanza namuomba Mwenyezi Mungu amrehemu hayati mzee Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar kwa uamuzi wake alioufanya baada ya Mapinduzi ya 1964, kutangaza rasmi kwamba maji bure.

Hoja hii ya maji bure ilikuja kwa maana Wazanzibari walikuwa wakipata tabu sana kwa maji, walikuwa wanakunywa maji sawa sawa na vyura, maji ya mitoni, visima vya kata, visima vidogo vidogo, shida ilikuwa kubwa. Wanyonge wa nchi hii walikuwa hawapati maji safi na salama, jambo hili *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake.

Mhe. Sika, ukweli usiofichika ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka awamu yake hadi awamu ya leo imefanikiwa kuleta maji bure na maji safi na salama.

Nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Seif Ali Iddi na uongozi mzima wa Serikali kwa kuhakikisha kwamba hoja hii ya maji bure inaendelezwa.

Mhe. Spika, hoja ya maji vijijini, hoja ya maji mijini kwa kweli imefikiwa asilimia 80, na kwa sasa Wazanzibari wanapata maji safi na salama, na hoja hii ni hoja ya kupigiwa mfano, kwani kuna nchi mbali mbali zimeshindwa

kuwapelekea wananchi maji safi na salama, lakini Zanzibar imefanikiwa mara moja kuwathibitishia wananchi wake wanapata maji safi na salama.

Jambo la kufurahisha pamoja na hali ngumu ya maisha, hali ngumu ya kiuchumi, lakini bado watu wanaendelea kupata maji bure kwa sababu huo mchango unaotolewa haujakuwa malipo ya maji, kwa hivyo ni vizuri wananchi wa Zanzibar wakaamini kwamba wanapata maji bure.

Malipo yanayotolewa ya kulipia maji ni pale maji yanapotokea bahati mbaya mfereji wako umekatika, paipu imetoboka, ni kama ada tu na kufundishwa taratibu za kutumia maji ili yasichafuke.

Mhe. Spika, nchi yetu imefanikiwa kuwa na maji kila pembe ya Unguja na Pemba, na kila yanapotafutwa maji yanapatikana, kwa hivyo ongezeko la watu ndio linalochangia maji kuwa kidogo kwa baadhi ya mwahala, lakini jitihada ya Serikali ni kuhakikisha kila mtu anapata maji safi na salama.

Ndani ya uongozi wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tumeshuhudia sote kwamba amefungua visima vingi ameweza kuonesha kufungua miradi mingi ya maji, ameweza kuleta kampuni mbali mbali mpaka kutoka Iran kwa ajili ya kutengeneza njia za maji wananchi waondokane na dhiki ya maji, hili suala la kwamba pale hapana maji pale pana maji basi lina mwisho wake. Zanzibar itafikia hatua ya kwamba kila pahala yatapatikana maji.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Wazanzibari kwamba Wizara ya Maji, Nishati iko njiani kuhakikisha kuwa kila pembe ya Zanzibar maji yanapatikana chini ya Waziri mzalendo na Naibu Waziri mzalendo, watu ambao kwa sasa hawana nafasi hata ya kupumzika.

Sisi sote ni mashuhuda kwamba hawatulii saa zote wako nje kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. Kwa hivyo mimi nawaomba Wawakilishi wote tupitishe bajeti hii, ili tuhakikishe kwamba mwenzetu huyu anakwenda kufanya kazi ya Wazanzibari bila ya kujali itikadi ya vyama vyao, bila ya kujali itikadi ya dini zao, bila ya kujali vijiji vyao. Kwa maana hiyo nahakikisha kwamba serikali yetu iko njiani kuhakikisha kuwa kila kitu kinafanikiwa.

Mhe. Spika, suala la umeme kwa Zanzibar ilikuwa ni kitu cha ajabu. Waliokuwa wakipata umeme walikuwa watu maalumu, umeme ulikuwa unakwenda kwa watu maalumu lakini leo Serikali imefanikiwa kupeleka umeme kila pembe ya Zanzibar, umeme umeweza kwenda sasa hivi kama biashara ya kawaida watu wamepewa fursa mpaka ya kukopa umeme.

Ule umeme wanaukopa, mtu anautumia halafu anakwenda kuulipa tena anaukopa umeme kwa zaidi ya laki tano au milioni lakini atatiliwa nyumbani kwake anakwenda kutumia na halafu analipa kidogo kidogo mpaka anamaliza, huo ni msaada mkubwa wa Serikali, huu ni msaada mkubwa wa uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, tunaamini kwamba haya yote yanafanyika kwa imani aliyonayo, kwa busara alizonazo, kwa vile nina hakika kwamba tatizo la umeme nalo litaondoka katika visiwa vyetu na kila mtu atafanikiwa, na hoja hii chini ya uongozi wa mawaziri tulionao hawa.

Mhe. Spika, pia ningependa kuchukua nafasi hii kuwaambia Wawakilishi kwamba hoja ya mafuta na gesi italetwa, ni wajibu wetu kusema kwamba itakapoletwa tutapewa taaluma, na taaluma hiyo pia itapelekwa kwa wananchi, na wananchi wote watapewa taaluma ya hoja hiyo.

Kwa nini basi, kwa sababu nchi yetu inapiga hatua siku hadi siku chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa hivyo suala hili ni suala ambalo tunaamini wazi itakuwa ni sehemu moja ya Wazanzibari kuondokana na shida na umasikini mkubwa ambao umetukumba.

Kwa hivyo, sisi kama Wawakilishi ni wajibu wetu kutumia nafasi hii kukubali bajeti hii ipite bila ya kupiga mabuti yaliyo mengi, kwa maana ya kumuwezesha Waziri afanikishe, akili yake itulie na ayapange yale yote aliyokusudia ndani ya uongozi huu wa Dkt. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wawakilishi nyinyi ni mashuhuda wa kuwa watu wanapenda kuturudisha nyuma, wanahakikisha kwamba eti Serikali isipige hatua, na wengine wanathubutu kusema kwamba eti muda mfupi tu tutaondoka kwenye madaraka.

Nathibitisha kwamba hawa ni maadui, ni mahasidi, na wapo tayari kuona nchi hii inapata matatizo kwa vile ninachotaka kuwaambia mshikamano wetu ndio ushindi, umoja wetu ndio ushindi, na nguvu zetu ni kumuwezesha Rais afanikishe kila alilokusudia kwa maslahi ya Wazanzibari, kwa vile hayo mabuti, mateke hebu leo tuyapunguze tupitishe hii hoja mara moja.(*Makofi*)
Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, Ardhi na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na kutoa baadhi ya ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa na Wajumbe.

Mhe. Spika, kwanza nianze kuwashukuru Wajumbe wote kwa kutoa michango waliyonayo kwa uwazi, ikiwa imelenga katika kujenga. Kwa ujumla niseme kwamba tumepokea na yale yote ambayo yanataka ufuatiliaji basi tunaahidi kwamba tutayafuatilia, na yale ambayo yanaweza kukamilika ndani ya kipindi kifupi tunaahidi kuyakamilisha.

Mhe. Spika, napenda wafahamu wajumbe kwamba Wizara yetu ni Wizara ya mahitaji sana kama ilivyo, ni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.Wakati tunaingia tumeona suala la kwanza la kipaumbele hasa ni suala la maji, na wakati najibu baadhi ya maswali niliwahi kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi wa Konde na nikamuahidi kwamba ndani ya kipindi kifupi tutalitatua tatizo, na hatua tuliyofikia sasa ni hatua ya kulikamilisha tatizo lile pale pale.

Pia naomba nimuahidi Mhe. Viwe Khamis Abdalla kilio chake tumekisikia na kama alivyosema na yeye ni shahidi kwamba siku ya pili tu pampu imefungwa, hii ni kwamba Serikali hii sikivu na bado tunasema kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba matatizo tunayatatua kwa kadri Mungu anavyotuwezesha. Wakati mwengine lakini wanapaswa Wajumbe wafahamu kwamba inawezekana hali, kwa sababu nia na hali ni vitu viwili tofauti, sasa tunayo nia na wengine walitu- *quote* vibaya pia kwamba hatuogopi gharama, ni kweli lakini pale ambapo hali inaruhusu. Sasa ukiangalia bajeti ya mwaka uliokuwa unaishia sasa utagundua kwamba Wizara hii ilipatiwa asilimia 25.5 jambo ambalo halikuweza kufanikisha yale yaliyokusudiwa…

Mhe. Spika: Mheshimiwa husikiki vizuri baadhi ya Waheshimiwa wanalalamika kwamba hawasikii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, Ardhi na Mazingira: Mhe. Spika, hata hivyo.

Mhe. Spika: Njoo mbele huku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, Ardhi na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Wizara yetu lakini pia kutoa baadhi ya ufafanuzi kwa maeneo machache yaliyoguswa na Wajumbe, lakini kabla ya hapo niwashukuru Wajumbe wote kwa ujumla wao.

Mhe. Spika: Mheshimiwa endelea usianze upya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, Ardhi na Mazingira: Kwa kuchangia kwa uwazi, lakini wafahamu kwamba baadhi ya mambo yanakamilishwa kutokana na hali ya uwezo ulivyo, sasa jitihada zetu zimeanza kuonekana, kwa mfano nilivyokuwa nimetangulia kusema kwamba jimbo la Konde tumetatua kwa kiasi kikubwa na asilimia chache imebakia na maeneo mengine hivyo hivyo, na tumeanza na maji zaidi kwa sababu ni huduma ambayo tunafahamu kila kitu kimeumbwa kwa maji na kinategemea maji.

Sasa niwaombe kwa ujumla kwamba tuwe na matumaini na Wizara hii na ufafanuzi zaidi kwa ujumla tukachukua maelezo yote, maswali yote lakini Mhe. Waziri atakapokuja atafafanua yale ambayo labda hatujamgusa mtu tayari atukumbushe, lakini kwa ujumla wetu tumeyachukua na tutayafanyia kazi, baada ya hayo Mhe. Spika, naomba nikushukuru ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, Ardhi na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe majumuisho ya Wizara yangu ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira leo tarehe 16/6/2016.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira napenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara moja kwa moja au kwa maandishi.

Jumla ya Wajumbe 23 waliochangia moja kwa moja na wajumbe 24 waliochangia kwa maandishi, kwa hivyo wote kufanya 47. Wizara yangu ni Wizara kubwa, wizara inayomgusa kila mtu. Kwa hivyo usishangae kuona kwamba wachangiaji ni wengi sana.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati kwa ushauri na maelekezo aliyotupa pamoja na Wajumbe wake wote, pamoja na Wajumbe wote wa Baraza hili, tunaahidi michango yao itaimarishwa utekelezaji na ufanisi katika majukumu yetu ya Wizara na kufikia lengo la kuwapatia huduma bora wananchi wa Zanzibar.

Aidha napenda kuwashukuru wale wote waliotupa ushauri binafsi na maelekezo katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ushauri wao tunaupokea na tutaufanyia kazi. Natumia fursa hii kuwapongeza sana sana Wajumbe wa Baraza hili kwa miongozo yao na hoja zao pamoja na pongezi nyingi walizozitoa kwa Wizara yangu tumezipokea, na tunaomba watuamini.

Mhe. Spika, kwa kuwa maswali mengi yamejirejea naomba radhi sitojibu mtu mmoja mmoja, majibu mengine nitayajibu kwa ujumla wake na hasa ukizingatia kwamba tumemaliza maswali na inabidi nijibu.

Mhe. Spika, Wajumbe waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kwa umuhimu wake na mazingatio napenda kuwataja kama ifuatavyo:

Waliochangia moja kwa moja:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf
5. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
6. Mhe. Simai Mohamed Said
7. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
8. Mhe. Asha Abdalla Mussa
9. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
10. Mhe. Omar Seif Abeid
11. Mhe. Nassor Salim Ali
12. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
13. Mhe. Shaibu Said Ali
14. Mhe. Suleiman Sarahan Said
15. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
16. Mhe. Said Omar Said
17. Mhe. Shamata Shaame Khamis
18. Mhe. Ali Suleiman Ali
19. Mhe. Hamad Rashid Mohammed
20. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
21. Mhe. Makame Said Juma
22. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed; na
23. Mhe. Said Soud Said

Vile vile wapo waliochangia kwa maandishi kama nilivyosema wapo 24 naomba pia niwatambue:

1. Mhe. Abdalla Ali Kombo
2. Mhe. Saada Ramadhani Mwenda
3. Mhe. Hidaya Ali Makame
4. Mhe. Mtumwa Peya
5. Mhe. Choum Khamis Kombo
6. Mhe. Tatu Mohammed Ussi

7. Mhe. Ussi Yahya Haji
8. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
9. Mhe. Harous Said Suleiman
10. Mhe. Juma Ali Khatib
11. Mhe. Miraji Khamis Mussa
12. Mhe. Asha Abdalla Mussa
13. Mhe. Mussa Ali Mussa
14. Mhe. Shehe Hamad Mattar
15. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
18. Mhe. Ali Khamis Bakari
19. Mhe. Moudline Cyrus Castico
20. Mhe. Said Mohammed Said
21. Mhe. Mussa Foum Mussa
22. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
23. Mhe. Maryam Thani Juma; na
24. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo kwa uwezo wa *Allah* naomba nijibu maswali yaliyoulizwa kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha.

Mhe. Spika, naomba katika kujibu maswali yangu naomba niyajibu kwa sekta, nitaanza na sekta ya ardhi, na kwa sababu nilisema mwanzo kwa sababu ya muda nimemaliza maswali na natakiwa nijibu, kwa hivyo naomba nianze kwa sekta kwa sababu niliyaweka kwa sekta.

Naomba nianze na Mhe. Hamza katika uwasilishaji wake wa Kamati ya Mawasiliano kama Mwenyekiti, lakini na yale yake mwenyewe binafsi basi nitaendelea kuyajibu.

Kwanza yeye aliuliza kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na matumizi bora ya ardhi na mipango mipya ya matumizi ya ardhi. Kusema kweli Serikali kwa kupitia Kamisheni ya Ardhi na Bodi ya Uhaulishaji itaendelea na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusiana na matumizi bora ya ardhi kwa kupitia Televisheni, Redio, Makongamano pamoja na Warsha mbali mbali kwa kupitia kila ngazi, ushauri huu umechukuliwa na utazidi kufanyiwa kazi.

Vile vile Mhe. Hamza aliuliza wawekezaji kuchukua ardhi kwa wananchi bila ya kulipia fidia. Serikali imejidhatiti kuhakikisha muwekezaji yeyote anayetaka

kuwekeza hapa Zanzibar kabla ya kukabidhiwa ardhi hiyo awe amelipa fidia kwa waliokuwa wakitumia ardhi hiyo. Hata hivyo suala la ulipaji fidia kwa ardhi ya Serikali mwananchi atalipwa kwa kile anachokiendeleza katika ardhi hiyo, na hilo tutaliangalia sana, pamoja na kwamba ardhi ni mali ya Serikali, lakini kile kilichopo basi watathmini watatathmini na hatimaye mwananchi yule atalipwa.

Hoja nyengine aliyoizungumzia ni kwamba wananchi hawajalipwa fidia Matemwe kwa sababu kuna malalamiko mengi kama alivyowasilisha katika taarifa, kwa hivyo hili alilitoa kama mchango wake binafsi.

Wizara inafahamu vyema kadhia ya wananchi wa Matemwe na muwekezaji wa mradi mkubwa unaoendelea huko, mradi wa *Pennyroyal,* kwa misingi ile ile kuhakikisha kwamba haki inatendeka, Wizara tayari inalishughulikia suala hili kwa nguvu zote.

Binafsi uongozi wa Wizara na Kamisheni ya Ardhi ushafika katika eneo linalolalamikiwa na kufanya mazungumzo na pande zote mbili zinazohusika ili kupata ufumbuzi wa suala hilo. La msingi katika hilo ni wananchi kuwa na imani na Serikali yao wakati wakishughulikia suala hili, na kutoa ushirikiano wao kila inapohitajika.

Serikali itahakikisha uwekezaji huo hautoathiri wananchi wa eneo hilo kwa hali yoyote ile, na pia una tija kwao na kwa vizazi vijavyo, na hayo ndiyo madhumuni ya kuanzisha uwekezaji hapa Zanzibar, na sio kuwanufaisha wachache tu na kuwaacha wazawa ambao wako katika maeneo yale.

Mhe. Spika, naomba niliseme hili hasa kwa hii *issue* ya Kaskazini Unguja, Matemwe, tunaendelea kulifanyia kazi na tunalishughulikia. Mimi mwenyewe binafsi nimeshakwenda, lakini na watendaji wangu wameshakwenda, hata baadhi ya mawaziri wameshakwenda na tutaendelea kwenda kuhakikisha mgogoro ule uliopo tutautatua. Lakini naomba niseme kwamba eneo linalolalamikiwa bado ofisi yangu haijatoa ruhusaa wala haijatoa hati ya kuendeleza eneo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje pia alitoa hoja Kamisheni ya Ardhi aliizungumzia kwamba imekaa bila ya sheria, jibu ni kwamba Mhe. Jaku utakumbuka kwamba Baraza hili tukufu ndio lilotunga na kuipitisha Sheria ya Kamisheni ya Ardhi namba 6 ya mwaka 2015, hivyo inaonesha wazi kuwa Kamisheni ya Ardhi ipo kisheria aidha taratibu za

kuitangaza kuanza kutumika kwake kwa sheria hiyo ilitangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali toleo la CXX 1V No.6574 la tarehe 24/7/2015.

Ama kuhusu shutuma za kukawia katika suala zima la utoaji huduma zake na kupelekea usumbufu kwa wananchi. Hapa ningewaomba sana Wajumbe wa Baraza lako hili na wananchi kwa ujumla kutafakari kwa kina madhumuni ya kuundwa kwa chombo hicho cha Utawala na Usimamizi wa Ardhi, ambayo ni kuondosha migogoro ya ardhi na matumizi ya ardhi iliyokuwa ikiongezeka kwa kasi kiasi cha kutishia usalama wa umiliki na matumzi ya ardhi, jambo ambalo linatatiza na kuviza maendeleo ya jamii na uchumi kwa ujumla.

Kamisheni hivi sasa inafanya kazi kwa umakini sana kwa kufuata miongozo ya Sheria na kanuni katika kuhakikisha umiliki, matumizi na uhaulishaji salama wa haki ya matumizi ya ardhi, ili kumlinda mwananchi kuingia au kuingizwa matatizoni, na wasiopenda maendeleo baada ya kupatiwa huduma za masuala ya ardhi na Kamisheni. Kwa misingi hiyo kinachotokea hivi sasa Kamisheni sio kuwapa watu usumbufu bali kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za utawala na usimamizi wa ardhi, kwa nia safi ya umiliki na utumiaji salama wa ardhi, na hii ndio maana halisi ya kuacha kufanya kazi kwa mazoea kunakohimizwa na Serikali kwa hivi sasa.

Na hili labda tukilizungumza tunasema hatuwezi kuja mtu kaleta ombi unamjibu hapo hapo bila ya kufanya utafiti, na ndio maana tukasema kwamba Kamisheni ipo kisheria lakini inafanya kazi zake kwa umakini zaidi, ili kuhakikisha inaondoa migogoro ambayo sisi tumeirithi.

Nini kazi za Bodi ya Uhalishaji? Nina imani kuwa Mhe. Jaku anazielewa vyema sheria za nchi hii ambazo huundwa na Baraza hili tukufu na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni mazuri tu ya kuimarisha utawala bora hapa nchini, kwa kuchelea kuchukua muda mrefu kulielezea hili ningemuomba kupitia vyema sheria Na. 8 ya mwaka 1964 na kufanyiwa marekebisho na sheria Na. 10 ya mwaka 2007 na kuanzishwa kwa Bodi ya Uhaulishaji Ardhi, ambapo imeelezwa kwa uwazi shughuli za kazi za Bodi, nguvu na mamlaka yake pamoja na taratibu za uhaulishaji wa kisheria.

Kazi kuu ya uhaulishaji ni kusimamia na kuidhinisha masuala ya uhaulishaji ardhi hapa nchini kwa kufuata misingi ya sheria na matumizi bora ya ardhi.

Hoja nyengine ilikuja nani ana sifa ya kuhaulisha au kuhaulishiwa. Mwenye sifa ya kuhaulisha au kuhaulishiwa ni mtu, taasisi, Jumuiya au Kampuni, hoja awe amefuata misingi ya sheria ya utoaji na upewaji wa ardhi hiyo.

Aidha Bodi pia ina kazi ya kulinda maslahi ya muhaulishaji na muhaulishwaji, kinachohaulishwa na kulinda haki na maslahi ya mtu wa tatu kwa mfano taasisi, jamii au familia.

Hoja nyengine ilikuja mtu mmoja kuwa na nafasi zaidi ya moja katika utendaji kazi. Hakuna mtu mwenye nafasi zaidi ya moja katika chombo kimoja, inawezekana mtendaji kuwa na nafasi yake ya kazi na Serikali ikampangia majukumu mengine, kwa mfano kuwa Mjumbe katika bodi fulani au kamati hii inafanyika kwa kuleta ufanisi katika chombo chenyewe kutokana na umuhimu wa kupatikana kwa mtaalamu huyo. Pia inatokezea mtendaji atakuwa katika afisi na akaingia katika kamati nyengine na ile nafasi yake ya *ex officio*.

Jengine lilikuja suala kuzuia ujenzi wa msikiti wa Mombasa na utoaji wa vibali vya ujenzi. Suala la ujenzi ni suala nyeti ambalo linahitaji kusimamiwa, matumizi bora ya ardhi hasa ukiangalia hii eka tatu, ndio maana sasa hivi imeundwa ile kamati ya *UDC* hili suala la msingi la kuweka katika sekta ya ardhi upatikanaji na wajumbe.

Kama tujuavyo msikiti ni sehemu nyeti, sisi hatuwezi kuuzuia lakini pahala ambapo pana misikiti mingi na wakati mwengine matumizi ya ardhi unaona kwamba hapana usalama au kuna kitu ambacho wataalamu wamekiona kwamba hapa wazuie basi wataendelea kuzuia, na kwa sababu kuna misikiti mingine mbele yake na inatosha kwa maslahi au ipo misikiti mingi, kwa hivyo tungeshauri kwamba iweze kupelekwa sehemu nyengine ili na watu wengine waweze kupata huduma hiyo ya imani zaidi.

Lakini pia upatikanaji wa wajumbe wa Kamati hii umezingatia sana ushirikisho wa taasisi na wadau ambao huingia katika kamati hiyo kwa nafasi zao. Pia kuundwa kwa UDC ni matakwa ya sheria ya mipango miji na vijiji ya mwaka 1955.

Lakini pia Mhe. Nadir Mwakilishi wa Jimbo la Chaani alitoa hoja ya ufutaji wa *lease* kwa wawekezaji na wanaolipia kodi ya ardhi.

Ni kweli kuna baadhi ya wawekezaji miradi yao imefutwa kwa sababu ya kuzitelekeza Ardhi au kushindwa kutekeleza masharti ya mikataba ya ukodishaji wa Ardhi hizo, jambo ambalo limesababisha kukosekana kwa manufaa kwa taifa. Ulipaji wa kodi huwa ni ujanja unaotumiwa na wawekezaji hao kuonekana kama wapo lakini wanakuwa wamehodhi tu ardhi hizo bila ya kutekeleza malengo ya upewaji ardhi hizo. Hivyo, Serikali kuzirudisha ardhi

hizo ni jambo la msingi ili kupewa wawekezaji wenye malengo ya kweli ya kuziendeleza Ardhi hizo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa naomba tusikilizane, endeleeni kumsikiliza Mheshimiwa, kwa sababu hamumsikilizi halafu mtakuja kusema sikujibiwa hoja yangu, naomba mumsikilize.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Halafu chengine alishauri kwamba kuwepo na ardhi tupu kwa ajili ya wawekezaji kwa kushirikiana na ZIPA. Naomba tuupokee ushauri huu ni mzuri tunauuchukuwa na tutaufanyia kazi. Hata hivyo, Serikali tayari imetangaza kwa muda mrefu maeneo ya uwekezaji ambayo yanasimamiwa na ZIPA (EPZ).

Mhe. Nadir aliuliza pia watu wangapi wana hati na wangapi hawana hati, kusema kweli ni lengo la serikali kuwapatia wananchi hati za matumizi ya ardhi kwa kupitia zoezi la utambuzi wa ardhi kwa Zanzibar nzima. Tayari limeshaanza kwa Unguja na Pemba katika maeneo ya mjini na vijijini kuweza kutambua takwimu hizo hadi hapo serikali itakapomaliza zoezi la utambuzi wa ardhi ambalo ni zoezi lenye gharama kubwa.

Zoezi hili linafanywa kwa ufadhili wa mradi wa MKURABITA na uliokuwa mradi wa SMALL ambao umemaliza muda wake kwa sasa. Serikali kwa sasa iko mbioni kutafuta njia mbadala ya kuendeleza zoezi hilo kama nilivyotoa katika hotuba yangu. Lakini vile vile alisema lease ngapi zimefutwa kiholela, hakuna *lease* iliyofutwa kiholela naomba nikuhakikishie Mwakilishi wa Jimbo la Chaani ufutwaji wa *lease* zote unahakikishwa unafutwa kutokana na utaratibu na sheria zilizowekwa na kwa yoyote anayeona kuwa ufutaji wake haukufata utaratibu basi anaweza kufika Ofisini kwetu kulalamika na tutamsikiliza na sisi huwa tunahudumia wajumbe wetu ipasavyo katika ofisi ile.

Kuhusu muekezaji aliyechukua ardhi yake huko Makangale Pemba, Mhe. Nadir aliuliza swali hili, swali lilifanyiwa kazi kwa pamoja kati ya Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi iliyopita na taasisi za ardhi. Eneo ambalo lilipendekezwa la Michamvi halikuwa sahihi kwa kuwa lilikuwa na umiliki wa mtu mwengine, swali hili tunalichukua na kulifanyia kazi.

Pia, naomba nimfahamishe Mhe. Nadir Abdul-latif wa Chaani kwamba mikataba iliyofutwa mpaka mwaka 2015/16 ilikuwa ni mikataba 9 naomba niitaje. *Zanzibar Investment*, uliopo Tazari, *Index Group* uliokuwepo Matemwe, Muyuni, *Ifa Hotel* Tazari, *Mpapindi Holiday* Makangale,

Vumawimbi Eco Luxury Makangale, *Hotel Mashallah* Kiwengwa, *Kalela Beach Resort* Michamvi, *The Address* Tazari na *Zanzisun Hotel* Kiwengwa.

Lakini mikataba 10 ilifutwa mwaka 2014/15 ni *Neptune Hotel* Dongwe, *Zanzibar Resort & Hotel Limited* Michamvi, *Landmark Hotel* Kiwengwa, *TB Investment* Pongwe, *Cristal Resort (Only Portion)* Paje, *Opulent Zanzibar* Pongwe, kuna *Bumweni Sea View* Bumbwini, *Zanzibar Masai Resort* Kiwengwa, *Bwejuu Beach Resort* Bwejuu na *Reliance Resort* Michamvi.

Mwaka 2013/14 jumla ya mikataba 6 ilifutwa, *Rhonit* Mangapwani, *Richard Antony* Mangapwani, *Sago Palm* Kizimkazi, *Soverein and Sand* Kizimkazi, Elewana Afrika Kiweni Pemba. Hiyo ni idadi ya Mikataba ambayo imefutwa kuanzia 2013.

Niende kwa maswali ambayo yalianza asubuhi ya leo, Mhe. Simai alisema lini wizara itatoa ramani mpya ya visiwa vyetu ukizingatia kujazwa kwa maeneo ya fukwe. Kwa sasa wizara inatayarisha ramani kadri ya mabadiliko yanavyojitokeza na kuweka kumbukumbu za ramani mpya kwa maeneo husika. Ama kuhusu ramani mpya za visiwa hutolewa kila baada ya miaka 10 au zaidi na mara zote husaidiwa na wafadhili kwani kazi hii ina gharama kubwa na inahitaji iende na mabadiliko ya teknolojia. Mfano ramani za mwaka 1977 waingereza walifadhili hilo na ramani ya mwaka 2004 wafindland walifadhili hilo.

Vile vile, Mhe. Simai aliendelea akauliza swali la ujazaji wa eneo la bahari katika eneo la mradi wa Mtoni Marine. Mtoni je, haitopelekea kubadilisha ramani ya Zanzibar.

Ujazaji wa eneo la bahari unalenga kuongeza eneo la ardhi, hivyo utaathiri ramani ya eneo hilo kutokana na mabadiliko ya ukubwa wa eneo la ardhi. Wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi ina kitengo maalum cha ramani ambacho kina jukumu la kutayarisha na kurekebisha ramani za nchi kila inapohitajika. Hivyo suala hilo litafanyiwa kazi na kitengo hicho itakapofika muda wake.

Mhe. Omar Mwakilishi wa Konde alikuwa anazungumzia suala la Makangale.

Tokea mwaka 1994 eneo la Makangale lilitengwa kwa ajili ya uwekezaji wa Hoteli, maeneo mengi yalipimwa lakini hadi leo ni maeneo sita tu yaliyoendelezwa kwa uwekezaji wa hoteli mengine yamezuiliwa kwa kupigwa makuta na kupelekea kuwazuia wananchi kushindwa kuyatumia maeneo yao. Aliniomba mimi kama Mhe. Waziri niweze kuyafatilia. Ninamshukuru sana

Mhe. Omar kwa ushauri wake huo kwa eneo la Makangale nimelipokea na nitaendelea kulifanyia kazi. Hata hivyo Wizara tayari imeshaanza kuchukua hatua kwani mwaka 2015/16 wawekezaji wawili *Mpapindi Holiday* na Vumawimbi *Eco Luxury* ambao hawajaendeleza tayari wameshafutiwa hati hizo.

Kulikuwa na kuna swali la Mhe. Simai nililiruka kuhusiana na upimaji wa viwanja Tunguu. Kwa nini wananchi wa eno hilo hawapatiwi viwanja.

Mhe. Spika, upangaji, upimaji na utoaji wa viwanja ni kwa ajili ya wananchi wote wa Zanzibar na haki ya kila mwananchi wa visiwa hivi kupata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya kuishi. Hivyo kama ilivyo wa wananchi wengine wananchi wa Tunguu wana haki ya kupatiwa viwanja hivyo. Kinachohitajika ni kufata uatratibu wa kuomba viwanja hivyo na maombi yao yatapokelewa na kufanyiwa kazi. Ila tunaomba wawe wastahamilivu katika wakati huu ambao serikali baada ya kubaini kuwa ardhi sasa imekuwa ndogo kuweza kukidhia mahitaji ya kila mwananchi sehemu ya kujenga makaazi binafsi. Serikali inajipanga kuanzisha mpango wa kuhakikisha kila mwananchi anapata nyumba ya makaazi badala ya kupewa ardhi. Ndio ule mradi ambao tumeuanza sasa hivi na tunautangaza wa ng'ambo tuitakayo na maeneo mengine pia tutakwenda.

Mhe. Simai nimeshamjibu swali hili kwamba utaratibu ufuate kwa sababu wananchi wafate utaratibu wa kuweza kuomba.

Vile vile, Mhe. Hidaya Ali Makame Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake alisema kuna watu wanajimilikisha ardhi bila ya kuwa na hati wala urithi wa ardhi hizo lakini wanahodhi mashamba zaidi ya matatu na hakuna sheria inayowabana.

Mhe. Hidaya kuna mashamba ambayo ni Serikali ila kuna watu wanajimilikisha na kuyafanya ni ya kwao, jee Serikali inayafahamu hayo na inachukua hatua gani.

Mhe. Spika naomba kumjibu hoja zote mbili alizozitoa kwa pamoja. Sheria ya umiliki wa ardhi ya mwaka 1992 imeweka wazi kuwa mwananchi anaweza kupewa ardhi na Serikali viwanja viwili tu kwa ajili ya makaazi na eneo moja la shamba kwa ajili ya kuliendeleza kwa kilimo.

Pia, Serikali inayafahamu masuala hayo na kwa kupitia zoezi la utambuzi wa ardhi linaloendelea inaweza kugundua watu hao wanaohodhi ardhi hizo na

utaratibu wa kuzirudisha ardhi hizo serikalini utafuata. Nimuombe Mhe. Hidaya kama yeye anawatambua naomba tushirikiane serikali ni yetu, serikali ni ya Chama cha Mapinduzi, tushirikiane basi uje Ofisini na utuletee ili tuweze kufanya kazi hii kwa pamoja.

Mhe. Saada Ramadhan Mwenda na Mhe. Shaib Said Ali waliuliza swali ni lini elimu ya usajili itatolewa kwa wananchi wa shehia zilizobaki, ili wananchi wafaidike na huduma hiyo.

Elimu ya usajili wa ardhi imeshatolewa nchi nzima kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na njia ya radio, televisheni, maonesho ya hadhara, majarida na vipeperushi na pamoja na kuwaelimisha wanafunzi wa skuli mbalimbali. Mbali ya elimu hiyo iliyokwisha tolewa, elimu ya ziada itatolewa kwa wananchi pale shehia husika itakapokuwa tayari kwa zoezi hilo la utambuzi na usajili.

Pia, naomba nimjibu Mhe. Asha Abdalla Mwakilishi wa Kiwengwa viwanja katika eneo la Gube wananchi wanalalamikia kuhusu ahadi waliopewa na kugaiwa viwanja katika eneo hilo. Eneo la Gube ni eneo la kilimo, hivyo hatuna budi kulilinda lakini ni kweli kuwa kuna baadhi ya wananchi tayari wameshajenga katika eneo hili, wizara yangu italifanyia kazi suala hili kuhakikisha kuwa eneo la kilimo linahifadhiwa na wananchi wenye manun'guniko yao nao watasikilizwa.

Mwakilishi wa Jimbo la Konde Mhe. Omar, kauliza kuhusu eneo la Makangale sehemu ambalo amelizungumza, ninafikiri nililijibu kwa ujumla wake. Pia Mhe. Omar alizungumzia ujenzi holela na uvamizi wa maeneo yaliyopangwa. Ni kweli kuwa lipo ongezeko la ujenzi holela katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba, sababu tatu zinazochangia katika jambo hili ni kama zifuatazo. Ukosefu wa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi, ukosefu wa mfumo mzuri wa utoaji vibali vya ujenzi, ukosefu wa ufatiliaji wa shughuli za ujenzi.

Wizara tayari imeshalifanyia kazi mambo hayo yote matatu. Kwanza wizara imetengeneza mipango mipya matumizi ya ardhi ya miji minne (4) kuweka mfumo mpya wa utoaji vibali. Pili wizara imeunda Kamati ya Usimamizi na Udhibiti Ujenzi na tatu wizara imeunda kikundi ufatiliaji, udhibiti wa ujenzi kila siku ya alkhamis.

Kuhusu mji wa Konde kwanza wizara imejipanga kufanya mipango ya mji huo, lakini kwa sasa wizara ikishirikiana na halmashauri itafanya ukaguzi katika eneo hilo na kuona athari zilizopo ili kuzipatia ufumbuzi kwa haraka.

Mhe. Suleiman Sarahan, utumiaji mzuri wa ardhi hususan eneo la Chake Chake, wizara inajiandaa kuanza utayarishaji wa *master plan* ya Chake Chake kama nilivyolieleza kwenye hotuba yangu ili kuondoa changamoto zilizopo katika mji huo, zikiwemo za ukosefu wa ardhi. Wizara yangu itafika katika mji wa Chake Chake kuziona changamoto hizo na kuzipatia ufumbuzi katika mpango huo mkuu wa matumizi ya ardhi ya mji wa Chake Chake. Nakubaliana na wewe vile vile na hoja ya kukutana Mawaziri watatu uliopendekeza ili kuziangalia kwa pamoja changamoto za mji huu.

Vile vile, nimshukuru sana Mhe. Maudline Castico kwa suala lake la kuwa serikali ihakikishe kwamba mashirika kama *ZSSF* kujenga majumba ya ghorofa ambayo ni mpango ambao sasa hivi serikali tunakwenda nao hasa ndio bado naendelea kusema tumeanza na ng'ambo tuitakayo, lakini tutafika na huko kwengine inshaallah kwa uwezo wa Mungu. Kwa hivyo sisi kama wizara tunaunga mkono ushauri wake huu na tunaendelea kuufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna suala la viwanja vya upimaji Tumbe/Chwaka awamu ya kwanza na ya pili vimegaiwa, lakini Chumbe/Chwaka bado, Mheshimiwa naomba vigaiwe na kupatiwa wananchi pia na wawakilishi.

Ni sahihi kuwa kazi ya upimaji imefanyika Tumbe/Chwaka awamu ya tatu na serikali tayari imeshapokea maombi mengi ya wananchi wanaoomba viwanja hivyo ambavyo kiukweli havitoshelezi. Ninamshauri Mheshimiwa kama bado hajawasilisha ombi lake namshauri afanye hivyo na suala hilo litafanyiwa kazi. Kupitia suala hili la Mheshimiwa wa Tumbe naomba niwajulishe Waheshimiwa Wawakilishi mwaka huu tumeseme Unguja hatupimi viwanja, tunaenda kupima viwanja Pemba, lakini Waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi basi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutapata viwanja katika maeneo ya Pemba na sote tutajenga nyumba zetu kule Pemba. *(Makofi)*

Naomba pia niende na swali la Mhe. Mihayo amependekeza kuwepo utaratibu mzuri katika ardhi wa kupunguza migogoro ya ardhi kwa kuunda chombo kimoja kitachosimamia uuzwaji, upimaji na utoaji wa vibali vya ujenzi na maswali mengine yanayohusiana na ardhi. Mhe. Spika, naomba kujibu swali hili kama ifuatavyo:

Napenda kumjibu Mheshimiwa kwamba serikali tayari imeona umuhimu wa kuwepo chombo hicho na tayari imeunda Kamisheni ya Ardhi ambayo jukumu lake ni kusimamia maswali yote yanayohusiana na ardhi ili kupunguza migogoro mingi ya ardhi.

Naomba pia niende kwa Mhe. Shamata. Mhe. Shamata ameshauri kuwepo kwa kitengo cha kuratibu maswali yote ya ardhi, ili kurahisisha utekelezaji wa maswali ya ardhi Micheweni. Ushauri tumeupokea na tutaufanyia kazi na lile la kusema watu wawepo pale pale Micheweni. Naomba kukuhakikishia Mhe. Shamata mwanafunzi wangu kwamba katika kila wilaya kuna maafisa ambao wanashughulikia maeneo yao. Lakini kwa maelezo uliyoyatoa kinachoonekana kwamba kuna haja sasa hata kwenye maeneo tukaweka *extension blocks* kwa hivyo tunaomba tuuchukue na tutaufanyia kazi.

Vile vile, naomba niende na swali la Mhe. Dr. Makame Ali Ussi nakubaliana nae kwamba kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi baina ya wananchi wenyewe na baina ya wawekezaji. Ushauri wako wa kuyatatua matatizo haya kwa haraka na kwa busara kubwa ili kuzuia mtafaruku mkubwa ndani ya jamii na wawekezaji tumeupokea. Naendelea kukuhakikishia kwamba wizara yangu imekuwa ikifatilia kwa karibu zaidi na kutatua migogoro ya ardhi kwa utaratibu kama ulivyotoa ushauri. Pia hutumika njia nyengine mbali za usulihishi ili kutatua migogoro hiyo.

Vile vile, wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine za serikali ikiwemo Wizara ya Misitu na Mazingira inalifanyia kazi suala la matumizi bora ya ardhi katika maeneo yanayochimbwa mchanga, mawe na kifusi ili kuhakikisha ardhi hizo zinarejeshwa katika hali inayokubalika kimazingira. Najua Mheshimiwa katika eneo lako una tatizo kubwa hasa la vijana wanaochimba michanga. Lakini kwa kushirikiana na wizara husika basi tutalifanyia kazi na ninamshukuru sana Mhe. Hamad Rashid aliweza kulitolea maelezo na ufafanuzi kuhusu suala hili.

Naomba ulipokee na ninakuahidi kwamba tutalifanyia kazi na nikiamini kwamba wewe kama kiongozi jasiri, ulishanichukua katika eneo moja na hili pia utanichukua kunipeleka kuona nini tunafanya tukashauriana vizuri zaidi.

Naomba niende kwenye swali la Mhe. Ali Khamis Bakari Mwakilishi wa Tumbe kwamba kuna viwanja vilipimwa eneo la Tumbe na wananchi wakaambiwa wachangie shilingi laki mbili ili wapatiwe viwanja hivyo. Lakini hadi leo viwanja hivyo wamepewa wakubwa serikalini na wananchi husika hawajapatiwa.

Mhe. Mwakilishi, viwanja 107 vilipimwa kwa gharama za serikali kwa ajili ya wananchi wa Kijichame na walitakiwa kutoa shilingi 200,000/= kwa ajili ya kupatiwa miliki, lakini waliotoa ni wachache na wamepatiwa na waliobakia hawakulipa na hivyo hawakuweza kupatiwa viwanja hivyo. Naomba nitoe wito

Mhe. Mwakilishi kama kuna watu waliotoa pesa zao na wana risiti mikononi bado hawajalipwa, basi tunaomba wizara yangu ipo kwa ajili ya watu na sisi tupo kwa ajili ya kuweza kuwahudumia naomba waende katika eneo husika, ili utaratibu ufatwe na waweze kupata haki yao iliyopo.

Niendelee na swali la Mhe. Shamata kwamba Mzee Karume aliweza kupanga vizuri mji lakini sasa hivi hakuna muongozo mzuri tunakwenda ovyo ovyo katika kupanga mji. Ninachotaka kukuhakikishia kwamba wizara yangu imekusudia kupanga miji 14 ukiwemo mji wa Micheweni. Katika kazi hiyo changamoto nyingi za mji huo zitaangaliwa ikiwemo ujenzi holela.

Aidha, wizara itaongeza kutoa taaluma na taarifa kwa wananchi ili kupunguza mizozo na kuongeza uelewa wa matumizi bora ya ardhi. Tumeanza kwa ng'ambo tuitakayo, kwa hivyo bado na Micheweni tutafika kwa hatua ya pili. Naomba nikuhakikishie hilo wala usiwe na wasiwasi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti wa Baraza Mhe. Mwanaasha ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani alisema kwamba ndani ya Jimbo la Chukwani kuna tatizo, naomba ukija katika majumuisho kesi ambazo zimetolewa maamuzi nimwambie ni ngapi na ngapi hazijatolewa maamuzi. Kwa sababu wananchi wanyonge wa eneo hilo wamedhulumiwa na kunyimwa haki zao.

Kwa sasa hatuna takwimu halisi ya kesi zilizopo kwenye jimbo lake, utaratibu wa takwimu tunaziweka kiwilaya. Lakini ninachotaka kukuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwa sababu sikuweza kwa muda niliokuwa nao kutembelea majimbo yote wala sijafika katika majimbo yote lakini kwa sababu watendaji wapo na mimi mwenyewe nipo. Ninachotaka kukuhakikishia kama kuna kesi kule bado tuendelee kushirikiana, naomba tuwe karibu, uniletee kuna kesi ipi na ipi ili niweze kuifatilia kama iko mahkamani watu wa mahkama wapo na kama ipo Ofisini kwetu, basi tutaifanyia kazi halafu utapata kujua idadi sahihi ambayo ipo.

Pia, ulitaka kujua kwa nini kesi zinachelewa, lakini sababu kubwa ya kuchelewa kwa kesi wakati mwengine inatokana na wadai wenyewe kwenda Mahkamani au Mawakili wenyewe wenye kesi kwenda mahkamani. Watakaotumia mbinu hizo za kutokwenda kwa sababu ya kucheleweshe kesi makusudi. Mara tutapolijua hili labda na kama na watu wote wanakwenda labda kesi haijaenda basi, pia wizara yangu kupitia Mahkama ya Ardhi italifanyia kazi.

Vile vile, kulikuwa na suala la Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe amezungumzia juu ya mambo 3 ya changamoto za Mahkama ya Ardhi. Alizungumzia hadhi ya majengo yenyewe, ukosefu wa karatasi za kuandikia, pia uchelewaji wa malipo ya wale ma-*assessors*.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Ofisi ya Mahakama ya Ardhi hasa, Mahakama ya Majestic haziendani na hadhi ya Mahakama kutokana na miundo ya jengo hilo. Kwa hiyo, bado wizara imelichukua hili kama changamoto na katika jibu la mwanzo ambalo Mhe. Naibu Spika alilijibu kwamba tumeshaomba pesa, lakini pia tunaangalia utaratibu wa kuona kwamba tufanyeje kuhakikisha jengo letu tunalolijenga au kupata eneo jengine kuendeshea kesi hizo.

Vile vile, ukosefu wa karatasi za kuandikia mwenendo wa kesi unatokana na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo *OC* inayopata wizara yangu. Aidha, hali hiyo inachangia pia kushindwa kuwalipa wazee wa Mahakama kwa wakati. Lakini juhudi zinafanywa ili kuweza kulimaliza tatizo hili. Tunajitahidi kila *OC* inapoingia wazee hawa kulipwa, hivyo kama kuna tatizo kubwa zaidi au kama kuna watu ambao hawajalipwa kiasi miezi miwili au mitatu, basi nikuombe Mhe. Mwakilishi tuonane labda uje tukae kwa pamoja tuweze kulitatua kwa pamoja, kwa sababu najua nilikwenda Pemba tukakuta hili tatizo, kwa tatizo la Pemba ilikuwa ni changamoto ya mwezi mmoja au miwili ambayo pesa ilikuwa bado haijaingia hasa ukizingatia kipindi hiki ni kipindi cha bajeti. Kwa hiyo, kila *OC* itavyoingia naomba kukuhakikishia kwamba tutalifanyia kazi na tutaweza kupunguza madeni hayo.

Pia, Mheshimiwa wa Jimbo la Chonga, Mhe. Shaib Said pia aliuliza suala la kutaka kujua wananchi wenye mashamba ambayo hayana hati na baada ya kutokea wajanja wachache na kudai ardhi hiyo na kuwashtaki.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, naomba niseme hivi mara nyingi kesi inatakiwa uwe na ushahidi Mahakamani, kwa hivyo ninatumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote wenye mashamba na ambao hawana hati kufuata taratibu za sheria zilizopo, ili kuweza kumiliki ardhi hizo na kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mhe. Asha Abdalla, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa aliuliza suala kuhusu ile kesi ya *restaurant* ya chakula *Chen* dhidi ya Peter Sipano imechukua karibu miaka mitano haijamalizwa.

Kwa mujibu wa kumbukumbu zetu Mhe. Asha hatuna kesi iliyotajwa kama hiyo, hata hivyo ipo kesi Nam. 173 ya mwaka 2013 ambayo ni baina ya Peter

Sipano kama mlalamikaji dhidi ya Vuai Ame Kondo na Haji Khamis Vuai ambapo kwa sasa ipo hatua ya kusikilizwa mashahidi, na kesi hii mashahidi walikuwa hawaendi Mahakamani ndio maana ikachukua muda mrefu.

Pia, Mhe. Mwakilishi alitaka kujua kwa nini Mahakama ya Ardhi haisimamii maamuzi yake baada ya kutoa hukumu. Nafikiri ni utaratibu wa Mahakama wakishatoa hukumu, hukumu ndio ishatolewa kwa hiyo vyombo husika vinachukua wajibu wake katika kutekeleza hukumu ambayo imetolewa na Mahakama.

Itakuwa si kazi rahisi mheshimiwa wangu kwamba Hakimu aende katika kila sehemu husika na kila kesi atoe hukumu kufanya hivyo, lakini kesi ikishakutolewa hukumu maana yake maamuzi ya Mahakama ndio yanakuwa yanachukuliwa.

Naomba nijibu suala la Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwenyekiti wa Baraza ambae pia Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni, suala lake alilowasilisha kwa maandishi. Kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama ya Ardhi husikiliza mgogoro wa ardhi na kutoa maamuzi. Na inapompa ama mdai au mdaiwa haki na inapotokea bado mdaiwa au mdai hajaondoka katika eneo alilotakiwa kuondoka, yule aliyepewa haki na Mahakama hutakiwa kuleta ombi la utekelezaji wa hukumu na Mahakama hulisikiliza ombi hilo na hutoa amri ya kumuondoa yule ambaye ameshindwa kwenye kesi na hataki kuondoka. Huo ndio utaratibu kama nilivyosema hapo awali.

Mhe. Spika, kwa upande wa ardhi kwa sasa hivi naomba niyaseme haya, nafikiri nimeyasema mengi na mengine yalijiingiza humu humu ya waheshimiwa wengine kwa sababu michango yao ilikuwa inaelekezana. Sasa hivi naomba niende kwenye sekta ya maji.

Katika sekta ya maji, nianze na Mhe. Hamza Hassan Juma ambae alianza na hoja ya kuipongeza wizara na sisi tumeipokea tunakushukuru ahsante sana. Pia ulitutaka tufanye ziara maalum Ras Al Khaimah kuhusu kumaliza vile visima vya Ras Al Khaimah. Ushauri umepokelewa na naomba nikuhakikishie kwamba katika hili kuna kamati ambayo inaongozwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman na sisi katika kamati tulivyokaa tuliliona hili, visima vya Ras Al Khaima ni vingi na serikali uwezo wake ni mdogo, kwa hiyo tukaona kuna umuhimu wa kuwaomba watusaidie, watuongeze *component* ya kusambaza mabomba, kutupatia *pump,* ili watu waweze kupata maji safi na salama kwa lengo tulilokusudia. Kwa hiyo, ushauri wako umepokelewa.

Pia alitaka Masheha kushirikiana katika kupeana taarifa juu ya mabomba yanayovuja na ubadilishaji wa mabomba machakavu. Naomba nikuhakikishie kwamba Mhe. Hamza wizara kupitia Mamlaka ya Maji ni miongoni mwa kazi zake za kawaida za kila siku kulingana na uwezo wake inategemea zaidi miradi mipya au ya wafadhili.

Ninachotaka kukuhakikishia kwamba tutashirikiana kwa asilimia kubwa na masheha na wao ndio wanaotupa taarifa za maeneo husika na pia hata hii issue ya kubadilisha mabomba machakavu,. Hata unapokwenda kwenye maeneo masheha wanashirikishwa ipasavyo.

Pia alitaka kujua maendeleo ya mradi wa uimarishaji wa miundombinu mjini. Mhe. Spika, ni kwamba utekelezaji wa mradi umeshaanza na unaendelea na kazi za uchimbaji wa visima. Aidha, kazi ya uendeshaji wa mitandao mibovu ambayo itabadilishwa na kuwekwa mitandao mipya bado unaendelea na haujaanza.

Suala la uajiri wa wafanyakazi wa kujitolea ambalo limezungumzwa na watu wengi katika vituo vya maji. Hili naomba nilijibu kwa ujumla wake, kwa sababu limetokea katika maeneo mengi. Katika vituo vya maji kuna wafanyakazi wa kujitolea na wamegawanyika katika utaratibu mbali mbali kwenye maeneo husika, ikiwemo utekelezaji na uendelezaji wa miradi ya *TASAF* ambapo wananchi walichukua ahadi ya kulinda na kuienzi miradi hiyo.

Kuna miradi inayoendelezwa na uongozi wa jimbo ama kupitia Mhe. Mbunge au Mwakilishi kwa baadhi ya wakati husika ambapo waheshimiwa huwateuwa watu katika jamii husika kwa ajili ya kulinda miradi hiyo.

Kuna baadhi ya maeneo ya uwekezaji huanzishwa miradi ya maji na kuweka ulinzi katika maeneo husika. Hali hiyo imepelekea katika maeneo mengi kuwa na walinzi wa kujitolea.

Mhe. Spika, na hili naomba nilizungumze kwa ufasaha kwa sababu ni suala ambalo limejitokeza sana, kwa sababu wale wafanyakazi wa kujitolea leo mimi Mhe. Mwakilishi, kesho yuko Mhe. Mwakilishi mwengine umeanzisha mradi lakini mradi ule ulivyoanzisha ilibidi utafute mtu ndani ya eneo lako kumuweka pale na wawakilishi na wabunge wengi mwanzoni walisema watajitolea kuwalipa wale maposho.

Sasa hivi kwa kuwa mwakilishi yule au mbunge yule hayupo kwa hiyo yule aliyekuwepo imekuwa sasa hana pakulipwa na malalamiko yamekuwa mengi.

Lakini mamlaka sasa hivi imeanza kufanya utaratibu, kutokana na mapato na uwezo ambao tumekuwa nao hatuwezi, kwa sababu wako wengi mno, tukisema gharama ile ukiiangalia hatuwezi kuwalipa wote, lakini bado tunaendelea na utaratibu na tutaona nini tufanye kuna mwelekeo katika hili.

Sasa hivi tunaanza ku-*study* na ku-*analyze* ile *situation* ambayo ipo ili tuifanyie kazi. Mimi binafsi na mwenzangu Naibu Waziri tumejikita katika suala zima la maji toka tumeingia, ili tuhakikishe wananchi wetu wanapata maji safi na salama kwa kipindi hiki cha muda mfupi kijacho, ili tukija hapa wakati mwengine tuhakikishe kwamba haya mengi yaliyokuwa kama ni changamoto basi iwe kwa asilimia kubwa tumeweza kuyatatua.

In shaa Allah Mwenyezi Mungu atatusaidia kwa nia zetu, kwa sababu tumekusudia kabisa kufanya kazi hii kwamba serikali ina nia nzuri na sisi tuna nia nzuri, lakini na sisi wajumbe tuna nia nzuri ya kuwasaidia watu wetu kwa asilimia kubwa.

Mhe. Spika, vile vile limekuja suala la maposho ya wafanyakazi wa Mikoani. Naomba niseme suala la wafanyakazi ambao wako katika mamlaka wengi waliokuweko katika Mikoa na Wilaya maposho yao yanaingia moja kwa moja kwenye mshahara na huu ni utaratibu ambao ulianzishwa katika mishahara ya mamlaka. Hasa kama wanataka yamegwe wapewe mkononi na mshahara upelekwe tofauti itakuwa ni vitu vyengine, lakini hakuna mfanyakazi ambae hapewi maposho yake, maposho yale yanaingizwa kwenye mshahara na analipwa wakati mshahara unatolewa moja kwa moja kwenye mshahara.

Kulikuwa na *issue* kwamba *ZAWA* waanzishe utaratibu wa kulipa kwa kutumia simu**.** Labda niseme kwa ujumla wake kwamba sasa hivi tayari mamlaka ya *ZAWA* imeshafanya mazungumzo kwa hatua ya awali na Benki ya Watu wa Zanzibar katika kuhakikisha kwamba wanaweza kutumia kampuni fulani kama Kampuni ya *Maxcom* Tanzania na ishafanya mazungumzo nayo, ili kuanza kutumia mitandao katika ulipiaji wa maji.

Kuanzisha vituo katika maeneo mengine mengi ili kuwarahisishia wananchi kulipa kwa uharaka zaidi. Kwa hiyo, suala hili bado tunaendelea nalo na tumo kwenye mazungumzo.

Vile vile kutakiwa *ZAWA* kuanzisha *database* ya wateja. Ninachotaka kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi wanaotusikiliza kwamba *ZAWA* tayari imeshaanzisha *database* na sasa inaendelea kuhakiki

wateja wake ambapo, kwa sasa tushafikia wateja 85,000 wamo ndani ya *database* ya *ZAWA*.

Pia ilikuja issue ya kutoa bili kwa watumiaji *ZAWA* inaendelea na zoezi la kutoa bili kwa wateja wake waliofungiwa mita na kwa baadhi ya maeneo. Kwa sasa hivi mita zile hawajafungiwa watu wote na bado zoezi linaendelea la kufunga mita isipokuwa maeneo ya Makadara, Gulioni, Mchangani, Bububu na Mwanakwerekwe ambao tayari wameshafungiwa mita na bili zao zinakwenda kama kawaida. Isipokuwa *ZAWA* sasa hivi ina mpango wa kuendelea kufunga mita na katika kipindi hiki tumekusudia kufunga mita 20,000 na kazi hiyo imeshaanzwa na inaendelea. Mita tulizokuwa nazo mpaka sasa ni 20,000 kwa hiyo tutafunga katika kipindi hiki.

Lakini *issue* ya kukusanya mapato *ZAWA* kwa kweli hata mimi nakiri kwamba ukusanyaji wa mapato umekuwa mdogo, umekuwa mdogo kutokana na muamko wa wananchi katika kulipia maji, na hasa kutokana na changamoto iliyopo. Mtu anapata maji kwa mgao au anasema kisima cha *TASAF*, anasema kisima hiki cha Mbunge, kisima hiki cha mwakilishi anasahau kwamba mitandao ile ni mamlaka ya *ZAWA*, pia kuimarisha hiyo huduma kwa maana ya ulipaji umeme na mambo mengine yote inategemea *ZAWA* na ndio maana huu uchangiaji wa maji tuliuhitaji.

Namshukuru sana Mhe. Said Soud alipotoa ufafanuzi wake pale kwamba serikali inabeba jukumu kwa sababu tukiangalia gharama inabidi kila mwananchi alipie 12,000, lakini sasa hivi serikali imekubali ku-*subsidize* nasema kwamba mwananchi alipie 4000.

Kwa hiyo, serikali ina nia ya dhati kuhakikisha kwamba inawasaidia wananchi wake na hili suala lilikuja katika suala la awali na tuliweza kulijibu, lakini pia limejirejea. Kwa hiyo, niwaombe sana sana Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba watoe ushirikiano wao kuhamasisha wananchi majimboni ili tuweze kuongeza makusanyo. Tutafanya jitihada hata kwa mgao lakini maji yapatikane, ila na nyinyi mtusaidie pia pamoja na *customer care* tuliokuwa nayo na wafanyakazi waliokuwepo. Pia tunaomba sisi tutatoa elimu kwa ushirikiano pamoja na nyinyi mimi naomba tushirikiane, ili mapato yaweze kuongezeka.

Mhe. Spika, vile vile niwaombe sana waheshimiwa wa Baraza lako maana yake lilikuja suala la kununua mabomba imara. Sisi kama taasisi mara zote tunaangalia kitu chenye *quality*, lakini wakati mwengine inatokea waheshimiwa wanachangia kwa kununua, lakini tunaomba sana wakati wa

ununuzi wa vifaa hasa kwenye mabomba ya maji, Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Wabunge, basi tulikuwa tunaomba mshirikiane na *ZAWA* hata kukupeni zile *specification* tu, ili tuweze kuwa na mabomba imara yatayoleta tija na yataweza kudumu kwa muda mrefu. Niwaombe sana katika suala hilo.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Hamza aliniomba pia suala la wizara kutembelea katika majimbo na hasa katika Jimbo la Shaurimoyo. Sisi tunamshukuru Mhe. Hamza kwamba sisi hatuna tatizo la kutembelea katika maendeleo na ndio kazi yetu na kiko kitengo kinatembelea, lakini pia na yeye tutafika katika jimbo lake atukaribishe tu na sisi tutafika.

Pia, Mhe. Shadya alizungumzia sana kwamba visima havisafishwi na zinazosafishwa ni *pump* tu. Naomba nimjibu kwa umakini kabisa Mhe. Shadya Mwakilishi wa nafasi za wanawake kule Kusini Pemba kwamba suala la usafishaji wa visima ni jambo la kawaida kwa *ZAWA*, na inafanya hivyo kila inapohitajika, na *pump* huwa zinawafanyiwa matengenezo, *pump* huwa haisafishwi sana mara nyingi huwa inafanyiwa matengenezo, lakini visima na matangi huwa vinasafishwa. Lakini havisafishwi kila siku kama tunavyosafisha vyombo nyumbani kuna utaratibu wake na kuna wakati wake.

Lakini ucheleweshwaji wa fedha za malipo ya likizo kwa wafanyakazi. Mimi nikubaliane na Mhe. Shadya kwamba ni haki ya kila mfanyakazi kupatiwa fedha ya likizo, na Mamlaka ya Maji huwa inafanya hivyo kila inapopata uwezo, wakati mwengine inawezekana wafanyakazi wanaenda likizo ofisi haina pesa. Kwa hiyo, yanabaki kama malimbikizo, *in shaa Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunaomba sana kwamba tutapopata uwezo na serikali itapotutilia pesa basi wafanyakazi huwa wanalipwa pesa zao.

Kuna suala la ucheleweshaji wa kupelekwa fedha za *ZSSF*. Naomba nimuhakikishie mwakilishi kwamba ni haki ya kila mfanyakazi kuchangia, na muajiri pia kumchangia na kupeleka zile pesa *ZSSF* kwa ajili ya malipo ya baadae ya uzeeni. Lakini kinachotokea ni nini? Wakati mwengine mshahara imefika, pesa imekatwa lakini fedha ile ya muajiri katika kulipia asilimia muajiri anakuwa bado hajapokea fungu.

Kwa hiyo, fedha zile inabidi zibaki kwenye kasma ili zibakie pesa ya muajiri ndio pesa zipelekwe. Kazi hiyo inafanywa na nina amini hakuna mfanyakazi atakayekwenda kuangalia akute pesa zake hazipo.

Mhe. Spika, kingine ninachotaka kusema kwamba hakuna pesa ya mfanyakazi hata mmoja kwa sababu hata mtumishi mwenyewe ana haki ya kwenda *ZSSF*

kuchukua *balance sheet* yake ya kuona michango yake inavyoingia. Kwa hiyo, mimi naomba nimuhakikishie kwamba fedha hizo zipo na fedha hizo mara tu baada ya bajeti tukishakupitisha mafungu na bajeti ikapatikana basi ule mchango wa asilimia ya muajiri pesa hiyo itakwenda.

Mhe. Spika, vile vile aliulizia suala la magari ambalo yana madeni ya mafuta kutofanya kazi. Kusema wizara yangu kupitia *ZAWA* inakuwa na utaratibu wa kukubaliana na vituo vya mafuta, ili tuweze kupata mafuta ya kuendesha kazi zake, na fedha ikiingia mara zote huwa tunafanya malipo. Mpaka sasa hivi hatuna taarifa wala hatujapokea kwamba gari hazifanyi kazi kwa sababu ya kutokuwa na mafuta na vituo vimekataa kuwalipa.

Mhe. Spika, pia kulizungumzwa kisima cha Wambaa kuhusu *issue* ya barabara ile ambayo haijasafishwa. Naomba nilipokee hili na hili tunalijua lilishakuja kwenye suala la awali siku ile na tumeshalijibu, kwamba pana mikarafuu na miti ilikatwa, kwa sababu ya uchimbaji wa visima. Pia suala hili bado tunalifanyia kazi na hali ya fedha ikiruhusu basi nataka kukuhakikishia kwamba wale watu watalipwa fidia yao.

Tunaendelea kupitia kwa sheha wa shehia kutafuta njia mbadala ya kuhakikisha kwamba tunaweza kufanya hiyo kazi. Sasa hivi mamlaka yangu ina mpango wa kutengeneza njia ya kudumu hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Jaku aliuliza kuhusu wananchi wa jimbo la Michamvi kwamba hawapati maji. Mimi nimuhakikishie Mhe. Jaku kwamba ni haki ya kila mwananchi wa Zanzibar kuweza kupata huduma ya maji safi na salama, na kwa wananchi wa Michamvi walikuwa wanapata huduma ya maji kutoka katika kisima kilichochimbwa na serikali kilichopo Michamvi kwa miaka ya nyuma.

Hata hivyo, kisima hicho kimeathiriwa na maji ya chumvi na sasa hivi hakitumiki. Aidha, hali ya upatikanaji wa maji safi na salama Michamvi kwa sasa hivi mamlaka imeanza kuchukua hatua ya awali, ambapo kwa sasa mtambo mmoja mdogo umeanza kufungwa na unasaidia kupata maji ya kunywa katika kijiji cha Kae na Pingwe kwa mgao.

Upatikanaji wa maji utaimarika zaidi baada ya kuendeleza visima vilivyochimbwa na Ras Al Khaimah, kama tulivyosema hapo mwanzo. Kwa hiyo, tumuombe tu Mheshimiwa Jaku aendelee kushirikiana na wizara yangu na mamlaka yangu kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji safi na salama na kama kuna changamoto basi tuko tayari kushirikiana ili kuzitatua.

Kuharibika kwa pump katika kituo cha Jambiani. Mimi naomba niseme kwamba ni hali ya kawaida katika utoaji wa huduma ya maji mashine zilizomo visimani kupata maharibiko.

Kisima cha Jambiani vile vile kimepata maharibiko ya mashine hayo yametokea katika siku mbili zilizopita na hivi sasa kimo katika matengenezo na huduma itarudi tu baada ya kukamilika kwa matengenezo ya pump hiyo.

Mhe. Spika, lakini vile vile Mhe. Nadir alizungumzia upelekaji wa maji kwa matajiri tu na kuwaacha wanyonge. Mhe. Nadir mwakilishi wangu, mtoto wangu wa Jimbo la Chaani kwa bahati nzuri naomba nikuhakikishie serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haina ubaguzi, na serikali hii na naomba Wajumbe wa Baraza hili watathibitisha kama serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi haina ubaguzi ndio maana sisi tuko hapa kwa sababu serikali haina ubaguzi.

Kwa hiyo, katika utoaji wa huduma za maji kwa wananchi imekuwa ikiwapelekea wananchi wote maji wa mjini na vijijini wakiwemo wananchi wa Chaani. Pia kama kulikuwa kuna tatizo basi bado nikuombe Mhe. Nadir kwa sababu Chaani si miongoni mwa sehemu yenye matatizo makubwa, kama Chaani kuna matatizo makubwa na kama kuna wanyonge ambao unahisi hawapati hiyo haki, basi mimi nikuombe idara yangu ipo kwa sababu ya kuwatumikia watu na tuko tayari kuwatumia na ndio maana Mhe. Rais alituamini akatupa wadhifa huu.

Vile vile, kusita kufanya kazi kwa kisima cha Chunga kuna swali lilikuja tukasema Chunga tuna visima vinne; viwili vikongwe vinafanya kazi na viwili vimechimbwa kupitia mradi wa *Ras Al Khaimah* na vipo katika mipango ya utekelezaji wa kuunganishwa kama visima vyengine ambavyo tumevitamka vya *Ras Al Khaimah*. Lakini bado niwaombe Waheshimiwa Wawakiilshi kwamba tuendelee kushirikiana, wananchi wanatuamini sana.

Mhe. Spika, Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Konde, Mhe.Omar Seif Abeid, alisema uhaba wa huduma ya maji wa Mkia wa Ng'ombe na mabomba mabovu yamejaa kwetu. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa wananchi wa Mkia wa Ng'ombe watafaidika vizuri na huduma hii kwa kupata bomba kubwa la nchi sita kutoka kisimani hadi Makangale; kwa hivi sasa kuna bomba ya nchi nne ambayo ni ndogo inayotolewa kwa mgao baina ya Makangale na mkiwa wa ng'ombe, tunamuomba Mhe. Muwakilishi ili kuweza kupata bomba zinazofaa aje tushirikiane. Nampongeza sana Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Konde alikuja kwa hatua ya awali kwa maeneo ya Konde tulifanya kazi nae kwa pamoja na sasa hivi yeye mwenyewe amekiri hapa kwamba wananchi wa

Konde katika maeneo mengine wanapata maji lakini bado naomba na hili aje tukae pamoja tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, lakini vile vile upande wa maji Shumba Viamboni, uhaba wa maji. Wananchi wa Shumba wanapata huduma kupitia kisima kilichopo Vikunguni ambacho kwa hivi sasa kimepunguwa uzalishaji ambapo Serikali kupitia visima vya *Ras Al Khaimah* imechimba kisima chengine na huduma ile itaimarika baada ya kuendelezwa kwa kisima hicho kama nilivyosema pale awali. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa tuendelee kushirikiana.

Mhe. Spika, lakini vile vile Mhe. Abdalla Diwani, Mheshimiwa wangu wa Jimbo la Jang'ombe alielezea kuhusu mapato madogo ya ZAWA ukilinganisha na makisio, na hii nafikiri nimeshaizugumzia pale awali kwamba sasa hivi kwa pamoja tushirikiane, tunajitahidi kuboresha huduma lakini tunajitahidi kutoa wito kwa wananchi kupitia vipindi mbali mbali lakini mikutano mbali mbali, lakini niwaombe na nyinyi Waheshimiwa wa Baraza tena kwa mara nyengine tushirikiane, tuwahamasishe wananchi wetu kuona umuhimu wa kuchangia huduma za maji kwa faida yetu sote na kwa faida ya jamii.

Mhe. Spika, vile vile taarifa za upatikanaji hazina ukweli, karibu miji na vijiji vyote vya Zanzibar tayari vimeshafikia. Mimi nilikuwa naomba kusema hili la Mhe. Abdalla Diwani, nimjibu hivi; kwamba anasema taarifa za upatikanaji wa maji hazina ukweli, kwa sababu hata Mhe. Rais alivyotoa hotuba yake alisema 87% naungana nae na naungana nae mkono. Hata mimi wakati nimeingia kwenye Wizara hii Mhe. Mwakilishi wa Jimbo langu la Jang'ombe nataka nikuhakikishie nilikuwa na uwelewa kama wako, nikasema inakuwaje mnaniambia eti 87% kwamba maji yanapatikana wakati maji mimi nikitembea nikirudi siyaoni na mgao unaendelea, lakini kumbe wenzetu wataalamu wanapozungumza 87% ya maji yamefika katika maeneo wanazungumzia uchimbaji, wanazungumzia usambazaji, lakini hawajazungumzia utokaji.

Kwa hiyo na mimi nilikuwa sielewi na ni changamoto kubwa nafikiri na mwenzangu Naibu Waziri ambayo ilikuwa inatupa hoja na ndio maana hata ninaposimama hapa na nilivyokuwa nazungumza nikawa nasema, kwamba mimi kitu changu cha mwanzo nilivyoingia mpaka leo tunafanya kazi na maji, tukasema haiwezekani, kwa sababu nilivyosikiliza hotuba ya Mhe. Rais, nikawa sielewi, lakini walivyokwisha kunipiga shule wananifanya imenibidi nifike pahala nielewe, wanapoizungumzia 87% wanazungumzia idadi ya visima vilivyochimbwa na uwezo wake na kazi nyengine ambazo zimefanywa. Lakini hizi kazi zote tukizimaliza kwa ujumla wake maana yake maji yatakuwa hayana tatizo, kwa hiyo kazi zote zitafanywa kwa asilimia 87% ya usambazaji

na nini. Kwa hiyo taarifa zina ukweli lakini ukweli wenyewe inabidi lazima upate elimu kidogo ili tufike pahala tufahamiane.

Mhe. Spika, lakini kuna swali ambalo mdogo wangu Mhe. Muwakilishi ndugu yangu wa Jimbo la Uzini Mhe. Simai, alilizungumzia kuhusu upatikanaji wa maji Uzi. Mhe. Simai nataka kukwambia Uzi Ng'ambwa inapata maji kutoka katika Vituo vya Unguja Ukuu ambavyo kwa sasa hayatoshelezi kutokana na ongezeko la mahitaji. Kwa sasa Serikali inaendelea na mazungumzo na MILELE Zanzibar foundation na kuendeleza mradi, ili kuondosha tatizo la maji katika kipindi hicho.

Aidha, kwa hatua za awali, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya MO kutoka Ujerumani imefunga mitambo ya kuchuja maji chumvi kuwa maji safi na salama kwa ajili ya wananchi wa Uzi, kuweza kupata maji ya kunywa na mitambo hiyo sasa inafanya kazi, na nafikiri Mhe. Muwakilishi ndugu yangu Mhe. Simai, kama hili ulikuwa hujalisikia basi mimi naomba mimi na wewe kwa pamoja hata mimi nilikuwa na hamu ya kwenda kutembelea katika eneo hili basi nafikiri tushirikiane siku hiyo tufatane baada ya kupitisha bajeti hii basi twende tukaone jinsi ya mtambo ule unavyofanya kazi na tuweze kutoa elimu zaidi kwa wananchi na kuona umuhimu wa kuendeleza maji chumvi kwenda kwa maji safi.

Mhe. Spika, lakini pia kulikuwa kuna swali la tatizo upatikanaji wa *pump* za maji na kuharibika mara kwa mara, nimeshalijibu lakini Mhe. Simai aliliuliza naomba pia nilijibu tena. Serikali kupitia Mamlaka ya Maji imeweka mkakati maalum wa kupitia na kuziangalia vianzio vyote vya maji na kuona vinafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Swali la kuharibika kwa *pump* ikiwa kama ni *mashine* nyengine ni jambo la kawaida na Mamlaka inachukuwa jitihada za kuzifanyia matengenezo na kurejesha huduma ikibidi kuziweka nyengine ili huduma hii iwe endelevu. Kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba tutawatumikia wananchi.

Mhe. Spika, Mheshimiwa wa Jimbo la Mtambile, Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Mtambile Mhe. Jecha, tangi la Mtambile linavujisha maji mengi. Ni kweli tangi linavujisha na Mamlaka imo katika jitihada za kupata vifaa kwa ajili ya kuvifanyia matengenezo, taarifa hizi tumezipata na kwa sababu matangi yale chuma chake si chuma ambacho unakwenda dukani tu kununuwa ni chuma ambacho inabidi kiagizwe, kitafutwe ndio kifike lakini tumelipata na jitihada zishachukuliwa tunasubiri *plate* yale yafike, ili tuweze kukamilisha huo ujenzi. Lakini tunakushukuru sana kwa mchango wako na tunakuhakikishia kwamba

mara tu kitapofika basi tatizo hilo na Mtambile litaondoka na tutaweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, lakini vile vile nimshukuru *classmate* wangu Mhe. Mohammedraza ambae ameulizia wananchi wake wa Jimbo la Uzini hawana maji kwa kipindi kikubwa. Vile vile bado naomba nilichukuwe kama changamoto lakini Serikali kupitia ZAWA kwa kipindi sasa inaendelea kushirikiana nae na kutatua tatizo la maji Jimbo la Uzini na itazidi kuendelea ushirikiano mwema wakati wowote kwa hali na mali kwa ustawi wa wananchi wa Uzini.

Mhe. Spika, Naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru sana sana na kumpongeza sana sana Mhe. Mohammedraza kwa kazi kubwa anayoifanya. Mimi nikipanda ngazi basi na yeye namkuta au ananikuta kule ZAWA, kwa hiyo siku zote namuona hii bidii kubwa anayoichukuwa lakini najuwa anahangaikia wananchi wake wa Jimbo la Uzini na mimi naomba nimuhakikishie Mheshimiwa, amesema anahitaji mashirikiano, hapa mashirikiano 100% na sitokuwacha mkono kila litapotokea na sasa hivi tunavyoendelea na tutaendelea kuwa na wewe kuhakikisha kwamba si wananchi wa Uzini tu lakini hata wananchi wa maeneo mengine ya karibu basi wanafaidika kupitia Jimbo la Uzini; naomba nikushukuru sana.

Mhe. Spika, lakini vile vile ukosefu wa maji wa Jimbo la Kiwengwa, dada yangu ndugu yangu Mhe. Asha Abdalla alisema visima vitano alivyovitaja Mhe. Mwakilishi vilitokana na *Ras Al Khaimah* na alisema kuna ukosefu wa maji Jimbo la Kiwengwa. Jimbo la Kiwengwa kuna visima vitano visima vinavyotokana na *Ras Al Khaimah* na kama tujuavyo mradi huu tu umechimba visima na kujenga tangi katika baadhi ya maeneo. Kazi iliyobaki kuziendeleza visima hivi bado tunaomba mpitishe bajeti, sisi kama Serikali tutaendelea kulifanyia kazi lakini na lile swali la ombi la kuzungumza na watu wa Rasilhema basi kupitia Mwenyekiti wa Kamati Mhe.Haroun Ali Suleiman tutaendelea nalo, lakini Serikali ina mpango wa kuziendeleza visima na hivi na ninaomba kila wakati ninasema kwa uwezo wa *Allah,* lakini naomba niamini kwamba tutajitahidi kufanya kazi kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata maji katika maeneo yote.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Harusi Said Suleiman, Mhe.Naibu Waziri wa Afya, akiwa Mwakilishi wa Jimbo la Wete, alisema maji yako mengi Pemba lakini miundombinu ya maji si mizuri, mabomba yanapasuka na maji mengi yanapotea hususan katika Jimbo la Wete. Sehemu kubwa ya mabomba yanayopasuka ni yale ya zamani ambayo ni *pipe* zinazo-*rust* na kupasuka.

Lakini bado Serikali kupitia Mamlaka ya ZAWA, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya ZAWA inafanya jitihada ya kubadilisha kulingana na upatikanaji wa fedha, kila hali inapokuwa tunajitahidi sana. Nikuombe sana Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wete bado tushirikiane na ninaendelea kushirikiana hasa kwa Waheshimiwa wenye Majimbo kwamba tayari mna mfuko wa Jimbo, kwa haya madogo madogo ya kubadilisha ambayo tunaweza kutumia mfuko wa Jimbo basi niwaombe sana kwa imani kabisa kwamba *priority* katika maeneo ambayo hapa maji yapo tatizo ni dogo basi tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunawapenda sana wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile naomba niendelee na Mhe. Mtumwa Peya mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini pamoja pia na swali hili limejirejea la Mhe.Asha. Kuhusu wale wafanyakazi wa kujitolea nimeshalijibu, naomba kwa ruhusa yenu Wawakilishi nisilijibu tena, lakini nimelipokea na majibu yake nimeshayatoa basi nisiendelee kuyatoa kwa sababu pia ya kuangalia muda.

Mhe. Spika, lakini pia kulikuwa na swali la uungaji holela wa maji alilizungumzia Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake simuoni Mhe. Suleiman Sarahani. Mimi niombe sana ushauri wake tumeupokea, aidha ZAWA katika kutatua tatizo hili limeweka masharti maalum wakati wa uungaji na kwamba mafundi wa ZAWA tu ndio wanaoruhusiwa kufanya kazi ya uungaji. Tunajuwa wako mafundi wanaopita huko kukatakata mabomba wakafanya hivyo, lakini sasa hivi Wizara yangu inaendelea kujipanga vizuri na mimi ninahakikisha kwa kushirikiana na nyinyi kwa sababu ndio mnayajua maeneo, mnayoyajua wapi kuna tatizo, lakin kwa kushirikiana na wananchi wetu wakubali kutoa taarifa za uhakika basi mimi ninaamini matatizo haya mengi tutayaondoa, kama sote tutakuwa na uthabiti wa dhati ndani ya nafsi zetu kuhakikisha kwamba tunatekeleza lengo la Serikali la kuondosha matatizo yaliyokuwepo na kuwapatia wananchi wetu maji safi na salama.

Mhe. Spika, lakini vile vile Mhe. Nassor Jazira, alizungumzia...

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tatu tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: ...hee yako mengi maswali. Ahsante Mhe. Spika, naomba niende tatizo maswali yalikuwa mengi arubaini na nane labda mengine..lakini kuna umeme, kuna mazingira sijagusa, sasa hivi ninamalizia sekta ya maji. Ninakuomba Mhe. Muwakilishi unipe nafasi ili niweze kuwajibu kidogo Waheshimiwa.

Mhe. Spika, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, kusema kweli tunamshukuru lakini naomba tushirikiane na uongozi wa Jimbo katika kulipatia ufumbuzi tatizo la maji Jimbo la Kikwajuni kama nilivyosema maeneo mengine. Katika swali la Jimbo la Kikwajuni katika ujenzi wa mradi mkubwa ule wa Mji Mkongwe wa ADB wa Benki ya Maendeleo ambapo pia na Jimbo la Kikwajuni upo, sasa hivi umeanza kufanya kazi na ninaomba tutashirikiana katika kuhakikisha wananchi wanafaidika na maji haya.

Mhe. Spika, Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa; Mwakilishi wa Viti Maalum, pia alizungumzia kuhusu Jimbo la Chumbuni kuwa lina visima vingi lakini wanaofaidika ni watu wa mjini. Nakubaliana na wewe lakini mtandao na mtiririko hata Chumbuni wanafaidika lakini unapita njia lakini yanakwenda katika maeneo ya Rahaleo, Kikwajuni, Mji Mkongwe na kwengine, kwa hiyo na tunasema kwamba bora tuwe nacho kidogo lakini tukubaliane kugawana kidogo kidogo. Kwa hiyo mimi ninaomba tuna vingi likini tushirikiane kwa pamoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ninaomba utoe hoja tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Naam, nitoe hoja! Umeme sijafika. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa ruhusa ya Waheshimiwa Wajumbe, majibu yako mengi katika maeneo ya ZECO, kuna maeneo ya mazingira naomba nitayakabidhi kwenye Baraza majibu hayo muweze kupatiwa, ili muweze kuwa na majibu sahihi ambayo mimi tayari nimeshayajibu katika karatasi zangu kwa hiyo baada ya hapo mkisha kupatiwa kitachokuwa hamjakielewa au kinachohitaji mashirikiano, nakuombeni tukizingatie, ili sote tufanye kazi kwa pamoja kama Wajumbe wa Baraza, Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi ambayo tuna nia, lengo langu nikuyajibu yote nilikuwa ninakwenda kwa sekta, lakini kutokana na muda basi mimi naomba kwa ruhusa ya Mhe. Spika, nitoe hoja, ili Baraza lako hili liridhie hotuba yangu hii ya Makadirio na Mapato na iweze kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2016/17, naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru sana Mhe. Spika, tunachojadili ni bajeti ya wananchi na kulikuwa kuna utaratibu na ukatizama hii programu kuu ni moja tu na ndogo ni moja tu na Wajumbe wengi. Mhe. Spika, aliyepita ambae umemrithi wewe alikuwa akitumia hekma katika suala kama hili.

Vifungu ni kidogo, sasa tunataka jicho lako la huruma uangalie, nina-*quote* kifungu 98 kwa mujibu wa kanuni zetu.

Mhe. Spika: Shida yako sijaifahamu Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: ehee! uzuri. Ungalikuwa na kanuni ningekufahamisha kidogo Mhe. Spika, Kanuni ya 98(3);

Mhe. Spika: Isome;

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: "Endapo hoja ya kupunguza fungu kwa kupunguza kifungu chake fulani kidogo cha fungu hilo imekubaliwa au kukataliwa, hoja nyengine si zaidi ya mbili zinaweza kuruhusiwa juu ya kupunguza kifungu hicho".

Programu Kuu ni moja na Kifungu Kidogo kimoja wachangiaji wako wengi wanaweza kusema watu watatu, wawili, mchezo ukawa umekwisha na hii hoja ya wananchi, kila mtu hana maji, hayatoki kwake Jimboni na majawabu mengine Mhe.Waziri, hayakuturudhisha sisi humu. Kwa hiyo nitaanza kuondoka mimi, Mhe. Suleiman bosi wangu Miraji hapa, wengine wakakosa katika fungu, tuangalie kitabu na hiki kitabu kina makosa vile vile.

Mhe. Spika: Mheshimiwa sawa naomba ukae. Ndio pale nilipokutakeni muwe makini sana Waheshimiwa kumsikiliza Mheshimiwa alipokuwa akijibu. Unajuwa makaratasi aliyonayo bado ni mengi, halafu kwa *style* anayokwenda nayo anamjibu mtu mmoja mmoja, itatuchukuwa muda mrefu sana kumaliza. Hivi sasa pia tutatengua kifungu cha muda yaani tutaongeza muda, lakini lengo ili tuende kwenye vifungu, tupitishe vifungu. Kanuni ninaizingatia lakini na mwenyewe Waziri ameahidi kwamba atakujibuni kwa maandishi watu wote walioiuliza. Kwa hiyo mimi ninaomba tuendelee Mheshimiwa usisimame, naomba tuendelee.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe.Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kuweza kutupa nafasi ya kukaa kama Kamati ya Matumizi, ili kuweza kupitisha hoja ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, kwa hiyo Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando, ili tuweze kumaliza hoja iliyo mbele yetu, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa naomba kuwahoji, wale wote wanaowafiki hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kwa kuwa pia Mhe. Waziri alitoa hoja kuhusiana na bajeti yake naomba pia hoja hiyo iamuliwa sasa hivi. Wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Ardhi wanyanyue mikono yao, wanaokubali, wanaokataa, waliokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU N01 WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA

Kifungu N0101

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba muongozo wako, wakati bodi zote au mamlaka nyingi kutokana na sheria hii ya *Water Act Nam. 4* ya mwaka 2006 inamtaka Mhe. Waziri atuletee ripoti hapa ya matumizi ambayo tayari yamefanyiwa *auditing* kama ilivyokuwa *CAG* na yeye vile vile. Sasa tulikuwa hatuoni hapa hata tukitaka tuhoji hatujaona ripoti ya Mhe. Waziri aliyotuletea au hatujaona ripoti yoyote hatuwezi kupiga buti kujua matumizi haya.

Nakuja tena kwenye kitabu hiki katika ukurasa wa 24 Mhe. Waziri anasema Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 5.1 kutokana na mauzo ya maji ya shughuli nyengine hadi kufikia Machi imekusanya shilingi Bilioni 1.9.

Mhe. Mwenyekiti, tunaona maongezeko mengi yameongezeka, mikato mingi ya maji imeongezeka na hizi pesa tunaziona kidogo sana. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba muongozo wako nini cha kufanya.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumjibu lile swali la mwanzo ambalo amesema hajaona ripoti ya mapato na matumizi ya mwaka uliopita, lakini naomba niseme tu kwa sababu ripoti ya matumizi mara zote nafikiri *CAG Report* wameiona na wameona jinsi wizara yangu matumizi yalivyokwenda na ilipatiwa hati safi. Kwa hiyo, mimi niombe tu kwamba kama hiyo nyengine ambayo anaitarajia basi itakuja kwa utaratibu wake wakati ukifika.

Pia alizungumzia suala la maji ambalo amesema mapato madogo ile 5.1 na 1.9. Nilieleza pale vizuri na nikawaambia kwamba, kutokana na wananchi kuwa hawajahamasika pamoja na jitihada kubwa ambayo sisi kama ofisi tunazichukua kama Mamlaka ina jukumu la kutoa elimu katika vipindi mbali mbali na mikutano mbali mbali, kuwapitia wananchi mmoja mmoja ndani ya nyumba, lakini bado mwamko ni mdogo na nitawaomba Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu, tushirikiane nao wao ndio wenye wananchi, ili waone umuhimu wa kuongeza mapato hayo basi kuhamasisha pia wananchi wao kupitia mikutano mbali mbali ndani ya maeneo yao, ili tuweze kuongeza mapato hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kusema kwamba, jitihada tutachukua na bado tutaendelea kwa kushirikiana na wao, ili tuweze kuongeza mapato.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nina *experience* ya miaka mitano na huu wa sita katika Baraza hili, lakini sijawahi kuona ripoti ambayo imeletwa. Vile vile anasema atatuletea ripoti hiyo muda wake ukifika, lakini hapa imetaka "*The Minister shall lay before House of Representative..."* ni *annual report*, hapa ndipo tunapofanya, *annual report* zote ndipo zinapokuja. Hili Baraza lako ndilo linalopitisha mapato na ndio linaloidhinisha matumizi ya wananchi. Sasa sijui muda wake utafika lini.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hatukufahamiana na Mhe. Mohamed Said Mohamed, alipokuwa akizungumza nilifikiri alizungumzia *Internal Auditing Report*, lakini kumbe anazungumzia kitu chengine, anataka ripoti ya wizara. Nataka kumhakikishia kwamba mimi toka nimeingia nafanya kazi ya maji lakini sikuhangaika na bajeti, anataka ripoti ya mamlaka.

Mimi nimuombe Mheshimiwa nikitoka hapa, naomba tupitishe bajeti halafu nitawataka watu wangu wa mamlaka wanikabidhi ripoti na hatimae nitaliandikia Baraza ripoti halafu Baraza litakupatia. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimemfahamu vizuri sana lakini ni jambo la kuchekesha sana huwa ninasema siku zote, leo nabadilisha kauli yangu. Juzi nilisema watu hawako makini, lakini nataka kusema hili ni Baraza la wananchi na chombo kikubwa katika Zanzibar hii kinachotunga sheria na sheria hii sikuitunga mimi ya mwaka 2006 hata mimi sijaingia Barazani, leo tunasema nitaileta.

Mhe. Mwenyekiti, nataka tuendelee lakini nina nia kubwa kweli lakini nitaitangaza huko mbele. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ningemuomba basi waziri akaipitia hiyo sheria ili akaona hiyo *requirement* ya sheria ikoje halafu baadae Baraza linaweza likatekeleza kupitia utaratibu huo. Tuendelee.

Kifungu N0101 Ofisi Kuu Pemba 40,000,000
Kifungu N0107 Idara ya Ardhi na Usajili

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa uchangiaji wangu wa jana nilisema kuna watu wameshachoka kufanya mazoezi kupanda ngazi na kushuka na ukizingatia pengine ni miaka miwili na sasa hivi ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani hati zao zimefikia hatua gani. Mhe. Waziri akasema kuna madudu nikamuomba anambie kuna madudu gani, ili atutajie tupate kuyajua madudu ya wizarani kwake ni nani na nani mfanyaji na hatua gani kachukua kama Mhe. Waziri. Kuna watu wameshachoka na muda mrefu nao ni wawekezaji wazalendo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe alilizungumza hilo katika suala lake la awali lakini ninachotaka kumhakikishia na kumwambia ni kwamba sisi baada ya kuona na nimeshalisema hapa, kuna mambo mengine ambayo sio ya wizara yangu na mengine ndani ya wizara yangu. Tutatoa hati kwa mujibu wa utaratibu, tutatoa hati kwa mwenye haki, lakini hatutotoa hati bila ya kufanyia uhakiki na bila ya kuhakikisha kwamba yule tunaempa tunampa kwa usahihi bila ya kuanza kuendeleza migogoro. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mhe. Waziri mpya wa wizara hii si mlaumu mimi anavyofanya

ndivyo kuangalia na kuhakiki. Basi baada ya mwalimu wangu kunipa mawaidha, naomba tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nachangia nilipeleka kwa maandishi kuhusu wananchi wangu wa Welezo palikatwa viwanja ukipandisha juu pale Jeshini *opposite* ... Walipokata viwanja serikali iliwaambia wakati huo itawapa viwanja vyengine; swali langu ni lini serikali itawapa viwanja vyengine wale wananchi wa jimbo langu ambao walipewa viwanja kabla.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nakiri na nakubali kwamba ofisi yangu ilitoa viwanja katika eneo analolisema na sina taarifa sahihi, lakini ninachoamini kama wako waliokatiwa viwanja na wakapimiwa na alishaniambia alileta kwa maandishi, wakapimiwa ambao hawakupewa viwanja vile baada ya jeshi kusema lile eneo haliwezi kutumika kwa maeneo ya makaazi basi waje ofisini wizara yangu ipo kwa ajili ya kuhudumia watu, ipo kwa ajili ya ku-*solve* matatizo kama hayo. Kwa hiyo, mimi naomba wale wote waliolipa ambao wana risiti zao mkononi basi waje ofisini kwangu na nitazungumza nao na kuondoa huo mgogoro.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa haya ni mapato tunamalizia, lile suala la Mhe. Mohamed Said Dimwa lilihusiana na mapato ndio maana niliruhusu, nilihisi kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa na jambo jengine na Mhe. Hassan Khamis Hafidh, lakini naona mnakamata vifungu vya mapato badala ya vya matumizi.

Kwa hiyo, tusubirini mpaka kwenye vifungu vya matumizi halafu ndio tuzuie, lakini atakuwa keshajibiwa sasa hivi Mhe. Hassan hatanyanyuka tena. Tunaendelea.

Kifungu N0107 Idara ya Ardhi na Usajili	5,508,000,000
Kifungu N0109 Mahakama ya Ardhi	5,400,000

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kila aliyefika Mahakama ya Ardhi anajua kuwa hili jengo halifai, N08 Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti: Mapato?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haya yatakuja mbele huko.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu N0109 Mahakama ya Ardhi	5,400,000
Kifungu N0113 Idara ya Upimaji na Ramani	

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohammed Said una *issue* na mapato au vipi. Mheshimiwa naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahaa, ndio sawa sawa.

Kifungu N0113 Idara ya Upimaji na Ramani	380,000,000
Kifungu N0118 Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar	46,600,000
Jumla Kuu:	**6,100,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU N01 - WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA

Kifungu PN0101	Program Kuu ya Mipango na Utawala wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
Kifungu SN	

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa leo asubuhi nilitaka kupata ufafanuzi juu ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu Kisiwa cha *Latham Island* ambayo ni Fungu Mbaraka, na hiyo ilikuwa na mgogoro mkubwa ambao hata Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Peter Pinda alisema Kisiwa cha Fungu Mbaraka ni cha Tanzania Bara. Sasa kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili kwa kipindi chote lilikuwa limetamka tamko la kusema Fungu Mbaraka imo ndani ya Zanzibar kwa zaidi ya miaka mia hata Tanganyika haijazaliwa, nataka nipate tamko la serikali litolewe rasmi la kusema Kisiwa hiki ni cha Zanzibar. Sikuridhika na majibu aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Nchii, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya ziada kutokana na maelezo ya ndugu yangu Mhe. Mohammedraza Hassanaali. Naelewa ukereketwa wake wa kusimamia haki za Zanzibar na napenda nimpongeze sana. Napenda nirudie kusema mbele ya Baraza lako tukufu hili kwamba Kisiwa cha Fungu Mbarak ni eneo la Zanzibar, kimo katika mipaka ya Zanzibar na hakina utata wowote. Hata wanasheria wetu

wakuu walipokutana jambo hili halikuwapa tabu katika mazungumzo yao wote wanaamini kwamba hili ni eneo la Zanzibar.

Jambo ambalo linaendelea ni kwa sababu huko nyuma kuanzia mwaka 1968 suala la mafuta na gesi asilia ilikuwa jambo la Muungano mpaka hivi karibuni mwaka 2015 wakati sheria iliyopitishwa na Bunge ikatoa nafasi kwa Zanzibar kuweza kushughulikia masuala yake ya mafuta na gesi asilia. Ndio maana tutaleta sheria Mhe. Mwenyekiti, hapa Barazani itakayoonesha na itakayoelekeza namna gani tutafanya shughuli zetu za utafutaji wa mafuta, namna gani tutagawa *blocks* zetu na kadhalika.

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa aelewe kwamba hatua za serikali mbili tumeafikiana vizuri na shughuli itakwenda vizuri na Zanzibar itachimba mafuta yake kila katika eneo linalohusu Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, taarifa zilizokuwepo kwamba ni kuwa na haja ya sehemu mbili kukaa kitako katika kujadili jambo hili na kama taarifa tupewe ambao walikaa pande zote mbili. Kwa hivyo, sikuona haja ya kukaa Zanzibar na ndugu zetu Bara kwa jambo hili ambalo hata Tanganyika haikuwa imezaliwa, Tanzania Bara. Sasa leo tunakuja kuambiwa mwaka 1968 tumekuja kusaini katiba kwamba mafuta yako chini ya Muungano, sasa na dhahabu iwe chini ya Zanzibar?

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo bado sijaridhika ninachotaka kupewa tamko. Kwa sababu hapa kuna kitalu cha saba na cha nane kilishatolewa na Tanzania Bara bila sisi kushirikishwa huo ushahidi ninao.

Sasa unaposema hiki cha Zanzibar halafu hekalu namba saba na nane ishachukuliwa na ndugu zetu wa Tanzania Bara halafu tisa, 10 tunavyo, tunataka tupate uthibitisho tunakaa, tunakaa na nani!

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini la pili kukushukuru wewe kwa hekima na busara kubwa unayotuonesha katika uendeshaji wa kikao chetu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri maelezo aliyoyatoa Mhe. Mohammedraza Hassanaali kuhusiana na suala zima la Kisiwa cha *Latham* au maarufu kinaitwa Fungu Mbaraka. Kuhusiana na suala la umiliki, naamini sote humu hatuwezi kuvutana, sote tunajua kwamba kisiwa hiki ni milki na mali ya Zanzibar. Lakini kuna jambo ambalo tunapaswa tujiulize kwamba kwa nini tunafika pahala

ikawa tunaulizana kisiwa hiki kama kinamilikiwa na Zanzibar au kinamilikiwa na upande wa pili wa Tanzania Bara.

Kisiwa hiki kipo muda mrefu kama vilivyo visiwa vyengine duniani na muda mrefu kimekuwa kikifanyika shughuli za uvuvi kwa wavuvi wanaotoka pande zote mbili; wale wanaotoka upande wa Zanzibar na wale wanaotoka upande wa Tanzania Bara kwenda kufanya madago na shughuli zao za uvuvi na uchumi kwa wakati wote ambao wamekuwa wakifanya harakati hizo.

Kwa mara ya kwanza lakini kwa mara ya kwanza kisiwa hiki kimeanza mivutano katika miaka ya 1990 na sote tunajuwa miaka ya 1990 ukirudi nyuma kutoka mwaka 1968 mpaka 1977 upande wa Tanzania Bara kilianzishwa chombo cha kusimamia na utafutaji wa mafuta na rasilimali yaani TPDC. Baada ya kuanza Shirika lile la TPDC ndipo ikaanza sasa kutafuta maeneo kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za utafutaji wa mafuta na rasimali nyengine zilioko chini ya ardhi. Sasa miaka ya 1990 wakati Zanzibar inahanganika kutafuta njia za kiuchumi ndio jambo hili likaanza kuja kwa sauti ya juu.

Mhe. Spika, sote tukiri kwamba nchi yetu tumeungana baina ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara na mwaka 1968 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha sheria hii inayohusiana na masuala ya mafuta na mengineyo hayo ikawa ni sehemu ya mambo ya muungano. Miaka ya 1970 baada ya kuanzishwa TPDC maana yake chombo cha muungano kilikuwa nia TPDC ambacho kilikuwa kina dhamana ya kutafuta suala zima la mafuta na katika utafutaji, kwa bahati nzuri au bahati mbaya eneo hili la Fungu Mbaraka likaangukia katika mtawanyo wa ugawaji kwa mapande ya ardhi kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na hivyo ikaonekana sehemu ile inamilikiwa na upande wa Tanzania Bara, kwa sababu moja tu kwamba chombo ambacho kilikuwa kipo kisheria ni TPDC ambacho kinamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, lakini jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa busara zao viongozi wetu mwaka 2015 jambo hili limeonekana kwa mapana makubwa sana na busara kubwa iliyotumika kwa viongozi wetu, kwa kuona kwamba pamoja na kwamba hatujakamilisha zoezi la upatikanaji wa Katiba Mpya ambayo itaweza kuweka mambo vizuri zaidi busara za viongozi ikaona kwamba tutunge sheria. Baada ya kutungwa sheria ikabainisha wazi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na uwezo na haki kisheria kutafuta maeneo na utafutaji wa mafuta na rasilimali kwa upande wa Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa ina haki ya kutafuta na kuendeleza maeneo ya uchimbaji wa mafuta na mengineyo kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, na kuthibitisha hili ni kwamba hata wenzetu wa TPDC miaka ya 1990 walipowapa Kampuni ya *SHELL* ya Uholanzi, Kampuni ya *SHELL* ilishindwa kufanya uendelezaji wote katika ma-*block* yote yale ambayo yalikuwa yanamilikiwa au ki-jeografia yalikuwa yako katika upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, nimthibitishe tu Mhe. Razza kwamba Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar asiwe na khofu na nimuombe tupitishe kifungu hiki, kesho kutwa Mwenyezi ajaaliye Serikali tutakuja nayo Sheria inayosimamia masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta, aje atoe michango yake katika sheria ile. Imeeleza maeneo ambayo yatakuwa yanahitaji uchimbaji kwa maana kwamba zile *block,* tutagawa sisi wenyewe, ukubwa wa *block,* maeneo yote.

Mhe. Spika, jambo kubwa la mwisho Mhe. Mwenyekiti ambalo nilitaka kulisema kwamba tusiyachanganye mambo sana tukaja tukajisahau, kwamba jiografia tutakuwa tuna maeneo yetu ya kimipaka. Katika mfumo wa kilimwengu unapozungumza katika msingi wa kidola tutakuwa tuna mipaka ya Tanzania, tunachokizungumza hapa Fungu Mbaraka kijiografia na kisheria katika utaratibu na utafutaji wa uchimbaji wa mafuta utakuwa ipo katika milki ya Zanzibar hili halina utata. Sasa tukijizonga kutafuta mengine tutaingia kwenye mambo ambayo hayatakuwa na msingi.

La mwisho tu nimalizie tu nimuombe sana Mhe. Razza tupitishe fungu hili, *concern* zako katika ugawaji wa maeneo ziweke tutakuja na sheria, tutakuja kugawana ma-*block*, eneo hili la Fungu Mbaraka tunakuthibitishia Serikali kwamba itaendelea kubaki kuwa mali ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Mohammedrazza Hasanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima ya komredi mwenzangu Mhe. Gavu na kauli ambayo ameitoa hapa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, inshaalah naomba tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, najua nilikurupuka lakini mimi kifungu changu kilikuwa utawala na maendeleo ya rasilimali watu. Kwa hiyo nafikiri hapa nilizungumza juu ya swali zima la mahitaji au maslahi ya wafanyakazi wa *ZECCO.* Nilisema sana kuhusu swali hili lakini sijapata jibu langu hata moja, sasa nilikuwa nipate majibu baada ya majibu niweze kupiga buti kama sijaridhika nayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe kama ifuatavyo: Wala hana haja ya kuzuiya ila nilikuwa sikufika kumjibu. Huyu bwana alizungumza kuhusu masuala ya wafanyakazi, lakini ninachotaka kukwambia ofisi yangu kupitia Shirika la Umeme linatambuwa tatizo la

wafanyakazi hawa na jitihada kubwa tumefanya ya kufuatilia katika Taasisi mbali mbali zinazohusika na utumishi wa umma, na hatua iliyofikiwa hadi sasa ni ya kuwa kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma, miaka yao ya uajiri wa muda utazingatiwa, watakapofanyiwa mafao yao watakapofikia umri wao wa kustaafu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumefuatilia sana hata mimi nilivyoingia mara ya kwanza katika mkutano wa *ZECCO* hili walilizungumza na nimelifuatilia na mimi bado najuwa kutokana na utaratibu na kiwango kilipofikia basi Idara husika inalifanyia kazi. Naomba niseme Mheshimiwa ili kwa faida ya wengine na wananchi wasikie. Kwa sababu viwango vya mishahara vinatafautiana sana baina ya Serikali baina ya mashirika haya; pia Serikali kupitia utumishi wa umma wameweka utaratibu sasa hivi, wameleta sheria ya kuleta viwango ili tafauti kubwa isikuwepo na ndio maana tuna-*delay* kidogo lakini linafanyiwa kazi, mimi binafsi limelichukuwa kwa *effort* yote na nimewahakikishia wafanyakazi wa *ZECCO* kwamba tutalifanyia kazi jibu lake litapatikana mara tu tutapokuja hapa na kumaliza haya matatizo na ninaamini Mhe.Haroun analifanyia kazi vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Diwani, kabla hujaendelea ningewaomba watendaji wa Mhe. Waziri wa Ardhi, waruhusiwe, wapo tayari eh! basi hamna tabu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, mimi bado sijaridhika nayo. Kwa sababu sheria inapotungwa inakuwa nje ya muda au ndani ya muda, sasa hivi sheria bado haijatungwa ya kuratibu hilo zoezi zima la mishahara, sasa hawa watu wanafanya kazi muda huu, wanahitaji muda huu, sasa itakapokuja sheria ndio hapo tutakuwa na nguvu ya kuibadilisha, lakini kama hii sheria haijatungwa na ukitilia maanani kwanza imekuwa ni ahadi ya muda mrefu ya Mhe. Rais, hii inaonesha wazi kwamba kuna *some elements* za dharau kwa Rais, kwa sababu hizi ahadi ameshatoa zaidi ya mara tatu ya kuwa waongezwe mishahara, ina maana Rais hili suala yeye halifahamu, kama kuna sheria inakuja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana ndugu yangu Mhe. Abdalla na masuala yake. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nilipokuwa ninatoa maelezo nikiunga mkono hoja hii ya Waziri, kwamba kupitia Kamisheni ya Utumishi wa Umma imetoa miongozo kwa mashirika na Taasisi zinazojitegemea ili kuweza kufanya marekebisho ya nyongeza hizo za mishahara. Mhe. Waziri, ameeleza hadharani hii imechukuliwa ili kusiwe na tafauti kubwa kati ya Watumishi waliopo Serikalini na Taasisi zake hizi ambazo zinajitegemea au mashirika

yanayojitegemea. Kwa hiyo muongozo upo ambao unatakiwa ufuatwe na kama kuna tatizo lolote kwa Shirika au Taasisi zinazojitegemea ukiona kuna matatizo ya msingi hayapati ufumbuzi katika level hiyo ya Taasisi ama ya Wizara basi Serikali kupitia Kamisheni ya Utumishi wa Umma milango iko wazi liletwe jambo hilo litajadiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka nimuhakikishie tu Mhe. Abdalla kwamba tutakaa na Waziri muhusika na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili la *ZECCO* ili tuone ni kwa namna gani tatizo lipo na lipate ufumbuzi, ili haki ya kila mmoja wetu iweze kupatikana. Naomba uvute subra hili tutalishughulikia kwa ukamilifu wake, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mheshimiwa, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa hiyo ninaomba *time limit* lini tutakaa tuweze kulimaliza hili swali, baada ya hapo mimi nitaunga mkono vyenginevyo sitaunga mkono.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hili suala la *ZECCO* limechukuwa muda mrefu sana kushughulikiwa na Kamisheni nakiri hilo na Kamisheni yetu imeshafanya kazi kubwa sana Mheshimiwa, na imeshaandaa mapendekezo ya utaratibu mzima wa malipo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kwa hiyo naamini kabisa hatutochukuwa siku nyingi suala hilo, kwa sababu suala si la *ZECCO* tu ni la Taasisi mbali mbali ya Mashirika ya Umma ambayo zinajitegemea, kuna matatizo mbali mbali ambayo tumeyaangalia tumeyaona na tayari hivi sasa kwenye meza yangu pana ripoti za aina hiyo. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa tuendelee nakuhakikishia kwamba Kamisheni yetu itafanya kazi ya ziada kuhakikisha suala tunaliharakisha na likamilike haraka iwezekanavyo na haki yao watapata kama ilivyopangwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mheshimiwa. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Utumishi ninataka *exact date* miezi sita, miezi mitano au mwaka kwani simple mimi nitakubaliana na hilo, lakini kwa kunambia kwa sababu hizi ni lugha za Serikali siku zote tutafanyam, tutakaa, tutaangalia, anipe *exact date* ah! baada ya miezi mitatu, mimi nitakuwa na nguvu baada ya miezi kuja kumuhoji tena.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, najuwa Serikali inakwenda kwa utaratibu wake vile vile. Mhe. Mwenyekiti, na hiki ni chombo kikubwa sana, mimi siwezi kuahidi kwamba kesho kesho kutwa itapatikana, masuala haya yana

technicality zake vile vile, kuna utaratibu wake na mambo yake, hatuwezi kwamba leo tutasema kesho itawezekana, lakini sisi ni viongozi tumekula kiapo kwamba tutatekeleza wajibu wetu na namuhakikishie Mheshimiwa yeye pamoja na wengine wote, kwamba jambo hili mimi mwenyewe linanigusa sana kwa sababu hawa wafanyakazi siku nyingi washaniambia washakuja mpaka kuniona mimi, nitahakikisha kwamba suala hili tunashirikiana kikamilifu na Mheshimiwa kama ana maelezo zaidi ninamuomba atafute wakati aje ofisini kwangu nitamuonesha kila ambacho kinahitajika, ili aridhike.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, umeshamaliza mara tatu Mheshimiwa, ndio kanuni hairuhusu inabidi tupige kura. Wale wote ambao wanakubaliana tuendelee wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi kwa *front benchers* wote Waheshimiwa Mawaziri kuwasili kwa wingi leo, nawapongeza sana. Vile vile, kwenye hotuba yangu nilizungumzia na nilichangia swali la Mhe. Waziri, aje anijibu ni *lease* ngapi zimefutwa katika Wizara yake kimakosa na waliofuta ni nani na hatua gani mpaka sasa hivi wamechukuliwa. Lakini jibu lililokuja kwa mama angu sio zuri sana sijaridhika nalo, nazungumza kidogo kidogo kwa sababu mama angu ninazungumza naye. Sasa naomba tu kidogo anijuulishe anijibu. Kwa sababu mimi hapa nilipo nina *lease* mbili zimefutwa kimakosa ninazo, haya.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Muwakilishi wa Jimbo la Chaani kama ifuatavyo. Nimemjibu *lease* zake zimefutwa tokea mwaka 2013/2014 nikazitaja kwa majina, nimejibu kumi na saba, inawezekana Mhe. Mwakilishi alikuwa hayupo au alikuwa amelala.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, inawezekana saa nyengine haya makofi inakuwa inamfanya mtu asipate kusikia, naomba anapozungumza watu wasipige makofi mpaka tutakapomaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa msishangirie mpaka...

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: eh! kwa sababu anazungumza na huku makofi!

Mhe. Mwenyekiti: Sasa tunaendelea na *issue* hii, Mhe. Waziri kajibu kwamba alikujibu kikamilifu itakuwa hukuwepo au ulikuwa unazungumza wakati jawabu ilipokuwa ikitolewa na kuna kama mara mbili nilitahadharisha kwamba jamani msikilizeni Waziri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ah! inawezekana binaadamu nilikwenda Msikitini na ndio jambo muhimu kuliko hili, lakini kwa kuwa nina vipande kama kumi na nne nitamuachia aendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa tayari watu watatu wameshakamilika. Mheshimiwa naomba ukae, Mheshimiwa naomba utoke nje, Mheshimiwa naomba utoke nje.

Kifungu FM010101	Programu Ndogo ya Mipango, Sera za Ardhi, Maji, Nishati, Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi	173,067,000
Kifungu FM010102	Programu Ndogo ya Utawala wa Maendeleo ya Rasilimali watu	808,112,000
Kifungu FM		

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati mimi ninachangia nilizungumzia suala la moja limeshajibiwa la *Latham* (Fungu Mbaraka) lakini nilikuwa nazungumzia suala la magharibi ya Pemba kuhusiana na *block* ya *Tanga Basin* ambayo wamepewa Taasisi ya.. iko magharibi inaitwa *Tanga Basin* iko magharibi ya Pemba. Lakini pia kwa mujibu wa nilipokuwa ninasoma nilimshauri pia Mhe. Waziri, kuhusiana na sheria ya *petroleum* nafikiri ni *Act* ya 2015 kwenye kifungu cha 65 *declaration of location* kilizungumza kwamba:

65(1) "*Where petroleum has been discovered in a block within an exploration area, not being a block that is or is included in a location, or is not a block that has a side in common or touches the discovery block, PURA (Petroleum Upstream Regulatory Authority) may upon reciept of a request from the licence holder declare by a notice published in the Gazette -*

(a) discovery block and not more than eight adjoining blocks within the exploration area that are nominated by the holder; and..."

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa ninataka kujua kuhusiana na *block* hili la Tanga ambalo ipo magharibi ya Pemba. Tumepata majibu mazuri kuhusiana na kusini ya Unguja, kuhusu *Latham* nimeridhika na naamini Serikali itafanya, nilikuwa nataka maelezo kwenye mpango mzima kwa sababu, kwa mujibu wa mpaka wa Zanzibar wa kihistoria kutoka hata katika Katiba ya 1963, hiyo Katiba ya bandia hukuti mpaka wa Zanzibar magharibi ya Pemba. Sasa ninataka kujuwa kuhusu hii Tanga *Basin* wakati *Petroleum Act* ya 2015 imeshataja maeneo yote na kuna hiki kifungu cha 63 kinatufunga sisi. Je, katika mpaka ule pale wa maji ni rasilimali ile ipi tunagawana sisi baina ya sisi na ndugu zetu wa Bara.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Simai, anisikilize vizuri, mkoa wetu mmoja wa kusini huyu, na kuna lugha tunaweza tukafahamiana mimi na yeye vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema kwanza ninataka nikuhakikishie kwamba ma-*block* haya hayajagawiwa kwa mtu yeyote mpaka sasa hivi. Sheria ndio tutaileta hapa, tutaipitisha hapa, tukisharidhika ile sheria mapendekezo yote mtayaona kwenye sheria, na hapo baadaye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ndio itakayoamua sasa *block* hii apewe na mpaka uko wapi mpaka wapi, kwa sababu yale ambayo yako chini ya Jamhuri ya Muungano ndio sasa hivi ya Bara yako Bara na Zanzibar yatakukwepo Zanzibar. Tupitisheni sheria kwanza kesho kutwa halafu tutaona mambo yanavyokwenda, tusifanye haraka sasa hivi tukatoa maamuzi, kwa sababu hatuwezi kugawa ya Tanga, kugawa ya wapi ya Pemba sasa hivi, kwa sababu bado hatupitishi sheria kwanza baadaye tutakwenda kuyagawa hayo ma-*block* kwa mujibu wa taratibu ilivyo, cha Zanzibar kitabakia Zanzibar cha Bara kitabakia Bara.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi sifa yangu kitu kimoja, ninapoongeza kitu ninapoongeza kitu inakuwa sibahatishi. Hizi *exploration* nimezungumza hapa mwanzo kwenye *activity map* ambayo ninayo hapa ya TPDC *Tanzania Petroleum Development Corporation* na ukenda ukasoma *Petroleum Act* ya 2015 ambayo alisaini Mhe. Rais Kikwete mle ndani kuna vifungu vinazungumza kabisa ni nani atakuwa na dhamana ambayo ni TPDC na upande gani wa muungano. Ukitafuta jina la Zanzibar kwenye ile sheria yenyewe na maeneo mangapi yametajwa basi unaweza kuhesabu ambayo ina vifungu karibia mia moja na thalathini mbili.

Sasa ukisoma katika vile vifungu vyote hata ukisoma katika Section 65 inapozungumza hii *Petroleum Act* ukiniruhusu mimi nikusomee ambayo hapa

inasema moja kwa moja, kwa ruhusa yako Mwenyekiti, kwa sababu hii inabidi niipeleke, kwa sababu nimeitafuta kwenye mtandao imenichukuwa kama masaa sita mpaka nikaipata.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kimsingi kuna bahari ya Tanga magharibi ya Tanga, kuna sheria ambayo imezungumzia juu ya *Petrolium Act* ya 2015 ambayo haitaji jambo lolote kuhusu Zanzibar na tunasubiri sera ya mafuta na gesi, ije hapa na huku wenzetu wameshaweka hii sheria, hasa mipaka ya Zanzibar hata ukiitafuta ya maji ya kusini mwa Zanzibar tunajuwa kama ni Fungu Mbaraka na Waziri amesema, kwa upande wa magharibi kutoka hii Tanga *Basin* mpaka wetu uko wapi?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Afya kwanza.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kujibu majibu ya nyongeza kidogo. Kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambae aliniwezesha kupata nafasi ya kuchangia mchango mkubwa katika *technical committee* ya sheria hii inayoletwa Barazani.

Naomba nimwambie ndugu yetu Mhe. Simai Mohammed Said kuwa katika sheria hiyo inayoletwa kuna kifungu kinatamka wazi kwamba kuanzia tarehe itakayosainiwa sheria hiyo ndiyo itaanza kutumika. (*Makofi*)

Ma-*blocks* yoyote yaliyotolewa kabla ya hapo aliyepewa mtu yeyote ikiwa ....., *SHELL*, ikiwa mwengine yeyote watakuwa *nonvoid* hayatofanya kazi.

La tatu katika sheria hiyo hata mimi mwenyewe niliuliza masuala mengi tu na kuridhishwa na wataalamu kuna kila *line of demarcation* ya *boundaries* zote baharini na *blocks* zote kwa *GPS*, yaani ile *GPS* baina ya Tanga na Zanzibar hatuwezi kugombana. Ile *GPS* ipo *very clear* mita moja. Kwa hivyo mipaka nayo iko *very clear*. (*Makofi*)

Ningeomba sana Mhe. Simai pamoja na Wawakilishi wote kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuvumilia kidogo ile sheria ikaletwa. Ninaomba sana Mhe. Waziri namuomba pia atoe semina, maana ile sheria ni pana. Itolewe semina maalum kwa Wajumbe wa Baraza lako Mhe. Mwenyekiti. Masuala yote hayo tutaweza kuyajibu kwenye semina, kwa sababu semina hiyo sisi tulipewa kama Mawaziri na tulishiriki na *technical committee* tuliwauliza masuala mengi sana.

Kuna Mawaziri hapa leo wapo ambao waliuliza masuala mengi sana na wengine ambao hawapo pamoja na sisi hapa huku mbele, lakini na wao pia waliuliza masuala mengi.(*Makofi*)

Kwa hivyo, ni hilo lakini kuna kila *line of demarcation* baina ya Tanga, baina ya Mombasa mpaka Kusini huko kwenye Mtwara, hiyo *latham Island* imetajwa hicho kisiwa cha Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali anachokitaja pia kimetajwa. (*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya muda na nimefurahi kwamba ametoa rai nzuri tutapata semina. Mimi nilitaka nisaidie Baraza kutokana na suala hili.

Sasa mimi nilikuwa na suala moja kuhusiana hapa hapa na issue *Tanga Basin* na kutokana na hivi vifungu vya sheria iliyopitishwa ya *Petroleum Act* ya 2015 ambayo niliyoipitia. Kwa upeo wangu mimi sioni kwamba *Tanga Basin* kuna eneo mule ndani, sisi kama Zanzibar tutakuwa tunajua wapi sisi kwa upande wetu.

Pia, baada ya maelezo aliyotoa Mhe. Waziri ambayo aliyozungumza ninataka nitoe rai ni kwamba serikali itambue kwamba mipaka yetu sisi kabla ya sheria ya *Law of the Sea* haijafika.

Mipaka yetu inajulikana kutokana na huko nyuma tulikotoka kabla ya muungano. Sasa ninachotaka kusema kwamba watakapokuja kutuletea hicho tueleze moja kwa moja mipaka yote pamoja na Tanga mpaka *Latham Island*, tujue maeneo yote yatatoka wapi *based on* kabla ya muungano maeneo yaliyokuwepo.

Naomba tuendelee baada ya hapo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naomba kumuuliza tena au kumkumbusha tena mama yangu Waziri kwa suala nililolizungumza la Makangale, wale mayatima waliodhulumiwa eneo lao na aliyefanya vile nilitaja jana Mhe. Mansour na ninarejea tena.

Sasa nilichouliza kwamba walifika hatua mpaka Kamati ilifika ya Baraza la Wawakilishi kwamba wachague viwanja viwili warejeshewe haki yao, kwa kuwa kule kwenye eneo walionyang'anywa kumejengwa hoteli kubwa ya *five*

star, ili tusiwakorofishe wageni na *investors,* tukaamua kukubali eneo jengine. Wale vijana wakenda wakaambiwa wachague sehemu mbili Pemba na Michamvi. Wamechagua Michamvi Baraza lako na wizara yako ikajibu kwamba sawa wameshakubali.

Leo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anakuja kusema kwamba ni kweli alikiri Michamvi lakini baadae ikajulikana kama ile Michamvi ....

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mheshimiwa maana yake hii *microphone* inakuwa ina matatizo. Kanuni hazituruhusu kuwataja watu ambao hawamo humu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Lakini mtu ambae aliyefanya wizi asitajwe.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh!

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mtu aliyefanya wizi.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! wewe ungeelezea tu wasifu tu Mhe. Waziri mwenyewe angefahamu ni nani. Kwa sababu unayemtuhumu, maana yake itakuwa ni tuhuma na hana uwezo wa kuja kujitetea hapa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Aah! yeye hakutaja na mimi nilichozungumza kwamba Waziri aliyefanya kosa hili ni Waziri Mansour, kamwibia huyu mtoto.

Mhe. Mwenyekiti: Ndiyo huwezi kumtaja kwa jina Mheshimiwa, Kanuni hazituruhusu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Alikuwa Waziri haya, lakini imeshafahamika. Sasa ninachoomba mimi kwamba eneo lao watapewa lipi jengine kwa muda gani anihakikishie, kwa sababu eneo hili ameshakiri kama ...

Mhe. Mwenyekiti: Ninafikiri suala lako limeeleweka Mheshimiwa ngoja Mhe. Waziri akujibu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Kidogo Mhe. Mwenyekiti, hajafahamu bado,...

Mhe. Mwenyekiti: Eeh!

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Kidogo hajafahamu bado

Mhe. Mwenyekiti: Unatuhutubia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Haya basi wacha anijibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chaani ndugu yangu Nadir wala asipate *pressure*, kila wakati ninamwambia wizara yangu ipo kwa ajili ya kutumikia watu.

Kama ana wasi wasi na jawabu ambalo nimelitoa, naomba ofisi yangu ipo aje na ushahidi, aje na makatarasi, lakini bado ninaendelea kusema hatutatoa *lease* kwa shindikizo wala hatutatoa hati kwa shindikizo. Tutatoa hati kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa sheria.

Naomba anikubalie.

Mhe. Nadir Abdul-lafit Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaamini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar tunawatendea haki kwa watu wote na ninamuamini sana Mhe. Waziri. Hawa watoto ni mayatima walifika wakati kuambiwa wachague sehemu mbili, wamechagua Michamvi. Matokeo yake wizara yake ile ile inakuja kusema ile Michamvi ina mtu mwengine, sijui Manji, sijui nani.

Sasa kwa nini asitaje tu kama atawapa eneo nyengine. Mimi ninataka kujua hiyo kauli tu kwa sababu imeshafika mpaka kwenye Kamati ilikuwa imeshaamua kwamba wapewe hayo maeneo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mbona inaonekana kama umeshachupia kitu chengine sasa hivi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Eeh!

Mhe. Mwenyekiti: Ninaona kama umesharukia jambo jengine sasa hivi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ataa! ni hilo hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza kulikuwa na tuhuma ya mtu aliyekuwa waziri kwenye hiyo hoja yako.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ndiyo nimemfahamisha kwenye hotuba yangu niliyozungumza nimerudia. Nililizungumza suala hili kwamba waziri fulani ndiyo kafanya kitu fulani. Lakini hoja kwamba ile ardhi watapewa ipi ile baada ya ile ya Michamvi aliyepewa mtu.

Kwa sababu ile ya Michamvi waliambiwa watapatiwa wao au Pemba, wakachagua Michamvi. Wakajibiwa kwamba sawa mushapewa Michamvi. Leo ninakuja kuambiwa Michamavi ina mtu mwengine. Sasa watapewa ipi baada ya hiyo. Mimi ninataka kujua tu ipi watapewa, sina mambo mengi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, namuomba tena Mhe. Nadir kwamba Wizara yangu ipo, kwa sababu ya wao na kwa watu. Kama kuna mgogoro, kama kuna tatizo wizara yangu ipo, watendaji wangu wapo, *documents* zipo, waje na *documents* zao, ma-*file* yapo. Hata mimi nitasoma nitaona haki iko wapi.

Nimesema wizara yangu bado haitomdhulumu mtu, haitomnyima mtu haki yake kama anayo. Lakini hatutatoa haki kwa masindikizo na kwa dhuluma.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakubaliana na hayo mambo wala sitaki kumtaabisha. Leo nilikuwa nimeshasema namsamehe hasa nikae kimya lakini masuala mengine itabidi tuyatetee.

Labda anihakikishie tu hili analijua au halijui.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kakwambia uchukue *documents* kama unazo na ushahidi, nenda nazo wizarani mutalifanya kwa pamoja wewe na hao wananchi wanaolalamika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wacha tuendelee hamna tatizo.

Kifungu SN 010103	Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Ardhi Maji, Nishati na Mazingira, Mabadiliko ya Tabia ya Nchi Pemba	Shs.1,361,267,000/-
Jumla		**Shs.2,342,446,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU PM 0102 Programu Kuu ya Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

Kifungu SN 010201

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yangu ya barua ambayo nimepeleka kwa Mhe. Waziri kule Dole kuna wakulima ambao muda mrefu walikuwa wanadai hati zao. Na hati 148 zilitolewa na Idara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo.

Suala langu ninaomba hawa wakulima 78 ambao hawajapata hati zao. Ni lini watapatiwa kwa sababu hoja hii ni ya muda mrefu na Mhe. Balozi ndiyo aliyekuwa analisimamia hili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Bubunu ambaye ni Mwakilishi wangu Mhe. Masoud Abrahman Masoud kama ifuatavyo.

Yeye mwenyewe amekiri kwamba hati 148 tayari zimeshatolewa kwa wananchi na kuna hati 78 ambazo hazijatolewa. Kama nilivyozungumza mwanzo, hatutoi hati kama karatasi; tunatoa hati kuangalia vigezo, tunatoa hati kutokana na utaratibu, tunatoa hati kuangalia kuhakikishi yaani kufanya *verification*. Kwa hivyo inawezekana pia hazijatolewa hati hizi, inawezekana sina hakika tutakwenda tutakwenda ofisini, inawezekana ukiangalia Dole maeneo mengi ni maeneo ya kilimo.

Tusije tukatoa hati halafu tukajikuta eneo lile ni kilimo. Lakini naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi wangu hivi kwamba hili ninalichukua, nitakwenda tena kulifanyia kazi, mimi nitalisimamia chini ya Kamisheni yangu ya Ardhi kuhakikisha hizi hati 78 kwa nini hazijatolewa.

Kama hati hizi zipo katika maeneo ya kilimo na maeneo ya serikali. Maana yake hati hizi hatutoweza kuzitoa. Lakini kama ni maeneo sahihi ya kawaida ya kuwapa watu, basi kwa utaratibu unafaa na kwa sheria iliopo hati hizo watapatiwa.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, eneo hili ambalo tayari wakulima hawa 178 walipatiwa hati ni kauli ambayo kaitoa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mbele yao kuwa hati hizo watapatiwa. Sasa sina uhakika kuwa

wana haki au hawana. Lakini kwa ule Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliahidi kuwa hati hizi zitapatikana na wote watakabidhiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kukuhakikishia kwamba ahadi ile imetolewa basi sisi tutatimiza ahadi kwa mujibu wa utaratibu na sheria ziliopo.(*Makofi*)

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee wakati kakubali.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa tunaendelea. Eeh! Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninaamini mama yangu ana majibu mengi leo hajawahi kuyamaliza kama alivyosema.

Sasa nilizungumzia suala la *Petrol Stations* ambazo zilizojengwa hasa katika maeneo ya watu chini ya nyumba. Ni vigezo gani hasa wizara yake inakubali *Petrol Stations* zile na zinazidi kujengwa *Petrol Stations* mpya za mafuta. Ni vigezo gani wanatumia kuwaruhusu hawa kujenga *Petrol Stations* na wakati ni hatari hasa kwa wananchi wa mazingira ya chini.

Sehemu nyingi zile *Petrol Stations* zimezunguka kwenye nyumba za watu. Ni vigezo gani wanatumia kuwaachilia kujenga.
Mhe. Mwenyekiti: Vituo vya mafuta *(Petrol Station).*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi pamoja na kwamba kwenye suala lako la awali halikuwepo hilo suala, lakini naomba nikujibu kama ifuatavyo.

Utaratibu wa kujenga vituo vya mafuta wataalamu wanapima, wanaangalia, wanatathmini, wanafanya *analysis* za kutosha wakisha ndiyo wanatoa vibali. Na sura inayotoa vibali ninafikiri sehemu changa lakini wale waliokuwa wakitoa vibali, walikuwa wakifanya *analysis* za kutosha na mara nyingi kwa sababu kukua kwa makaazi utakuta eneo *Petrol Stations* zimepewa kibali mwanzo, lakini ujenzi wa makaazi umekuja umefuata *Petrol Station* baadae. Na hili ndilo linalotuathiri sana na kuna sehemu nyingi ambayo yamepewa vibali, kwa vile walichukua muda mrefu kujenga, walianza kujenga hawajamaliza lakini wananchi waliwafuata katika maeneo ya pale.

Lakini ushauri wako tunaupokea na watu wangu wataalamu wangu watafanya kazi, lakini zile *Petrol Stations* ambazo wananchi wanazifuata naomba na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi, kwa sababu ni watu wenu, kwa sababu ni wananchi wetu. Basi naomba muwape elimu kwamba kukaa pale karibu na vituo vya petroli vina athari kubwa. Kwa hivyo athari zile muweze kuziainisha ili wananchi wetu baadae wasije wakapata madhara ya kiafya.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti, mimi nimeridhika sana na majibu ya mama yangu, lakini ninachomshauri kwamba waangalie kwa sababu Zanzibar hatuna *fire* za kutosha.

Shells moja inaporuka nyumba mia nne zitakuja kuungua, wawe makini sana kwenye suala hili ni muhimu sana, bado hatupo *more advance*. Hatuna *helicopter* ya kuzima moto labda magari yatoke mjini na sehemu nyenginezo.

Ninamuomba sana suala hili lisiendelee kwenye vijiji. Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti.

Kifungu SN 010201	Programu Ndogo ya Utawala wa Ardhi	Shs.1,065,460,000/-

Kifungu SN

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi wakati ninachangia nilizungumzia suala la Jimbo langu la Tunguu kuhusiana na miji mipya. Ninashukuru Mhe. Waziri amezungumza mengi kwa ukubwa, lakini nilitaka kauli yake katika mpango mzima wa kutoa viwanja kwenye eneo la Tunguu katika *units* zote. Maeneo ambayo maombi ya wananchi ambayo tayari kule ni maskini walikuwa wanakaa kule haweshi kuhamishwa. Atapokea maombi yatakuja kwake nitayaleta.

Pia tuna tatizo kama nilizungumza eneo la Binguni. Lakini pia nilikuwa naomba eneo la Jumbi kuitwa Jumbi Jaani, naomba liachwe kuitwa Jumbi Jaani, jimbo langu siyo jaani, watafute jina jengine.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hizi nyengine ni taarifa. Ninafikiri hili moja ndiyo unapaswa kujibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Eeh! sijafahamu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Zile za mwisho kule kubadilisha jina sijui, jibu hilo la mwanzo tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu kwamba na ninaomba nilipokee hili lakini ninafikiri majibu mazuri tushazungumza mimi na yeye na tushakubaliana. Kuna moja nimeshalijibu hapa lakini na mengine tushakubaliana mimi na yeye.

Naomba Mhe. Mwakilishi aridhike na tuweze kuvipitisha vifungu, ili anipitishie kifungu na baadae tuweze kuyatimiza yale ambayo umeuliza.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa wizara yake inafanya mambo mengi ninataka kauli yake ya kuwa utaratibu wa kutumia Jumbi Jaani.

(Hapa kulisikika milio ya simu)

Mhe. Mwenyekti: Mheshimiwa kuna *interference* hapo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Hapana mimi sina simu, labda *internet*.

Mhe. Mwenyekiti: Ni hiyo hiyo *internet*.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza kuwa wizara yake ina mambo mengi na eneo la Jumbi Jaani utaratibu wa ndani ya kisheria na kikaazi wanaita Jumbe Jaani. Sasa nilikuwa naomba kwamba hilo Jumbi Jaani ninapokea kauli yake hapa itasimama wataita Jumbi kwa jina jengine, hilo jaani litaondoshwa.

Ninataka hilo tu jibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi nimepokea ushauri wake naomba nilifanyie kazi. Kwa sababu siwezi kutoa jibu la moja kwa moja isipokuwa nitalifanyia kazi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi nilimpelekea Mhe. Waziri *survey* iliyofanywa na *world plan survey* ambayo utafiti ule umebaini kwamba Zanzibar, walipofanya *survey* ya nchi za

visiwa Zanzibar ni miongoni mwa kisiwa kinachotumia vibaya ardhi yake na inatuongezea umaskini.

Sasa mimi nina wasi wasi kwamba kwa utaratibu tunaotumia ardhi Zanzibar tutakosa hata pa kuzikiwa na hata kukosa kibustani kidogo cha kujenga. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri. Je, wizara yake ina mkakati gani mahususi kwa kutumalizia hapa Zanzibar hasa Unguja kadhia hii ya matumizi mabaya ya ardhi na majenzi holela ambayo yana hatari kwa maisha yetu na ardhi ndiyo uti wa mgongo wetu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Welezo.

Mhe. Mwenyekiti: Nikikaa hapa ninakuwa ni Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mimi ninafikiri kama alinifuatilia vizuri katika hotuba yangu na wakati ninajibu masuala na ninaomba pia Mhe. Mwakilishi aangalie vipindi kwenye redio na kwenye televisheni, sasa hivi mji tulivyoupanga na sasa hivi tukasema tunaanza na ng'ambu tuitakayo. Tumetoa kauli mbiu hiyo kwa sababu ya kuona hii athari ambayo yeye anaizungumza. Na hapa wakati wakati ninazungumza nimesema tunaanza na mitaa hii ya mjini kuja ng'ambu hii ya Makadara, Gulioni, Rahaleo, Mwembeshauri lakini tumeanza kupiga hiyo kampeni wananchi wameshaanza kuwa *aware*.

Naomba na Waheshimiwa Wawakilishi wawe *aware* kupitia vyombo vya habari na ile mikutano yetu. Lakini sasa hivi tunaanza kutumia matumizi mazuri ya ardhi kwa kutumia nafasi ndogo kwa kuweza kuweka wakaazi wengi. Na kampeni hiyo tumeianza na inshaallah Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake atatujaalia tuweze kufanikiwa na huko mbele na maeneo mengine hayo pia tutafikia, ili tuweze kuwa na matumizi mazuri ya ardhi.

Pia ninawaomba tena Waheshimiwa Wawakilishi waweze kutusaidia katika kuhamasisha wananchi yao katika maeneo kama ninavyosema kila wakati Wizara yangu ni wizara *touchable* ambayo inamgusa kila mtu na kila mtu ana hisia tukishirikiana kwa pamoja tutaweza. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya dada yangu Mhe. Waziri kaizungumzia ng'ambu tuitakayo *well and good*.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii ya matumizi mabaya ya ardhi sasa hivi hayapo ng'ambu tuitakayo, yapo Nyarugusu huko, Tomondo, Magharibi "A" na "B", ndiko mji unavyoendelea kujengwa na unaendelea kuchafuka, unaendelea kuwa mbaya na Zanzibar sasa hivi hasa Unguja itakwisha kutokana na hali ya matumizi ya ardhi yaliyokuwepo kule. Namuomba asahau huku ahamie Magharibi "A" na "B" kuifanyia kazi, vyenginevyo ni aibu. Mji wa Kwahani leo umepangika kuliko Nyarugusu, Mji wa Kwahani umejengwa miaka 50 au 60 iliyopita nyuma, hii ni aibu kwa nchi yoyote duniani kwamba mji wa zamani ni mzuri kuliko mji mpya. Naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu SN010202	Programu Ndogo ya Upangaji wa Mji kwa matumizi ya ardhi	1,021,398,000
Kifungu SN0		

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sasa Jumbi Jaani inaitwa Jumbi Mji Mpya, nimeletewa memo nimefurahi sana. Kwa hivyo, tunampongeza Mhe. Waziri. Kwa hivyo, karibuni sana Jumbi Mji Mpya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati nachangia nilizungumzia suala la wawekezaji ambao wanakua na *lease* zao tayari wameshawekeza, wanakuwa na *lease* ambayo inaitwa *consolidate lease* na wako wengine zimefutwa futwa zimefanywa madudu ambayo hayafahamiki. Mhe. Waziri nimeomba kwa sababu hujapata muda wa kulizungumzia hili, nilikua nataka kauli yako kwamba utalifuatilia na utahakikisha kwamba hawa wawekezaji hatuwafanyi kuwa wanyonge, wanakuwa mabalozi wazuri wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilimjibu vizuri tu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu ndugu yangu Mhe. Simai Mohammed kwamba hili tumelipokea na tutalifuatilia kama tulivyolizungumza.

Mhe. Simai Mohammed Said: Namna hiyo, bomba sana tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu SN010203	Programu Ndogo ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi	188,214,000
	Jumla Kuu	**2,275,072,000**

Kifungu PN0105 Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati

Kifungu SN010

Mhe. Mwenyekiti: Nitamuanza Mhe. Viwe Khamis Abdalla, halafu atafuatia Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata. Yule kule nyuma nani, halafu Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, nilipokua nikichangia katika wizara hii nilimtaka Mhe. Waziri aje anipe maelezo kuhusu tatizo la maji linalosumbua katika Shehia ya Kiuyu Kigongoni.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika majibu yake alinijibu akasema kwamba tatizo hili kwenye kisima hiki limemaliza, lakini Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kisima kile kimetengenezwa, lakini tatizo la maji katika Shehia ya Kiuyu Kigongoni bado lipo. Hata leo asubuhi nilizungumza na mwananchi wa Shehia ile na ameniambia bado tatizo la maji lipo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipatie maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Mjumbe amekiri kwamba kisima kimetengenezwa na ameambiwa na mwananchi wake kwamba tatizo bado lipo. Mhe. Mwenyekiti, tatizo la kutoka maji masaa 24 kwa mamlaka sasa hivi hatujawa na uwezo nalo. Lakini nimuhakikishie Mhe. Viwe Khamis kwamba maji yatapatikana kwa mgao na kwa sababu ya matumizi mengi ya umeme, lakini pia upatikanaji wenyewe wa maji unatoka chini, kwa hivyo bado hatuwezi kuu- *force* kwa masaa yote. Lakini naomba nikiri kwamba kisima kimetengenezwa na kazi imefanyika na wananchi wake wataendelea kupata maji.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nibishane na Mhe. Waziri, lakini kwa kuwa wananchi wale wa kijiji hiki cha Kiuyu Kigongoni zamani walikua wanapata maji ambayo yalikuwa yanatoka Ole, kwa nini sasa hivi zisifunguliwe zile bomba ambazo zilifungwa baada ya kupatiwa kisima hiki wananchi wale zikarudi kama yalivyokua yanatolewa zamani maji haya.

Namuomba Mhe. Waziri aniambie atakubaliana na mimi, ili azungumze na wafanyakazi wake wa Pemba wanaohusima na mamlaka hii ya maji, ili wananchi hawa waweze kupatiwa maji kutoka kisima ambacho kipo Ole.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe, anasema kwamba mwanzo walikuwa wanapata maji ya Ole, sina uhakika sana kwa sababu sijatembelea hayo maeneo, lakini naomba nikubaliane naye. Pia namuomba Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine ni lazima wakubali kwamba, mahitaji yanazidi na mji unakua, kwa hivyo yale ya mwaka 1964 tulikua watu laki 300,000 na sasa hivi tuko karibu watu milioni moja. Kwa hivyo, kutegema kisima cha mbali kwenda eneo jengine, wakati mwengine pia miundombinu hairuhusu. Lakini naomba nikubaliane naye na mimi nilichukuwe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimepata shida kidogo alivyoniambia kwamba *cock* zinafungwa. Kwa hivyo, suala hili naomba nilichukuwe na nilifanyie kazi, kwa sababu umewagusa watumishi wangu. Lakini ninachokuomba tuipitishe bajeti na hili nitaendelea kulifanyia kazi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, lakini kama tatizo hili bado litakuwepo nitaendelea kulipeleka mbele.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Viwe Khamis. Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nampongeza Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anayofanya katika maeneo mbali mbali. Lakini pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi mdogo tu naomba Mhe. Waziri anipe. Najua katika kujibu majibu hakuwahi kunijibu, nimeridhika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika kitabu hiki kwenye ukurasa wa 30 katika jadweli namba 6 *paragraph* ya kwanza, kilieleza maeneo mbali mbali ambayo yamesambazwa mabomba yamaji. Mimi nikamwambia katika maeneo hayo moja wapo ni Kwarara. Kwa bahati nzuri au mbaya, naweza kusema bahati mbaya hakuna bomba hata moja lililotandikwa, kwa sababu mimi katika maeneo yangu nimefanya utafiti wa kutosha.

Je, Mhe. Waziri tukimaliza bajeti hii atakuwa tayari kufuatana na mimi kwenda kumuonesha katika maeneo hayo kwamba hakuna mabomba, na kama hakuna ataniahidi vipi juu ya kutandazwa mabomba hayo, ili wananchi waondokane na adha wanayopata kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe kwamba tutakuwa tupo tayari na

hapa alipokuwa kanukuu yeye ni kwamba matengenezo ya miundombinu. Sasa kwa kifupi tupo tayari. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa busara iliyotokea baadae. Lakini kama anasema miundombinu, miundombinu ndio mabomba na kila kitu. Naridhika tuendele. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru. Nilipokuwa nikichangia kwa maandishi nilizungumza kusikitishwa sana na kisima cha Mpendae Kwa Binti Amrani, viongozi wa jimbo lile walichimba visima akiwemo Mbunge na Mwakilishi na kuweka kila kitu, lakini umeme tukawaachia *ZAWA* na operesheni yake, lakini kisima kile ni kipindi kirefu zaidi ya miezi mitatu kimekaa hakitoi maji na Ramadhani hii tunawapa shida wananchi. Naomba basi *commitment* ya serikali nini watafanya au kimewashinda tuendeshe wenyewe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu visiwa vilivyochimbwa na mwakilishi na mbunge. Kusema kweli wizara yangu tunawapongeza sana kwamba walichimba visima na tunatamani tuliwekee miundombinu, ili wananchi wafaidike. Lakini bado tuna ukwasi wa mafungu, kwa hivyo kila hali itakavyoruhusu, nataka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tutaendelea kufanyakazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia fursa hii, naomba nimuombe hapa hapa kwamba zile fedha za jimbo kwa safari hii naomba azielekeze kwenye mfuko wa maji, ili tuweze kufanyakazi ipasavyo visima hivi kwa faida ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, na mfuko wa jimbo wala hauna tatizo, ndio maana tukachimba visima vile zaidi ya vitatu ili kuwaondolea adha wananchi wetu. Lakini tumefanya kila kitu wao waendeshe tu kile kisima. Lakini mpaka kuendesha tu kisima basi serikali inashindwa na kisima kile wamekuja kutoa ile mashine. Watuambie wataweza kuinunua au hawawezi basi tutainunua wenyewe.

Vile vile tukishanunua wenyewe watuachie na mamlaka hiyo, iwe Mamlaka ya Mpendae basi isiwe mamlaka ya kuja kukusanya pesa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kusema kwamba sisi tuko hapa kwa sababu ya wananchi na nasema kila hali ikiruhusu tutakuwa tunahudumia visima kimoja baada ya chengine,

kwa sababu visima viko vingi mno. Kwa hivyo, kama bado utaweza na umesema mfuko wa jimbo hauna tatizo, basi bado tutashirikiana na uongozi wa Mpendae ili kuhakikisha wananchi wanapata maji, na mimi naamini kwa kupitia kwako kada wa Chama cha Mapinduzi, lakini ukiwa mheshimiwa, basi tutashirikiana Mhe. Mjumbe ili hivyo visima vifanye kazi. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Sasa nataka kauli tu aniambie yuko tayari kuanzia kesho ili tusiwape tabu wananchi wa Mpendae, ili kesho tufuatilie tuone kama wizara haina pesa basi mimi nitatoa tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, *Inshallah,* naomba nimshukuru sana Mhe. Dimwa kwa upendo wake kwa wananchi wake, lakini kwa upendo wake ndani ya wizara. Mimi niko tayari, pamoja na kwamba nikimaliza kazi yangu ya bajeti, na nikitoka hapa hata leo basi nitamkabidhi watendaji wa kuweza kushirikiana naye ili kuhakikisha kwamba wanakamilisha huduma hii. *(Makofi)*

Kifungu SN010501	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati	48,978,195,000
	Jumla Kuu	**48,978,195,000**

Kifungu PN0106 Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi

Kifungu SN01

Mhe. Mwenyekiti: Haya, nitaanza na Mhe. Simai Mohammed Said Mpakabasi, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi nilikua na swali moja tu, kwa sababu kwa kweli Mhe. Waziri alikua anakuja ku-*summarise* jana na sikupata taarifa zake, kwa sababu hakupata muda wa kutosha, ila nilikua na suala moja.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kwa hisia sana kwamba suala la haya mabadiliko ya tabia nchi lipo na linakuja kwa nguvu. Kutokana na upepo uliopiga mwaka huu inaelekea mazingira haya pia yataendelea mwaka ujao. Kwa hivyo, nilikua nataka kujua tu Mhe. Waziri kutokana na haya yaliyojitokeza, je ni utaratibu gani atakaotumia kwanza kuwahamasisha

wavuvi, lakini pia wakazi wetu wanaoishi katika *Coastal Areas* usalama wao utakuwa uko vipi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Samahani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe anaweza kurejea, kuna kitu sijakipata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Rudia kidogo.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kwamba mwaka huu tulipata upepo mkali, tumeona mazingira, mafuriko nakadhalika ambayo inawezekana na inaaminika kwamba hizi hazikuwa ni mvua za masika, na inawezekana mwaka ujayo na miaka tunayokwenda mbele kutajitokeza hali kama hii ya mvua kubwa, mafuriko, pia na wavuvi wetu kuweza kuathirika pamoja na wananchi wanaioshi katika maeneo ya pwani kwenye *Coastal Areas*.

Sasa nilikua nataka kufahamu Mhe. Waziri kwa kupitia idara yake ya mazingira na haya ni mabadiliko ya tabia nchi. Atajipangaje yeye ili kuhakikisha kwamba moja kwa moja anatoa elimu ya kuweza kuwasaidia, ni njia gani atatumia, je atatumia namba ya simu kwa ajili ya wavuvi. Kwa sababu, kwa mfano kwenye Idara ya Maafa wanayo 114, lakini wavuvi wanapokua baharini kutoa taarifa zao inakua hatujui na wakati mwengine hawana taarifa. Sasa hawa wote pamoja na *Coastal*...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nina wasi wasi kwamba suala la mazingira analo mheshimiwa, lakini jambo unalolieleza liko zaidi kwenye *meteorology* ambayo inaangukia kwenye *portfolio*. Naam, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ni kweli suala analolizungumzia Mhe. Mjumbe, linahusiana na suala la *meteorology*, kwa maana ya utabiri wa hali ya hewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida wenzetu wa utabiri wa hali ya hewa wanakuwa wanadesturi ya kutoa taarifa zao kwa mifumo minne. Wana mfumo ule wa utabiri wa mwaka, utabiri wa miezi mitatu, utabiri wa mwezi na utabiri wa wiki, baadae wa mwisho kuna utabiri wa siku.

Kikawaida huwa wanatoa taarifa rasmi kwa utaratibu wa miezi mitatu na hapa huwa ana- *coordinate* na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na

baadhi ya sekta za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kuhusiana na vituo vyao vilipo. Kwa hapa cha Victoria na cha Kizimbani.

Sasa wanapotoa taarifa zao kuna *Coordinate Centre* kwa maana kwamba masuala yanapotokea baharini, basi moja kwa moja wana-*deal* na *ZMA* kwa ajili ya kuvitaarifu vyombo pamoja na sekta ya uvuvi, yanapokuwa masuala ya kilimo, basi wanavitaarifu vyombo husika vya Idara ya Kilimo kwa ajili ya kujiandaa na miongo. Sasa *concern* ya Mhe. Mjumbe kwamba mwakani labda kutakuwa na matarajio haya.

Mhe. Mwenyekiti, nimuhakikishie tu Mhe. Mjumbe kwamba tayari utaratibu huu serikalini upo, tunapokea taarifa kutoka kwa wenzetu katika mfumo wa miezi mitatu, mwezi mmoja na siku moja. Sisi tuseme tunamshukuru yeye kwa kutukumbusha, lakini tayari mfumo huu serikalini upo na taarifa hizi zinaendelea kufanyiwa kazi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nizidi kumpongeza Mhe. Waziri na kwa uwezo wa Mwenye Mungu bajeti yake sasa hivi itamaliza. Kwenye michango yangu nilizungumzia suala la mazingira. Nilizungumza kwamba Zanzibar tukisema tuweke mazingira safi tu, watu wengine bila ya marungu kama Punda hawendi.

Sasa namuomba Mhe. Waziri nilipendekeza ashirikiane na Mhe. Waziri wa Vikosi, watu wengi hawana ajira Zanzibar, basi waanze kutayarisha vikundi anayetupa taka wanamkamata analipa shilingi 30,000, shilingi 15,000 ya yule aliyemkamata na shilingi 15,000 inakwenda wizarani.

Basi hapa ndio usafi utakuwa hapa Zanzibar, lakini tukisema kwa mdomo mtupu bila ya vitendo vyovyote, basi itakuwa Zanzibar kila siku kuchafu. Naomba sana wizara hizi mbili zishirikiane, na watu wengi hawana ajira basi wawape kazi hizi kama nchi nyengine wanavyofanya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alisahau tu kuja kulizungumzia ndio nikasema nilizungumze au niliulizie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba sasa nimpe waziri mwengine, kwa sababu hili sasa pia ni jambo la *portfolio* tofauti. Mazingira sijui labda tuelimishwe tu. Mnapoita mazingira hasa mnakusudia nini, sio usafi wa mazingira, nafikiri ni vitu tofauti kidogo. Kwanza ngoja nimpe Mhe. Waziri wa

Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Nadir Abdul-latif, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, kwa suala lake ambalo ameliuliza. Ni kweli sisi kama wizara au sekta husika tumepitisha sheria namba 7 ya mwaka 2014 na tayari kanuni zake ziko tayari, hili ambalo amelisema tunahitaji mashirikiano ya wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Serikali kwa kupitia wizara yangu, tumejipanga kulitekeleza hilo kwa mfumo ambao Mhe. Nadir Abdul-latif anaupendekeza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana kwanza kamanda wangu wa Kaskazini kwa kusema kwamba yeye mwenyewe pia keshalifikiria hilo, na vile vile Kiswahili kigumu ndio maana nilizichanganya wizara mbili makusudi, kwa sababu mimi mwenyewe hii mazingira ilinichanganya ndio maana nikazipiga mbili, ahsante sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru, lakini niendelee kuishukuru sana wizara. Wakati nilipochangia kwa maandishi nilionesha wasi wasi wangu wa kuwa mabadiliko ya tabia nchi yametuathiri katika jimbo langu, kwenye eneo la Kilimani Pwani mpaka maji kuja karibu ya majumba na yale mabonde yaliyokuwa yakilimwa mpunga sasa hivi yameingia maji.

Nilitaka nijuwe Mhe. Waziri ana mpango gani, kwa sababu tulikwenda kupanda mikoko pamoja. Anampango gani wa kujenga ukuta katika eneo lile, ili maji yasiathiri majumba yale kwa haraka zaidi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naomba nimjulishe kwamba kama alivyokiri kuwa hatua ya awali ya kupanda mikoko tumeanza na tulishirikiana. Namshukuru sana kwamba hata yeye na wananchi wao walitoka katika kushirikiana na sisi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile taratibu za matayarisho ya kitaalamu zimo katika hatua ya mwisho kukamilika. Ni juzi tu tarehe 28/05/2016 wakandarasi wametembelea maeneo yale yote ya mradi, likiwemo eneo la Kilimani kama ni hatua ya mwisho ya matayarisho. Nafikiri watu wake kama walimuambia kwamba watu walikwenda, maana yake tulitoa taarifa kwa Sheha. Kwa hivyo, wanakamilisha makisio ya mahitajio yao yanayohusu kazi, ili mkandarasi

atakayekubalika kukabidhiwa kazi hiyo kwa maeneo hayo ikiwemo Kilimani na Kisiwa Panza, ujenzi huo unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2016.

Kwa hivyo, naomba nimtowe hofu Mhe. Mwakilishi, kazi inaendelea na tumejipanga kufanyakazi kwa uadilifu zaidi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri na nimpongeze sana pamoja na serikali yote kwa jumla kwa jitihada kubwa ambayo wanaanza kuchukua. Naomba tuendelee.

Kifungu SN010601	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi	3,860,473,000
	Jumla Kifungu	**3,860,473,000**
	Jumla Kuu	**57,456,186,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ilivyokua Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa sasa naomba iamuliwe. Wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Walikubali wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe nafasi hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri kwa namna alivyoweza kutulia katika kujibu hizo hoja, wakati wa kupitisha hivi vifungu.

Pia nimpongeze kwa kuweza kufanikiwa kupitisha bajeti yake. Sasa nimtakie utendaji mwema. Isipokua nitapenda kumwambia Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata aliomba mara baada ya kumaliza hizi shughuli hapa, afuatane na Mhe. Waziri. Spika, alimchagua kwa makusudi Mhe. Naibu Waziri ili afanye kazi

hiyo badala ya Mhe. Waziri. Ili sasa kumpa nafasi Mhe. Waziri kwenda kusimamia futari. *(Makofi/Vicheko)*

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwashukuruni na nyinyi nyote kwa pamoja kwa ushirikiano ambao tumekua nao katika kuziendesha hizi shughuli. Kwa hayo, machache naomba sasa niakhirishe shughuli za Baraza mpaka kesho siku ya Ijumaa, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 10:03 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 17/06/2016 saa 3:00 za asubuhi)